Mamlaka

Ya

Mwamini

na

A.L. Gill

Gill Ministries

www.gillministries.com

Vitabu vya A.L. na Joyce Gill

God's Promises for Your Every Need

God's Covenant Blessings for You

Destined for Dominion

Out! In the Name of Jesus

Victory over Deception

Nakala Katika Mwongozo Huu

The Church Triumphant
Through the Book of Acts

God's Provision for Healing
Receiving and Ministering
God's Healing Power

The Ministry Gifts
Apostle, Prophet, Evangelist,
Pastor, Teacher

Miracle Evangelism
God's Plan to Reach the World

New Creation Image
Knowing Who You Are in Christ

Patterns for Living
From the Old Testament

Praise and Worship
Becoming Worshipers of God

Prayer
Bringing Heaven to Earth

Supernatural Living
Through the Gifts of the Holy Spirit

Kuhusu Wabuni na Waanzilishi

A.L. na Joyce Gill ni wanenaji wajulikanao kimataifa, waandishi na walimu wa Biblia. Matembezi ya utume ya A.L. yamempeleka katika mataifa zaidi ya hamsini ya ulimwengu, akihubiria umati zaidi ya laki moja, moja kwa moja na kwa milion nyingi kwa redio na runinga.

Vitabu vyao vilivyouzwa pamoja na nakala viliuzwa zaidi ya milioni mbili Marekani. Maandishi yao, ambayo yametafsiri katika lugha nyingi, inatumika katika vyuo vya Bibliad na katika semina ulimwenguni.

Kweli zenye nguvu na zibadilishazo maisha za Neno la Mungu hulipuka katika maisha ya wengine kupitia huduma yao ya mahubiri, kufundisha, kuandika na sinema na pia kanda za kusikiliza.

Utukufu mkuu wa uwepo wa Mungu huonekana katika kusifu na kuabudu kwao katika semina wakati waamini hugundua jinsi ya kufanyika waabudio wa kweli kwa Mungu. Wengi wametambua mbinu mpya na yenye busara na ujasiri kupitia mafundisho yao kuhusu mamlaka ya mwamini.

Gill wamefundisha waamini kuingia katika huduma za kiasili walizopewa na Mungu wakiwa na uponyaji na nguvu mikononi mwao. Wengi wamejifunza kuwa wa asili wanapoachiliwa na kutenda katika karama zote tisa za Roho Mtakatifu maishani mwao na huduma kila siku.

A.L. na Joyce wana shahada za *Master of Theological Studies*. A.L. pia amepata shahada ya *Doctor of Philosophy in Theology* kutoka *Vision Christian University*. Huduma yao imewekwa juu ya Neno la Mungu, inaangazia Yesu, ina nguvu katika imani na hufundishwa katika nguvu za Roho Mtakatifu.

Huduma yao ni kielelezi juu ya moyo wa Baba wenye upendo. Mahubiri yao na mafundisho huambatana na upako wenye nguvu, ishara na miujiza, na uponyaji na wengi wakianguka katika nguvu za Mungu.

Ishara za uamushwo pamoja na kicheko kitakatifu, kilio mbele za Bwana na kuonekana kwa utukufu wa Mungu na nguvu zionekanazo na wengi wanaohudhuria mikutano.

Kwa Walimu na Wanafunzi

Mafundisho haya yenye nguvu kuhusu Mamlaka ya Mwamini yataleta ufunuo juu ya utawala ndani ya kila mwanafunzi. Watajifunza jinsi ya kukoma kushindwa na kuanza kushinda katika kila vita maishani. Waamini watatiwa moyo kupitia ufunuo mpya kuwatambua katika Yesu Kristo. Mafunzo haya yataleta ujasiri na ushindi katika maisha ya wanafunzi.

Tungependekeza kabla ya kufunza kosi hii uweze kusikiliza na kuona kanda za sinema katika mfululizo huu na pia kusoma vitabu vya Masomo Yaliyopendekezwa. Kadri unavyosoma na kufahamu Neno la Mungu kuhusu mamlaka ya mwamini na vita vya kiroho, ndipo kweli hizi zitaweza kuingia rohoni mwako. Nakala hii basi itakupa mwongozo ili utumie unapoonyesha kweli hizi kwa wengine.

Mifano kuhusu maisha ya binafsi ni lazima kwa ajili ya mafunzo bora. Mwanzilishi ameacha haya kutoka kwa kazi hii ili mwalimu aeleze ustadi kutoka maishani mwake, au kutoka kwa wengine ambao wanafunzi wataweza kuhusiana nao.

Itakumbukwa kila mara kuwa ni Roho Mtakatifu ndiye amekuja kutufundisha katika yote, na kuwa tunapojifunza au kufunza, ni lazima tuwe kila mara tukiongozwa na Roho Mtakatifu.

Mafunzo haya ni bora zaidi kwa kujifunza binafsi au katika kikundi, shule za Biblia, shule ya Jumapili na makundi ya nyumbani. Ni vyema kuwa mwalimu na mwanafunzi awe na nakala ya kitabu hiki wakati wa masomo.

Vitabu vizuri vimeandikwa, kutiwa msitari, kutafakariwa na kutumika. Tumeacha nafasi kwa ajili ya maelezo na kunakili kwako. Mpangilio umewekwa ili uweze kurudia na kupata msaada na kutafuta sehemu tena. Mpangilio bora hurahihisha kila mtu, mradi tu asome nakala, awafundishe wengine yaliyomo.

Paulo alimwandikia Timotheo:

> **Hayo uwakabidhi watu waaminifu watakaofaa kuwafundisha na wengine. 2 Timothy 2:2b**

Mafunzo haya yameundwa kama kosi ya Biblia inayohuzisha katika utaratibu wa *MINDS (Ministry Development System)*, mbinu iliyoundwa kwa ajili ya mafunzo yaliyoandaliwa. Wazo hili limeundwa ili kuzidisha katika maisha, huduma na mafunzo ya usoni ya wanafunzi. Wanafunzi wa awali, kwa kutumia nakala hii, wanaweza kufunza wengine kosi hii kwa urahisi.

Orodha ya Yaliyomo

Somo La Kwanza	**Mtambue Adui Wako**	**7**
Somo La Pili	**Mamlaka Hapa Duniani**	**15**
Somo La Tatu	**Mpango Wa Hila Ya Shetani**	**23**
Somo La Nne	**Kisha Akaja Yesu – Mpango Wa Mungu**	**30**
Somo La Tano	**Yesu Alihudumu Katika Mamlaka**	**39**
Somo La Sita	**Kutoka Msalabani Hadi Enzini**	**45**
Somo La Saba	**Mamlaka Kurejeshewa Mwanadamu**	**52**
Somo La Nane	**Mbinu za Shetani Za Kisasa**	**62**
Somo La Tisa	**Kanisa na Mamlaka**	**69**
Somo La Kumi	**Funguo Za Ufalme**	**77**
Somo La Kumi Na Moja	**Jina La Yesu**	**85**
Somo La Kumi Na Mbili	**Ushindi Wa Vita Vya Kiroho**	**93**
	Mistari Ya Kukariri	**102**

Maandiko katika **Mamlaka ya Mwamini**
yametolewa kutoka **The New King James Version.**

Haki ya Mwandishi 2009

Masomo Yaliyopendekezwa Kwa Kosi Hii

Destined for Dominion, *na*
Out! In the Name of Jesus
Na A.L. Gill, Powerhouse Publishing

Somo La Kwanza

Mtambue Adui Wako

TUKO VITANI!

Vita

Kama Wakristo, ni lazima tutambue na kujua kuwa tunahusika katika vita. Mojawapo ya mbinu kuu za Shetani imekuwa kutufumba macho tusione hitilafu na pigano tulilo nalo, na kwa hivyo kutufanya kukosa ulinzi dhidi ya mashambulizi yake. Lakini Mungu ametupatia kila silaha tunayohitaji ili kuwa washindi kwa adui wetu!

2 Wakorintho 10:3, 4 Maana ingawa tunaenenda katika mwili, hatufanyi vita kwa jinsi ya mwili; (maana silaha za vita vyetu si za mwili, bali zina uwezo katika Mungu hata kuangusha ngome;)

1 Timotheo 6:12 Piga vita vile vizuri vya imani; shika uzima ule wa milele ulioitiwa, ukaungama maungamo mazuri mbele ya mashahidi wengi.

Ni muhimu kukumbuka kuwa silaha hizi si za kiulimwengu. Ni za kiroho.

Wengi wa waandishi wa Agano Jipya walitumia matamshi ya vita. Haya si majina ya utani tu, bali ni maelezo ya vita ambavyo tunahusika. Vita hivi ni sharti vifanyike katika ulimwengu wa kiroho.

Adui Wetu

Tuko chini ya uvamizi wa adui toka pande zote katika maisha na uhusiano wetu – katika:

- ➢ Jamii
- ➢ Kifedha
- ➢ Kazi
- ➢ Mawazo(akili)
- ➢ Mili (afya)
- ➢ Nyumbani
- ➢ Majirani
- ➢ Miji
- ➢ Mataifa
- ➢ Ulimwengu

Mojawapo ya mambo muhimu ya kujifunza ni kuwa vita vyetu si dhidi ya watu. Ni dhidi ya Shetani na mapepo yake maovu. Ni katika ulimwengu wa kiroho. Kuingia katika hitilafu na watu huleta usumbufu na kushindwa tu.

JE, ADUI WETU NI NANI?

Tukijua kuwa tuko vitani, ni muhimu kutambua adui wetu ni nani.

Je, adui wetu ni –

- ➢ Jamii zetu?
- ➢ Watu tunaofanya kazi nao?
- ➢ Serikali yetu?
- ➢ Fedha zetu?

Hapana!

Tawala – Mamlaka

Mamlaka – Nguvu za Kiroho

Mtume Paulo anaeleza kuhusu adui wetu kwa undani kabisa. Alitwambia kuwa vita vyetu si kati ya watu wanaotuzunguka. Alisema hatupigani dhidi ya mwili na damu.

Waefeso 6:12 Kwa maana kushindana kwetu sisi si juu ya damu na nyama, bali ni juu ya falme na mamlaka, juu ya wakuu wa giza hili, juu ya majeshi ya pepo wabaya katika ulimwengu wa roho.

Shetani

Petro aliweka wazi kuwa adui wetu ni Shetani

1 Petro 5:8 Mwe kiasi na kukesha; kwa kuwa mshiriki wenu Ibilisi, kama samba angurumaye, huzunguka-zunguka, akitafuta mtu ammeze.

Hila / Ujanja

Hila za Shetani ni mbinu zake, maarifa na mipango ya ujanja, anayotumia dhidi yetu. Ana mbinu ya kijeshi ya vita anayotumia katika kutushinda. Hata hivyo, kadri tunapogundua mipango yake, ni sharti tuwe waangalifu zaidi kuhusu silaha na zana za vita ambazo Mungu ametutengea kwa ajili ya vita. Zana hizi ni za kutukinga. Silaha ni za ushindi dhidi ya adui zetu.

Waefeso 6:11 Vaeni silaha zote za Mungu, mpate kuweza kusipinga hila za Shetani.

Onyo

- ➢ ***Uzingirwe na Yesu***
- ➢ ***Fahamu Mamlaka***
- ➢ ***Usije Ukazushwa na Ibilisi***

Tusije tukajawa na kutafakari juu ya Ibilisi, mapepo zake au mbinu zake. Badala yake, tujawe na Yesu. Tunapoweka macho yetu Kwake, tutatambua sisi ni nani ndani Yake. Tunapotambua uwezo wetu uliorejeshwa katika Yesu, ujasiri utashuka ndani ya roho zetu. Hatutamwogopa Ibilisi wala mbinu zake.

MUNGU ALIWAUMBA VIUMBE MALAIKA

Mungu Ni wa Milele

Mungu ni wa milele. Yeye amekuwepo na Yeye ni muumba wa vitu vyote.

Yohana 1:1-3 Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwa kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Huyo mwanzo alikuwako kwa Mungu. Vyote vilifanyika kwa huyo; wala pasipo yeye hakikufanyika cho chote kilichofanyika.

Yohana 1:14 Naye Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu; nasi tukauona utukufu wake, utukufu kama wa Mwana pekee atokaye kwa Baba; amejaa neema na kweli.

"Neno" ni Yesu.

Mungu aliwaumba Malaika

Kama Mwana wa Mungu, Yesu aliumba vitu vyote wakiwemo malaika. Hakuwaumba tu bali kwa kazi ya Mungu.

Wakolosai 1:16, 17 Kwa kuwa katika yeye vitu vyote vilivyo juu ya nchi, vinavyoonekana na visivyoonekana; ikiwa ni viti vya enzi, au usultani, au enzi, au mamlaka; vitu vyote viliumbwa kwa njia yake, na kwa ajili yake. Naye amekuwako kabla ya vitu vyote, na vitu vyote hushikana katika yeye.

Malaika Wana Mipango

Wakati Paulo aliorodhesha enzi, mamlaka, utawala na nguvu na uwezo, alikuwa akizungumzia juu ya malaika. Alitumia maneno yanayotaja kazi zao.

Zina vyeo tofauti-tofauti:

- ➢ Malaika Mkuu
- ➢ Makerubi
- ➢ Maserufimu
- ➢ Viumbe wanaoishi

Wana Kazi tofauti-tofauti:

- ➢ Enzi
- ➢ Utawala
- ➢ Mamlaka
- ➢ Nguvu

MUNGU ALIMUUMBA LUSIFA

Kwa vile tunajua kuwa Yesu aliumba vitu vyote, tunafahamu kuwa alimuumba Lusifa.

Cheo cha Lusifa cha Zamani

Cheo cha Lusifa cha awali kilikuwa cha hali ya juu na chenye heshima. Mojawapo ya cheo chake ilikuwa Nyota ya Alfajiri.

Isaya 14:12 Jinsi ulivyoanguka kutoka mbinguni, Ewe nyota ya alfajiri, mwana wa asubuhi! Jinsi ulivyokatwa kabisa, Ewe uliyewaangusha mataifa!

Ayubu 38:7 ...Hapo nyota za asubuhi zilipoimba pamoja, Na wana wote wa Mungu walipopiga kelele kwa furaha?

Maelezo Kuhusu Lusifa

Manabii Ezekieli na Isaya wanatupa mawazo juu ya maelezo kuhusu Lusifa.

- ➢ ***Mfano Bora wa Ukamilifu***
- ➢ ***Hekima Tele***
- ➢ ***Amekamilika Kiurembo***

Ezekieli 28:12b ...Bwana MUNGU asema hivi, Wewe wakitia muhuri kipimo, umejaa hekima, na ukamilifu wa uzuri."

- ➢ ***Amefunikwa na Johari***

Ezekieli 28:13a ... Ulikuwa ndani ya Adeni, bustani ya Mungu; kila jiwe la thamani lilikuwa kifuniko chako, akiki na yakuti manjano, na almasi, na zabarajadi, na shohamu, na yaspi, na yakuti samawi, na zumaridi na baharamani, na dharabu;

- ➢ ***Sauti Nzuri ya Kuvutia***

Ezekieli 28:13b ...kazi ya matari yako na filimbi zako ilikuwa ndani yako; katika siku ya kuumbwa kwako zilitengenezwa tayari.

Matari ni vyombo vya muziki. Filimbi ni vyombo vya upepo kama vile filimbi au zomari.

Isaya 14:11a Fahari yako imeshushwa hata kuzimu, Na sauti ya vinanda vyako.

Sauti yake ilisikika kama muziki wa kutamani.

➢ ***Asiye Lawama***

Ezekieli 28:15 Ulikuwa mkamilifu katika njia zako tangu siku ile ulipoumbwa, hata uovu ulipoonekana ndani yako.

Kazi yake Lusifa

Nabii Ezekieli aliandika kuhusu kazi ya Lusifa ya awali.

➢ ***Mlinzi wa Enzi***

Ezekieli 28:14 Wewe ulikuwa kerubi mwenye kutiwa mafuta afunikaye; nami nalikuweka hata ukawa juu yamlima mtakatifu wa Mungu, umetembea huko na huko kati ya mawe ya moto.

Hata wakati makerubi walipokuwa kila upande wa kiti cha rehema wakilifunika Safina la Agano (Kutoka 25:18-22), Lusifa alikuwa kando na Mungu katika nafasi ya heshima kuu. Kama Nyota ya Alfajiri au Mwana wa Alfajiri, alikifunika na kulinda kiti cha Mungu cha enzi na kuonyesha mng'aro na utukufu wa Mungu. Alikuwa ametakaswa kama makerubi mlinzi. Alipewa na Mungu cheo cha jukumu kuu.

➢ ***Kiongozi wa Sifa***

Kutokana na maelezo kuhusu sauti yake ya kimuziki, inaonekana kuwa aliwaongoza malaika wote katika sifa zao na kuabudu Mungu na kulinda kiti cha enzi cha Mungu kwa kukifunika kwa sifa na kuabudu.

VITA MBINGUNI – LUSIFA AANGUKA

Ilisababishwa na Kiburi / Uasi

Kuelewa uasi wa Lusifa, kuanguka na vita vilivyofuatia huko mbinguni, hutusaidia kuelewa umuhimu wa vita tunavyopigana sasa hapa duniani.

Ezekieli 28:15,17 Ulikuwa mkamilifu katika njia zako tangu siku ile ulipoumbwa, hata uovu ulipoonekana ndani yako. Kwa wingi wa uchuuzi wako watu walikujaza udhalimu ndani yako, nawe umetenda dhambi; kwa sababu hiyo nimekutoa kwa nguvu katika mlima wa Mungu, kama kitu kilicho najisi; nami nimekuangamiza, Ewe kerubi ufunikaye, utoke katika mawe hayo ya moto.

Moyo wako uliinuka kwa sababu ya uzuri wako, umeiharibu hekima yako kwa sababu ya mwangaza wako; nimekutupa chini nimekulaza mbele ya wafalme, wapate kukutazama.

Lusifa alikuwa mwema hadi alipoweka mawazo yake kwa urembo wake mwenyewe badala ya urembo wa Yule aliyemuumba. Kiburi kiliingia. Aliwaza juu ya mng'aro wake badala ya kuweka mawazo yake kwa mng'aro wa Mungu Mwenyewe.

"Nita Mapendekezo"

Palikuwa na pendekezo moja tu, mapenzi ya Mungu iliyotawala ulimwengu mpaka kiburi kikamwingia Lusifa.

Isaya 14:12-17 Jinsi ulivyoanguka kutoka mbinguni, Ewe nyota ya alfajiri, mwana wa asubuhi! Jinsi ulivyokatwa kabisa, Ewe uliyewaangusha mataifa! Nawe ulisema moyoni mwako,

Nitapanda mpaka mbinguni,
Nitakiinua kiti changu juu kuliko nyota za Mungu;
Nami nitaketi juu yam lima wa mkutano,
Katika pande za mwisho za kaskazini;
Nitapaa kupita vimo vya mawingu,
Nitafanana nay eye Aliye juu.

Lakini utashushwa mpaka kuzimu; Mpaka pande za mwisho za shimo.

Wao wakuonao watakukazia macho, watakuangalia sana, wakisema, Je, Huyu ndiye aliyetikisa falme; Aliyeufanya ulimwengu ukiwa, akaipindua miji yake; Asiyewafungua wafungua wake waende kwao?'

Mpaka sasa palikuwa pendekezo moja tu ulimwenguni – mapenzi ya Mungu. Katika kuasi, Lusifa alifanya kuchagua mapenzi yake kinyume na Mapenzi ya Mungu. Kama ilivyoelezwa katika 'Nita' zile tano za Lusifa, ujanja na kiburi chake uliendelea hadi kufikia kujaribu kumwondoa Mungu kwenye kiti cha enzi kule mbinguni.

Vita

Ufunuo Wa Yohana 12:7-10 Kulikuwa na vita mbinguni; Mikaeli na malaika zake wakapigana na yule joka, yule joka naye akapigana nao pamoja na malaika zake; nao hawakushinda, wala mahali pao hapakuonekana tena mbinguni.

Yule joka akatupwa, yule mkubwa, nyoka wa zamani, aitwaye Ibilisi na Shetani, audanganyaye ulimwengu wote; akatupwa hata nchi, na malaika zake wakatupwa pamoja naye. Nikisikia sauti kuu mbinguni, ikisema,

Sasa kumekuwa wokovu, na nguvu, na ufalme wa Mungu wetu, na mamlaka ya Kristo wake; kwa maana ametupwa chini mshitaki wa ndugu zetu, yeye awashitakiye mbele za Mungu wetu, mchana na usiku.

➢ ***Shetani na Malaika Watupwa Nje***

Ezekieli 28:16 Kwa wingi wa uchuuzi wako watu walikujaza udhalimu ndani yako, nawe umetenda dhambi; kwa sababu hiyo nimekuangamiza, Ewe kerubi ufunikaye, utoke katika mawe hayo ya moto.

Lusifa na malaika wake walitupwa nje ya mbinguni.

Matokeo ya Vita

➢ ***Theluthi Moja ya Malaika Walianguka***

Theluthi moja ya malaika walikuwa chini ya amri ya Lusifa na walianguka pamoja naye. Malaika wengine waliokuwa chini ya amri ya Mikaili na Gabrieli, walibaki waaminifu kwa Mungu.

Ufunuo Wa Yohana 12:4a na mkia wake wakokota theluthi ya nyota za mbinguni, na kuziangusha katika nchi.

Lusifa na "malaika wake" walitupwa chini duniani.

Ufuno Wa Yohana 12:9 Yule joka akatupwa, yule mkubwa, nyoka wa zamani, aitwaye Ibilisi na Shetani, audanganyaye ulimwengu wote; akatupwa hata nchi na malaika zake wakatupwa pamoja naye.

➢ ***Kubadilishwa Majina***

Majina ya Lusifa yalibadilishwa. Aliyekuwa na vyeo kama vile Mwana wa Alfajiri na vile vile Makerubi Aliyepakwa, majina yake yalibadilishwa na kuwa:

- ➢ joka
- ➢ nyoka
- ➢ ibilisi
- ➢ Shetani

Malaika waliokuwa chini ya uwezo wa Lusifa, wale waliomfuata katika kuasi, waliendelea na mipango yao ya enzi, nguvu, mamlaka, uwezo na viongozi, lakini majina yalibadilika kuonyesha hali yao ya kuanguka. Sasa walitambulika kama mapepo, ibilisi, mapepo mabaya.

➢ ***Kubadilisha Hali***

Hali ya Shetani ilibadilika kabisa.

Alikuwa:

- ➢ Nyota ya alfajiri
- ➢ Mwana wa Alfajiri
- ➢ Yeye aliyeongoza sifa na kuabudu
- ➢ Yeye aliyelinda na kuchunga kiti cha enzi cha Mungu

Alifanyika:

- ➢ mwovu
- ➢ fedheheshwa
- ➢ katupwa toka Mbinguni

Alipoteza:

- ➢ urembo wake mkuu
- ➢ nafasi yake kuu katika ufalme wa Mungu

Hali yake ilifanyika na kuwa:

- ➢ giza
- ➢ sura isiyopendeza
- ➢ ovu
- ➢ iliyojaa chuki

Haya yalikuwa matokeo ya dhambi zake za kiburi na uasi.

MASWALI YA KUJIFUNZA

1. Eleza kazi na cheo cha Lusifa cha awali.

2. Eleza uasi wake, kuanguka na vita vilivyofuatia.

3. Nani adui wa kweli wa waamini nyakati hizi?

Somo La Pili

Mamlaka hapa Duniani

DUNIA KUUMBWA

Na Mungu

Katika Mwanzo tunaelezwa kuwa Mungu aliumba dunia.

Mwanzo 1:1 Hapo mwanzo Mungu aliziumba mbingu na nchi.

➢ ***Ili IwezeKukalika***

Kulingana na Isaya, dunia haikuumbwa ili iwe tupu. Iliumbwa ili ikalike.

Isaya 45:18 Maana BWANA, aliyeziumba mbingu, asema hivi; Yeye ni Mungu; ndiye aliyeiumba dunia na kuifanya; ndiye aliyeifanya imara; hakuiumba ukiwa, aliiumba ili ikaliwe na watu; Mimi ni BWANA, wala hapana mwingine."

➢ ***Ilifanyika bila Umbo***

Hata hivyo, Mwanzo 1:2 inaeleza dunia kama isiyokuwa na umbo, tupu na yenye giza. Maelezo haya si ya mahali palipo tayari kukalika. Katika Waebrania, neno linalotafsiri kama "ilikuwa" inaweza pia kutafsiriwa vyema kama "ilifanyika."

Mwanzo 1:2 Nayo nchi ilikuwa ukiwa, tena utupu, na giza lilikuwa juu ya uso wa vilindi vya maji, Roho ya Mungu ikatulia juu ya uso wa maji.

Katika Yeremia tunapata neno kama hilo la Kiebrania na kutafsiriwa.

Yeremia 4:23-25 niliiangalia nchi, na tazama, ilikuwa ukiwa, haina watu; naliziangalia mbingu, nazo zilikuwa hazina nuru. Naliiangalia milima, na tazama, ilitetemeka, na milima yote ilisongea huko na huko. Nikaangalia, na tazama, hapakuwa na mtu hata mmoja, na ndege wote wa angani wamekwenda zao.

➢ ***Ilifanyika Giza na Tupu***

Yeremia anaeleza kuwa hukumu ya Mungu iligeuza dunia iliyokamilika na kuwa mahali pa uharibifu (yenye giza).

Yeremia 4:23 Naliiangalia nchi, na tazama, ilikuwa ukiwa, haina watu, naliziangalia mbingu, nazo zilikuwa hazina nuru.

Yeremia aliendelea kueleza hukumu ya Mungu iliyokuwa duniani.

Yeremia 4:26,27 Nikaangalia, na tazama, shamba lililozaa sana limekuwa ukiwa, na miji yake yote ilikuwa imebomoka mbele za BWANA, na mbele za hasira yake kali.

Maana BWANA asema hivi, Nchi yote itakuwa ukiwa; lakini sitaikomesha kabisa."

➢ ***Shetani Alikuja Duniani***

Kuna uwezekano kuwa Shetani alitupwa duniani kati ya Mwanzo 1:1 na Mwanzo 1:2. (Taz Kumbukumbu: ukur. 17)

Jaribu kuwaza juu ya Shetani alipotupwa hapa duniani. Alikuwa na mojawapo ya vyeo vikuu mbinguni. Alikuwa na urembo wa hali ya juu. Alikuwa ndiye kielelezo cha utukufu wa Mungu. Hata hivyo, katika kuasi kwake, alitaka hata zaidi. Alitamani kutawala mbinguni.

Palikuwa vita. Yeye na malaika waliomfuata walitupwa duniani. Kila mahali Shetani alipotazama alikumbushwa kuhusu Mungu Muumba ambaye sasa anamchukia sana. Alikumbushwa kuhusu vyote alivyopoteza baada ya kuasi.

Labda Shetani, kama aliyekuja kuiba, kuua, na kuharibu, katika chuki yake na hasira alikuwa tayari ameiharibu dunia. Kile ambacho Shetani alibakisha ili kutawala kilifanyika tupu, wazi, na kubaki katika giza tele. Lusifa alitamani kutawala dunia nzima. Sasa, kile alibakisha ni nyota moja ndogo, yenye giza, tupu.

Dunia Kurejeshwa na Mungu

Katika Mwanzo 1:2, tunasoma kuwa Roho wa Mungu alikuwa juu ya maji. Mwanzo 1:3 inataja kuwa Mungu alisema "hebu na kuwe na mwanga." Shetani aliitambua sauti hiyo!

Alikuwa ameisikia katika milele awali. Hebu fikiri juu ya vile alivyobabaika alipoisikia sauti ya Mungu. Hata hapa duniani hawezi kujificha kutoka kwa Mungu. Pia Mungu hamwachi afanye atakavyo.

Je, Shetani alitiwa hofu kiasi gani alipomtazama Mungu akiirejesha dunia katika hali yake ya awali kwa siku tano zilizofwata.

"Kisha Mungu Akasema"

Dunia iliumbwa tena kwa maneno ya Mungu. Ni muhimu kuelewa kuwa Mungu alinena na kurejesha vyote vilivyoharibika.

Mwanzo 1:3 Mungu akasema, Iwe nuru; ikawa nuru.

ms. 6 Mungu akasema, Na liwe anga katikati ya maji, likayatenge maji na maji."

ms. 9 Mungu akasema "Maji yaliyo chini ya mbingu na yakusanyike mahali pamoja, ili pakavu paonekane", ikawa hivyo.

ms. 11 Mungu akasema, "Nchi na itoe majani, mche utoao mbegu, na mti wa matunda uzaao matunda kwa jinzi yake, ambao mbegu zake zimo ndani yake, juu ya nchi;" ikawa hivyo.

ms. 14 Mungu akasema, "Na iwe mianga katika anga la mbingu ili itenge kati ya mchana na usiku; nayo iwe ndiyo dalili na majira na siku na miaka."

ms. 20 Mungu akasema, "Maji na yajawe kwa wingi na kitu kiendacho chenye uhai, na ndege waruke juu ya nchi katika anga la mbingu."

ms. 24 Mungu akasema, "Nchi na izae kiumbe hai kwa jinsi zake, mnyama wa kufungwa, nacho kitambaacho, na wanyama wa mwitu kwa jinsi zake;" Ikawa hivyo.

ms. 26 Mungu akasema, " Na tumfanye mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu; wakatawale samaki wa baharini, na ndege wa angani, na wanyama, na nchi yote pia, na kila chenye kutambaa kitambaacho juu ya nchi."

ms. 29 Mungu akasema "Tazama, nimewapa kila mche utoao mbegu, ulio juu ya uso wa nchi yote pia, na kila mti, ambao matunda yake yana mbegu; vitakuwa ndivyo chakula chenu."

Shetani Kuitikia

Yote iliyokuwa kamili, yaliyoharibiwa hapa duniani, Mungu aliifanya kamili tena. Je, mipango ya Mungu ilikuwa gani? Kwa nini Mungu alifuatilia nyota (dunia) hii?

Fikiri juu ya Shetani akiwaita mapepo, "kwa nini Mungu hatuachi sisi? Anayo dunia nzima kuitawala nasi tuko tu na nyota hii ndogo!"

Hofu na chuki lazima vilimshika Shetani wakati kila siku kwa siku tano, sauti ya Mungu ilisikika. Wakati Mungu aliponena, dunia ilirejeshwa na kuboreshwa katika hali yake ya awali. Chuki ya Shetani kwa Mungu lazima iliendelea kuongezeka kila siku.

Kumbuka: Wasomi wa Biblia wanatofautiana kuhusu utaratibu wa mambo yanayohusu kuanguka kwa Shetani na kuumbwa kwa mwanadamu. Nakala katika somo hili inagusia "wazo la pengo" amabayo hufundisha kuwa pana "pengo" katika nyakati kati ya msitari wa kwanza na wa pili katika kifungu cha kwanza cha Mwanzo. Makisio haya hufundisha kuwa Shetani alitupwa chini duniani baada ya uasi wake na kisha, dunia ikawa bila umbo, tupu na yenye giza kama inavyoelezwa katika msitari wa pili.

Wengine hufundisha kuwa kuasi na kuangushwa kwa Shetani kulifwatia kuumbwa kwa mwanadamu. Pia, wasomi wengine hutofautiana juu ya nyakati za kumtupa Shetani duniani toka mbinguni.

Si muhimu hasa kukubaliana na utaratibu wa matukio kama ilivyotajwa katika somo hili, kama ilivyo kuelewa kuwa mwanadamu, aliyeumbwa katika mfano wa Mungu, alipewa uwezo wa hali ya juu na utawala wa dunia. Ni muhimu pia kuelewa kuwa hii ndiyo sababu inayomfanya Shetani amchukie mwanadamu sana.

MAMLAKA ALIYOPEWA MWANADAMU

Aliumbwa Katika Mfano wa Mungu

Baada ya Mungu kuiumba dunia, Aliwaumba mume na mke kwa mfano Wake. Kisha akawapa uwezo juu ya vyote vilivyoishi duniani.

➢ ***Hebu na Wapate Kutawala***

Katika Mwanzo moja, tunaambiwa kuwa mwanadamu aliumbwa kwa mfano wa Mungu. Katika Mwanzo tisa, tunaambiwa kitu kile kile tena.

Mwanzo 1:26 Mungu akasema, " Na tumfanye mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu; wakatawale samaki wa baharini, na ndege wa angani, na wanyama, na nchi yote pia, na kila chenye kutambaa kitambaacho juu ya nchi."

Mwanzo 9:6 Atakayemwaga damu ya mwanadamu, damu yake huyo itamwagwa na mwanadamu, maana kwa mfano wake Mungu alimfanya mwanadamu.

Kutambua kuwa waume kwa wake waliumbwa kwa mfano wa Mungu in muhimu katika kuelewa somo hili kwa sababu mfano wa Mungu ni mojawapo ya uwezo.

Mwanzo 1:27 Mungu akaumba mtu kwa mfano wake, kwa mfano wa Mungu alimwumba, mwanamume na mwanamke aliwaumba.

Kupewa Uzima wa Mungu

Mungu aliumba mwili wa mwanadamu toka vumbi la udongo kwa mikono Yake, na kisha akaivuvia pumzi Yake Mungu. Mungu alivuvia pumzi katika mwanadamu hali Yake ya asili.

Alitupatia uzima Wake. Uzima wa Mungu uko ndani yetu!

Mwanzo 2:7 BWANA Mungu akampulizia puani pumzi ya uhai; mtu akawa nafsi hai.

Mamlaka Juu ya Shetani

Baada ya vita mbinguni, Shetani alitupwa duniani. Je, unaweza kufikiri jinsi alivyojawa na hofu alipomtazama Mungu akimuumba mwanadamu, akimvuvia pumzi ya uzima wa Mungu, na kisha kumpa kiumbe huyu mpya utawala na mamlaka juu ya vyote vinavyoishi duniani?

Shetani alikuwa akiishi duniani! Utawala aliopewa mwanadamu ulijumlisha mamlaka juu ya Shetani na wafuasi wake.

Mamlaka Kupewa Wote

Mungu alimuumba Hawa na Adamu, na wawili hao walikuwa na mamlaka na utawala juu ya vitu vyote duniani.

Katika Mwanzo 2 tunapata hadithi ya kuumbwa kwa Hawa.

Mwanzo 2:21-24 BWANA Mungu akamletea Adamu usingisi mzito, naye akalala; kasha akatwaa ubavu wake mmoja, akafunika nyama mahali pake.

Na ule ubavu alioutwaa katika Adamu BWANA Mungu akaufanya mwanamke, kwa maana ametwaliwa katika mwanamume.

Adamu akasema, "huyu ni mfupa katika mifupa yangu, basi ataitwa mwanamke, kwa maana ametwaliwa katika mwanamume."

Kwa hiyo mwanamume atamwacha baba yake na mama yake naye ataambatana na mkewe, nao watakuwa mwili mmoja.

➢ ***Sio Tu Kwa Adamu***

Katika kutaja mwanadamu mara ya kwanza, Mungu alisema "hebu na wawe na utawala" hakusema "hebu na awe na utawala"

Mwanzo 1:26-28a Mungu akasema, " Na tumfanye mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu; wakatawale samaki wa baharini, na ndege wa angani, na wanyama, na nchi yote pia, na kila chenye kutambaa kitambaacho juu ya nchi."

Mungu akaumba mtu kwa mfano wake, kwa mfano wa Mungu alimwumba, mwanamume na mwanamke aliwaumba.

Mungu akawabariki, Mungu akawaambia, Zaeni, mkaongezeke, mkaijaze nchi, na kuitiisha; mkatawale samaki wa baharini, na ndege wa angani, na kila kiumbe chenye uhai kiendacho juu ya nchi."

Mwanadamu asionyeshe utawala juu ya mwanamke, au mwanamke kwa mwanamume, bali kama mwili mmoja, ni sharti wawe pamoja katika utawala na mamlaka hapa duniani.

Pamoja, walipewa mamlaka juu ya:

- ➢ Samaki baharini
- ➢ Ndege wa angani
- ➢ Mifugo
- ➢ Dunia nzima
- ➢ Kila kiumbe anayeishi

➢ ***Sio Juu ya Watu Wengine***

Mwanadamu hakupewa mamlaka juu ya mwanadamu mwenzake. Alipewa uwezo juu ya viumbe vyote vya Mungu hapa duniani na juu ya Shetani na mapepo yake.

Mungu sasa alikuwa na uwezo na utawala wote katika dunia nzima isipokuwa katika nyota ya arthi. Hapa Alitoa uwezo na mamlaka haya kwa viumbe hawa wapya wafananao na Mungu waitwao mume na mke.

Mwanadamu Alipewa Uhuru wa Kuchagua

➢ ***Kuchagua***

Mungu alimpa Adamu uhuru wa kuchagua. Alikuwa na uwezo wa kuchagua kumtii au kutomtii Mungu. Mwanadamu alipewa uwezo au uhuru wa kuchagua.

Uhuru wa kuchagua ulipimwa katika bustani ya Edeni kati ya kutii au kutotii, kati ya kula kutoka kwa mti wa mema na mabaya, au kutokula. Mwanadamu bado ana uhuru wa kuchagua.

Mwanzo 2:16, 17 BWANA Mungu akamwagiza huyo mtu, akisema, matunda ya kila mti wa bustani waweza kula, walakini matunda ya mti wa ujuzi wa mema na mabaya usile, kwa maana siku utakapokula matunda ya mti huo utakufa hakika."

SHETANI ANAMCHUKIA MWANADAMU

Shetani alimchukia Adamu na Hawa kwa sababu waliumbwa kwa mfano wa Mungu. Wakati wa kuumbwa kwao, walipewa kila kitu alichojaribu kunyakua kwa nguvu.

➢ Walionekana kama Mungu

➢ Walinena kama Mungu

➢ Walitembea kama Mungu

Walipewa mamlaka juu ya vitu vyote duniani ambayo ilijumlisha Shetani. Hiyo ilijumlisha kila kitu alichokua akitawala. Hiyo ilijumlisha ufalme "wake" wote.

Hofu Kuu ya Shetani

Shetani anajua mamlaka tuliyo nayo. Anajua kile Mungu amesema na kutenda.

Ni muhimu sana kwake kuwa tusitambue mamlaka yetu – kuwa tusitambue na kutembea katika uwezo na mamlaka tuliyopewa na Mungu. Shetani hana sababu ya kuwaogopa waume kwa wake wanaotembea katika mamlaka waliyopewa na Mungu.

"Nitafanya" za Shetani

Kumbuka "nita" za Shetani katika Isaya.

Isaya 14:13-15 Nawe ulisema moyoni mwako:

Nitapanda mpaka mbinguni,
Nitakiinua kiti changu juu kuliko nyota za Mungu;
Nami nitaketi juu ya mlima wa mkutano, katika pande za mwisho za kaskazini;
Nitapaa kupita vimo vya mawingu;
Nitafanana nay eye aliye juu;

Lakini utashushwa mpaka kuzimu, Mpaka pande za mwisho za shimo.

Kila Kitu Alichopewa Mwanadamu

Kila kitu ambacho Shetani alitaka chini ya uasi wake, Mungu alimuumba mwanadamu!

➢ Shetani alisema, "Nitapaa mbinguni."

Mwanadamu aliumbwa awe na ushirika na Mungu. Tuliumbwa kutembea na kuongea na Mungu! Tuliumbwa kutawala pamoja Naye.

Ufunuo Wa Yohana 20:6 Heri, na mtakatifu, ni yeye aliye na sehemu katika ufufuo wa kwanza; juu ya hao mauti ya pili haina nguvu; bali watakuwa makuhani wa Mungu na wa Kristo, nao watatawala pamoja naye hiyo miaka elfu.

➢ Shetani alisema, "Nitainua enzi yangu juu ya nyota za Mungu."

Nyota za Mungu ni malaika. Shetani alitamani awe juu ya malaika katika umuhimu.

Mtume Paulo aliandika kuwa siku moja tutatoa hukumu kwa malaika.

1 Wakorintho 6:2, 3 Au hamjui ya kwamba watakatifu watauhukumu ulimwengu? Na ikiwa ulimwengu tahukumiwa na ninyi, je! Hamstahili kukata hukumu zilizo ndogo? Hamjui ya kuwa tutawahukumu malaika, basi si zaidi sana mambo ya maisha haya?

➢ Shetani alisema, "Pia nitaketi kwenye mlima wa mkusanyiko upande wa kasikazini."

Tumeketi katika mbingu katika Yesu.

Waefeso 2:6 ... akatufufua pamoja naye, akatuketisha pamoja naye katika ulimwengu wa roho, katika Kristo Yesu;

➢ Shetani alisema, "Nitapaa juu ya mawingu kabisa"

Tutakutana na Yesu hewani – katika mawingu.

1 Wathesalonike 4:16, 17 Kwa sababu Bwana mwenyewe atashuka kutoka mbinguni pamoja na mwaliko, na sauti ya malaika mkuu, na parapanda ya Mungu; nao waliokufa katika Kristo watafufuliwa kwanza. Kisha sisi tulio hai, tuliosalia, tutanyakuliwa pamoja nao katika mawingu, ili tutakuwa pamoja hewani; na Bwana milele.

➢ Shetani alisema, "Nitakuwa kama Yeye aliye Mkuu."

Mwanadamu aliumbwa katika mfano wa Mungu. Je, bado una shaka kwa nini Shetani anamchukia mwanadamu?

Tumeumbwa ili:

➢ Tuwe kama Mungu

➢ Kuongea kama Mungu

➢ Kutembea kama Mungu na

➢ Kutawala pamoja na Mungu!

Itakuwa yenye fedheha kiasi gani kwa Shetani kuwa tumepewa vyote alivyokuwa akinyakua katika uasi wake.

MASWALI YA KUJIFUNZA

1. Eleza katika maneno yako mwenyewe, asili ya dunia, kuanguka kwa Shetani na hukumu iliyofuatia katika dunia.

2. Eleza jinsi Mungu alivyofanya katika utawala na mamlaka alipoiumba dunia tena.

3. Eleza kwa nini Shetani anakuchukia. Nini umefanya kilichosababisha chuki hiyo?

Somo La Tatu

Mpango wa Hila ya Shetani

Shetani aliona kuwa Adamu na Hawa, na bila shaka wanadamu wote, walipewa uzima na hali aliyokuwa nayo Mungu. Shetani lazima alijawa na hofu kuwa mwanadamu sasa alikuwa na mamlaka juu vyote duniani.

Mwanadamu alionekana kama Mungu. Alitenda kama Mungu. Chuki yote aliyokuwa nayo Shetani juu ya Mungu, alimgeukia mwanadamu. Hakupenda kumwona mwanadamu akifaulu. Kwa hivyo, Shetani mwenyewe aliunda mbinu yake!

MPANGO WA SHETANI

Hila

Shetani aliwadanganya malaika mbinguni, na theluthu moja waliwafuata katika uasi. Alijulikana kwa kuhadaa.

Mungu alimpa mwanadamu uhuru wa kuchagua – wangeweza kuchagua kutii au kutotii. Katika uhuru huo wa kuchagua, alitoa pia adhabu ya kutotii.

Mwanzo 2:17 ... walakini matunda ya mti wa ujuzi wa mema na mabaya usile, kwa maana siku utakapokula matunda ya mti huo utakufa hakika."

➢ ***Alijibadilisha Alimwuliza Mungu***

Shetani alichagua kujibadilisha mwenyewe kama nyoka ili aingie katika bustani bila kugunduliwa. Hakuwa na ruhusa kuwa katika bustani na Adamu angemrusha nje kama Shetani angeingia kwa ujasiri bila kujibadilisha.

Mwanzo 3:1a Basi nyoka alikuwa mwerevu kuliko wanyama wote wa mwitu aliofanya BWANA Mungu.

"erefu" ina maana mwongo au mjanja.

Shetani alikuwa ndani ya mwili wa nyoka alipoongea na Hawa. Mapepo hukalia mili hata sasa. Hiyo ndiyo hali yao danganyifu na inayowakilisha uovu wanaotaka kutenda.

Mwanzo 3:1b Akamwambia mwanamke, Ati! Hivi ndivyo alivyosema Mungu, Msile matunda ya miti yote ya bustani?"

Shetani aliuliza kuhusu kile Mungu alisema, na kwa wakati huo aliacha adhabu ya dhambi.

➢ ***Alimnukulu Mungu***

Ngundua kuwa Shetani anayanukulu maneno ya Mungu ili kuyabadilisha kwa uwongo wake.

Mwanzo 3:2, 3 Mwanamke akamwambia nyoka, Matunda ya miti ya bustani twaweza kula; "lakini matunda ya mti ulio katikati ya bustani Mungu amesema, Msiyale wala msiyaguse, msije mkafa." Hawa akaongeza "guza" kwa kile Mungu alinena kwa kweli, lakini bado alikumbuka adhabu.

➢ ***Uwongo wa Shetani***

ms. 4b "Hakika hamtakufa."

Shetani alisema kinyume na kile Mungu alisema, lakini Hawa aliendelea kusikiliza. Kisha Shetani aliahidi mshahara wa dhambi.

➢ ***Utakuwa kama Mungu***

ms. 5 "Kwa maana Mungu anajua ya kwamba siku mtakayokula matunda ya mti huo, mtafumbuliwa macho, nanyi mtakuwa kama Mungu, mkijua mema na mabaya."

Shetani aliwaambia Hawa na Adamu, "macho yako yatafunguka na utakuwa kama Mungu!" walikuwa kama Mungu lakini Shetani aliwadanganya katika kujitakia zaidi.

ADAMU NA HAWA WALITENDA DHAMBI

Wote Walitenda Dhambi

Mara nyingi, tunamwona Hawa pekee wakati Shetani alijibadili kuwa nyoka na kumjia. Biblia haisemi hivyo. Katika msitari wa sita, tunasoma "Pia alimpa mume wake aliyekuwa naye, na akala."

Wote waliacha kufuata Neno la Mungu, wakafuata hisia zao, wakamsikiliza Shetani, na kula tunda.

ms. 6 Mwanamke alipoona ya kuwa ule mti wafaa kwa chakula, wapendeza macho, nao ni mti wa kutamanika kwa maarifa, basi alitwaa katika matunda yake akala, akampa na mumewe naye akala.

Wakati Adamu na Hawa walimwasi Mungu na kula tunda, hali Yake Mungu iliondoka ndani yao. Walikuwa wameviswa katika utukufu mkuu – hali ya Mungu – sasa wakawa uchi.

Kwa kutumia mti wa ufahamu wa mema na mabaya, Shetani aliwadanganya Adamu na Hawa, kuwahadaa na kuwashinda.

Shetani hajabadilika. Mbinu zake ni zile zile hata sasa!

Waliachwa

- ***Kushindwa***
- ***Uchi***

Shetani aliwadaganya, na mwanadamu akatolewa maficho yake, utawala na mamlaka.

Mwanzo 3:7 Wakafumbuliwa macho, wote wawili wakajijua kuwa wa uchi, wakashona majani ya mtini, wakajifanyia nguo.

- ***Wenye Hofu***
- ***Kujificha***

Shetani aliwashinda Adamu na Hawa. Sasa, waliokuwa watawala wa ulimwengu walikuwa waoga na kujificha nyuma ya kichaka!

Mwanzo 3:10 Akasema, "Nalisikia sauti yako bustani, nikaogopa kwa kuwa mimi ni uchi; nikajificha."

- ***Bado katika Sura Ya Mungu***

Ni vyema kuelewa kuwa hata baada ya Adamu na Hawa kutenda dhambi bado walikuwa katika mfano wa Mungu. Hata hivyo, hawakuwa na uzima wa Mungu ndani yao. Walikuwa wamekufa kiroho.

Mwanzo 9:1,2,6 Mungu akambariki Nuhu na wana-we, akawaambia, "zaeni, mkao-ngezeke, mkaijaze nchi" Kila mnyama wa katika nchi atawaogopa ninyi na kuwahofu, na kila ndege wa angani; pamoja na vitu vyote vilivyojaa katika ardhi, na samaki wote wa baharini; vimetiwa mikononi mwenu." "Atakayemwaga damu ya mwanadamu, damu yake huyo itamwagwa na mwanadamu, maana kwa mfano wake Mungu alimfanya mwanadamu."

Mwanadamu alikuwa bado:

- Azae Matunda
- Ongezeka
- Jaza Dunia
- Kuilinda
- Kuwa na mamlaka na kutawala

Sasa, hii itafanyika kwa maumivu, kwa jasho lake, na viumbe vyote vitaishi katika hofu ya mwanadamu.

Rudia

Mungu alimwumba Adamu na Hawa kuitawala dunia. Lakini, baada ya mwanadamu kuasi Mungu na kukosa kutii kinyume na matakwa ya Mungu, alikufa kiroho. Alinyang'anywa mamlaka na utawala wa Mungu.

Mapenzi ya Mungu yalikuwa ya waume na wake wawe na mamlaka na utawala.

Mapenzi ya Shetani yalikuwa mwanadamu kuasi mbele za Mungu.

Adamu na Hawa walikuwa na uamuzi wa kufanya – walikuwa na uwezo wa kuchagua.

Waliamua kuegemea upande wa Shetani.

Shetani aliiba kutoka kwa Adamu vyeo:
mtawala wa dunia hii,
mwana wa kiume wa mfalme wa dunia hii.

BAADA YA MWANADAMU KUTENDA DHAMBI

Laana Zilizofuata

➢ ***Kwa Nyoka***

Kwa vile nyoka alimruhusu Shetani kuutumia mwili wake, laana iliwekwa kwa nyoka wote.

Mwanzo 3:14 BWANA Mungu akamwambia nyoka, kwa sababu umeyafanya hayo, umelaaniwa wewe kuliko wanyama wote, na kuliko hayawani wote walioko mwituni; kwa tumbo utakwenda, na mavumbi utakula siku zote za maisha yako."

➢ ***Kwa Mwanamke***

Palikuwa na aina mbili za laana iliyowekwa kwa mwanamke. Atazaa watoto katika maumivu na mwanamume atamtawala.

Mwanzo 3:16 Akamwambia mwanamke, "Hakika nitakuzidishia uchungu wako, na kuzaa kwako; kwa utungu utazaa watoto; na tama yako itakuwa kwa mumeo, naye atakutawala."

Mwanamke anapomkubali Yesu kama mwokozi wake wa pekee, anapokea tena nafasi yake katika uumbaji. Yesu alifanyika laana kwa niaba yake.

Wagalatia 3:13 Kristo alitukomboa katika laana ya torati, kwa kuwa alitukomboa katika laana kwa ajili yetu; maana imeandikwa, ("Amelaaniwa kila mtu aangikwaye juu ya mti.")

➢ ***Kwa Mwanamume***

Laana iliyowekwa kwa mwanamume ni kuwa kwa maumivu atailima ardhi ili kupata chakula.

Mwanzo 3:17 Akamwambia Adamu, "Kwa kuwa umeisikiliza sauti ya mke wako, ukala matunda ya mti ambao nalikuagiza, nikisema, Usiyale; ardhi imelaaniwa kwa ajili yako; kwa uchungu utakula mazao yake siku zote za maisha yako."

➢ ***Kwa Dunia***

Dunia pia ililaaniwa.

ms. 18,19 Michongoma na miiba itakuzalia, nawe utakula mboga za bondeni; kwa jasho utakapoirudia ardhi, ambayo katika hiyo ulitwaliwa; kwa maana u mavumbi wewe, nawe mavumbini utarudi.

➢ ***Kwa Shetani***

Kwa wakati ambao Shetani alipata ushindi mkuu juu ya mwanadamu, Mungu alitaja laana juu yake.

Mwanzo 3:15 Nami nitaweka uadui kati yako na huyo mwanamke, na kati ya uzao wake; huo utakuponda kichwa, na wewe utamponda kisigino.

Mungu alinena na Shetani, aliyekuwa ndani ya nyoka, na kumwambia kuwa mbegu ya mwanamke itakiponda kichwa chake.

Ahadi ya Kukombolewa!

Laana iliyowekwa juu ya Shetani pia ilikuwa ahadi ya kwanza ya kuja kwa Masiya. "Mbegu" ilikuwa unabii juu ya Yesu atakayezaliwa na Mwanamke.

Shetani ni sharti awe chini ya miguu ya Yesu. Kichwa chake kitapondwa na kuchubuka.

Mifano ya Baadaye/Usoni

Katika historia ya kuanguka kwa mwanadamu kuna aina nyingi, au mifano, ya usoni.

➢ ***Tawi la Mzabibu***

Matawi ya mzabibu ambayo Adamu na Hawa walitumia kujifunika yalikuwa mifano ya jaribio la mwanadamu kufunika dhambi zake mwenyewe. Ni mifano ya dini zilizoundwa na mwanadamu.

➢ ***Wanyama Kuchinjwa***

Kumwagika kwa damu ya kwanza kulifanywa na Mungu ili kuwafunika Adamu na Hawa. Hii ilikuwa dalili ya, au mfano wa Yesu ambaye atauliwa kama malipo ya dhambi za ulimwengu wote.

Mpango wa Mungu

Hata katika sehemu ya giza kabisa katika historia ya mwanadamu, Mungu alikuwa na mpango wa wokovu kwa mwanadamu.

Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, katika uamuzi Wake, atatoa maisha yake kwa ajili yetu.

Kwa kifo Chake, atamshinda Shetani. Shetani atakigonga kisigino cha Yesu, lakini Yesu atakiponda kichwa cha Shetani. Mamlaka ya Shetani yatapondwa na kurejeshewa mwanadamu kulingana na mpango wa Mungu wa awali.

MPANGO WA SHETANI

Uwongo wa Shetani

Shetani hajaacha kumchukia na kuwaogopa wanadamu walioumbwa kuonekana na kutenda kama Mungu. Mpango wake wa uwongo haujaisha. Katika uwongo, viongozi wa kiroho kila mara wamepoteza uwezo wao. Wamekuwa viongozi vipofu wongozao vipofu.

Kazi ya Shetani

Shetani ameandaa jeshi lake katika mpango wa vita kamili. Viongozi wa giza wamewekwa kwa kila nchi, kila mwanamume, mwanamke na mtoto, ili kuwaweka katika ufungwa. Maagizo yao ni kuiba, kuua na kuharibu.

Mungu aliileta sheria kwa wanadamu ili wawe na msamaha wa dhambi na kutembea katika uhusiano naye. Lakini kwa miaka elfu nne Shetani aliishi akiitawala dunia kwa sababu ya uasi wa mwanadamu.

Watu walioumbwa kuitawala dunia hii walikuwa:
vipofu na waombao kando ya barabara,
wamefungwa na pepo za udhaifu,
wamepagawa na jeshi la mapepo.

Nyuso na mili, zilizoumbwa kuonekana kama Mungu,
zimeliwa na ukoma unaotisha.

Waume na wake walioumbwa ili kutawala waliishi katika kushindwa!

MASWALI YA KUJIFUNZA

1. Eleza kwa nini Shetani anawachukia sana viumbe waitwao wanaume na wanawake.

2. Eleza matokeo ya kuanguka kwa mwanadamu na dhambi.

3. Je, ahadi ya Mungu ya kukombolewa ilikuwa nini kama inavyoonyeshwa katika Mwanzo 3:15?

Somo La Nne

Kisha akaja Yesu – Mpango wa Mungu

ADAMU WA KWANZA – ADAMU WA MWISHO

Mungu alimtuma Mwanawe

Wakati Adamu na Hawa walitenda dhambi, Mungu aliahidi kumtuma Mwanawe, mbegu ya mwanamke, kukiponda kichwa cha Shetani. (Mwanzo 3:15) Paulo anaeleza kuhusu kitendo hiki huku akilinganisha na ahadi ya kwanza ya Mkombozi.

Wagalatia 4:4, 5 hata ulipokuwadia utimilifu wa wakati, Mungu alimtuma Mwanawe ambaye amezaliwa chini ya sheria, kusudi awakomboe hao waliokuwa chini ya sheria, ili sisi tupate kupokea hali ya kuwa wana.

Uhusiano kati ya mwanadamu na Mungu na mamlaka yake ungerejeshwa na dhabihu ambayo Yesu angefanya alipokufa msalabani.

Kukombolewa kutoka dhambini, ni adhabu, na matokeo ya laana kutokana na sheria, mwanadamu anaweza kuzaliwa upya katika jamaa ya Mungu. Anaweza kufanyika kiumbe kipya. Anaweza tena, kupokea Roho wa Mungu ndani yake.

Adamu Alileta Dhambi

Dhambi ilikuja ulimwenguni kupitia kuasi kwa Adamu.

Warumi 5:12 Kwa hiyo, kama kwa mtu mmoja dhambi iliingia ulimwenguni, na kwa dhambi hiyo mauti; na hivyo mauti ikawafikia watu wote kwa sababu wote wamefanya dhambi...

Yesu Alileta

➢ ***Haki***

Kupitia kutii kikamilifu kwa mtu mmoja, Yesu, wengi wanaweza kufanyika wa haki.

ms. 19 Kwa sababu kama kwa kuasi kwake mtu mmoja watu wengi waliingizwa katika hali ya wenye dhambi, kadhalika kwa kutii kwake mmoja watu wengi wameingizwa katika hali ya wenye haki.

➢ ***Habari Njema***

Baada ya Adamu na Hawa kutenda dhambi, walipogundua Mungu anawaendea, walijificha nyuma ya vichaka. Sasa Yesu, Mwana wa Mungu alikuwa akija na malaika wakasema, “Usiwe na hofu! Hii ni habari njema kwenu.”

Luka 2:10, 11 "Malaika akawaambia, Msiogope; kwa kuwa mimi ninawaletea habari njema ya furaha kuu itakayokuwa kwa watu wote; maana leo katika mji wa Daudi amezaliwa, kwa ajili yenu, Mwokozi, ndiye Kristo Bwana."

➢ ***Amani kwa Wanadamu***

Malaika mmoja akaanza habari kwa wachungaji katika milima ya Bethlehemu usiku ule, lakini furaha mbinguni ilipita kifani, hali ya kiroho ilipasuka katika hali ya asili.

ms. 13, 14 Mara walikuwapo pamoja na huyo malaika wingi wa jeshi la mbinguni, wakimsifu Mungu, na kusema. Atukuzwe Mungu juu mbinguni, Na duniani iwe amani kwa watu aliowaridhia!"

Je, ni ahadi njema iliyotolewa, hata wakati Kristo alipozaliwa. "Ulimwenguni amani, wema kwa wanadamu!"

Hakuna maneno ya kueleza furaha iliyokuwa ulimwenguni kote.
Malaika walikuwa na furaha sana
Wakaimba nyimbo za sifa mbele ya wachungaji.
hata nyota walitangaza kuzaliwa Kwake!

YESU ALIFANYA KAZI ULIMWENGUNI KAMA MWANADAMU!

Je, Yesu alitenda katika mamlaka na uwezo alipokua hapa duniani kama Mungu, au kama mwanadamu – katika nguvu za Roho Mtakatifu?

Yesu, Adamu wa Mwisho

Paulo alimtaja Yesu kama Adamu wa Mwisho.

1 Wakorintho 15:45 Ndivyo ilivyoandikwa, Mtu wa kwanza, Adamu, akawa nafsi iliyo hai; Adamu wa mwisho ni roho yenye kuhuisha.

Yesu, kama Adamu wa mwisho, alitembea na kuhudumu katika mamlaka hapa duniani kama vile alivyomuumba Adamu wa kwanza kutenda.

Ni muhimu kuelewa haya kwa sababu ni kupitia kutimiza sheria kama Adamu wa Mwisho angeweza kutuletea uhuru kutokana na sheria. Ni kwa kuwa mwanadamu tu angeweza kufanyika Mwokozi wetu. Ilikuwa vyema amshinde Shetani, kama mwanadamu, ili kurejesha mamlaka ambayo Shetani alikuwa ameiba kutoka kwa Adamu wa Kwanza.

Kwa maana Yesu ndiye alikuwa mwanadamu wa kwanza aliye mkamilifu baada ya Adamu wa kwanza, alikuwa na

mamlaka aliyopewa Adamu. Wakati Roho Mtakatifu alipokuja juu Yake, alikuwa na nguvu za Mungu ndani Yake.

Ubatizo wa Yesu

➢ ***Roho Alishuka juu Yake***

Yohana Mbatizaji aliona Roho wa Mungu akishuka juu ya Yesu na tukio hili lilikuwa la muhimu hata likaandikwa katika Injili zote nne (Mariko 1:10, Luka 3:22, Yohana 1:32).

Mathayo3:16 Naye Yesu alipokwisha kubatizwa mara akapanda kutoka majini, na tazama, mbingu zikamfunukia, akamwona Roho wa Mungu akishuka kama hua, akija juu yake.

➢ ***Miujiza Kutendeka***

Yesu, hakutenda miujiza yoyote kwa miaka thelathini ya kwanza ya maisha Yake, lakini alipokuwa akianza huduma ya wazi Roho Mtakatifu alishuka juu Yake. Na, katika nguvu za Roho Mtakatifu, huduma Yake ya miujiza ilianza.

Mamlaka ya Mungu ikitenda kazi na Roho wa Mungu ni vitu viwili vyenye nguvu katika ushindi!

Yesu aliacha Haki Yake kama Mungu

➢ ***Alijitoa Kabisa***

Mtume Paulo anatupa mawazo katika mambo ya Kristo alivyokuja hapa duniani. Paulo aliandika kuwa Yesu aliweka kando hali Yake kama Mungu.

Wafilipi 2:5-8 Iwenii na nia iyo hiyo ndani yenu ambayo ilikuwamo pia ndani ya Kristo Yesu; ambaye yeye mwanzo alikuwa yuna namna ya Mungu, naye hakuona kule kuwa sawa na Mungu kuwa ni kitu cha kushikamana nacho; bali alijifanya kuwa hana utukufu, akatwaa namna ya mtumwa, akawa ana mfano wa wanadamu; tena, alipoonekana ana umbo kama mwanadamu, alijinyenyekeza akawa mtii hata mauti, naam, mauti ya msalaba.

Yesu alikusudia:

➢ Azushwe na kutokuwa na heshima

➢ Kuchukua mfano wa mtumishi

➢ Kuja katika mfano wa mwanadamu

➢ Kunyenyekea

➢ Kutii hadi akafa

Yesu alikuwa na asili ya Mungu, na alikuwa sawa na Mungu na bado, alijinyima katika haki zake zote kama Mungu, ili kutumika hapa duniani kama mwanadamu. Alichukua juu Yake mfano wa mtumishi na umbo la mwanadamu. Alinyenyekea na kutii hadi kufa. Alikuja

ulimwenguni kama mwanadamu na nguvu zake hapa duniani zitakuja katika Roho Mtakatifu.

Kwa nini hii ilikuwa muhimu?

Adamu, mwanadamu wa kwanza, alimuasi Mungu na akatoa mamlaka yake kwa Shetani. Yesu, kama Adamu wa Mwisho, atafanya kila kitu hapa duniani kama mwanadamu aliyetiwa nguvu na Roho wa Mungu. Yeye atakuwa mwanadamu aliyekamilika akitenda kazi hapa duniani kama vile Adamu alivyoumbwa kutenda.

Kama Mwana wa Adamu

Wakati Yesu alikuwa hapa duniani, mamlaka aliyotumia yalikuwa katika Mwana wa Adamu. Katika kifungu kifwatacho, Yohana alitumia maneno yaliyo kamili kabisa: "Mwana wa Mungu" – "Mwana wa Adamu."

Yohana 5:25-27 Amin, amin, nawaambia, Saa inakuja, na sasa ipo, wafu watakapoisikia sauti ya Mwana wa Mungu, na wale waisikiao watakuwa hai. Maana kama vile Baba alivyo na uzima nafsini mwake, vivyo hivyo alimpa na Mwana kuwa na uzima nafsini mwake. Naye akampa amri ya kufanya hukumu kwa sababu ni Mwana wa Adamu.

Wafu wataisikia sauti ya Mwana wa Mungu. Nje ya dunia hii, Yesu alitenda kama sehemu ya utatu wa Mungu.

Duniani, Yesu alitembea katika mamlaka kwa sababu alikuwa Mwana wa Adamu. Mwanadamu aliumbwa ili kutembea katika mamlaka na utawala. Alikuwa Yesu mwanadamu aliyekuwa na mamlaka. Ni kwa sababu alikuwa Mwana wa Adamu, Adamu wa Mwisho, sio kwa sababu alikuwa Mwana wa Mungu.

Ikiwa Yesu alitenda, Basi nasi Tunaweza Kutenda Pia!

Yesu alifanya tu kile ambacho mwanadamu aliumbwa kutenda duniani. Alitembea katika nguvu za Roho Mtakatifu, na wala si kwa nguvu za Mwana wa Mungu!

Hii ni muhimu sana kwetu! Ikiwa Yesu alitembea kama mwanadamu hapa duniani, basi pia tunaweza kufanya hivyo. Tunazo nguvu zile, mamlaka, na haki ya kutenda yote ambayo Yesu alitenda alipokuwa hapa duniani kama Mwanadamu .

Kujaribiwa kama Sisi

Mungu aliwapa Adamu na Hawa hisia za uhuru, kuchagua. Yesu alikuwa na uwezo huo pia. Ili afanyike Adamu wa Mwisho kabisa, ilimbidi Yesu ateswe katika majaribu pia.

Adamu na Hawa walijaribiwa katika sehemu tatu:

- **Mwili** – Hawa aliona tunda, kuwa lilikuwa nzuri kwa chakula
- **Nafsi** – Shetani alimwahidi hekima, kubaini kati ya mema na mabaya
- **Roho** – Mwishowe Shetani alimwahidi atakuwa kama Mungu.

Yesu alijaribiwa katika sehemu hizi tatu.

Jaribio la Kwanza – Mwili

Yesu alikuwa jangwani kwa siku arubaini. Shetani alimjaribu, wakati huu wa udhaifu wa mwili, kumjaribu Yesu ili azitumie nguvu Zake kama Mwana wa Mungu kuyatosheleza mahitaji ya mwili wake kama mwanadamu. Lakini Yesu aliweka kando hali ya Mungu alipokuja hapa duniani na kutenda kama Mwana wa Adamu.

- ***Kutosheleza Mahitaji ya Mwanadamu***

Mathayo 4:1-3 Kisha Yesu alipandishwa na Roho nyikani, ili ajaribiwe na Ibilisi. Akafunga siku arobaini mchana na usiku, mwisho akaona njaa. Mjaribu akamjia akamwambia, "Ukiwa ndiwe Mwana wa Mungu, amuru kwamba mawe haya yawe mikate."

Mjaribu alipomjia, alisema, "kama wewe ni Mwana wa Mungu, jionyeshe, chukua haki zako kama Mungu. Kama wewe ni Mwana wa Mungu, amuru kuwa mawe haya yake mikate."

Kama Yesu angebadili mawe yawe mkate, hangetenda kama mwanadamu. Angetumia hali yake kama Mungu. Kama angefanya hivyo, Shetani angeshinda Adamu wa Kwanza na Adamu wa Mwisho.

- ***Yesu Alijibu***

Yesu alimjibu Shetani kwa kunukulu Neno la Mungu.

Mathayo 4:4 Naye akajibu akasema, Imeandikwa, "Mtu hataishi kwa mkate tu, ila kwa kila neno litokalo katika kinywa cha Mungu."

Gundua kuwa Yesu alijitambulisha kama mwanadamu.

ms. 5 Kisha Ibilisi akamchukua mpaka mji mtakatifu akamweka juu ya kinara cha hekalu.

Jaribio la Pili – Nafsi

Jaribio la pili lilikuwa katika sehemu ya nafsi. Shetani alimjaribu Yesu atende kinyume na mapenzi ya Mungu katika maisha na kutenda katika hisia Zake.

➢ ***Jidhihirishe***

ms. 6 ... akamwambia, "Ukiwa ndiwe Mwana wa Mungu jitupe chini, kwa maana imeandikwa Atakuagizia malaika zake; Na mikononi mwao watakuchukua; usije ukajikwaa mguu wako katika jiwe."

Hii ilikuwa kuendeleza majaribu hayo hayo ya kimsingi. "Ikiwa wewe ni Mwana wa Mungu …" Shetani alijua Yeye alikuwa Mwana wa Mungu. Maisha ya Yesu hapa duniani yalikuwa aishi kama Mwana wa Adamu, Adamu wa Mwisho.

➢ ***Yesu Alijibu***

Yesu alimshinda Shetani kwa kunena Neno la Mungu kwa kweli. Yesu alifahamu alikuwa Bwana na Shetani alijua hivyo.

ms. 7 Yesu akamwambia, Tena imeandikwa, " Usimjaribu Bwana Mungu wako"

Jaribio la Tatu – Roho

Katika jaribio la tatu, Shetani, alimpa Yesu falme zote hapa duniani. Je, hiyo haikuwa sababu Yesu alikuja hapa duniani? Kwamba alikuja kuishinda na kuitwaa dunia kutoka kwa Shetani?

➢ ***Awe Mungu wa Dunia Hii***

Mathayo 4:8,9 Kisha Ibilisi akamchukua mpaka mlima mrefu mno, akamwonyesha milki zote za ulimwengu, na fahari yake, akamwambia, "Haya yote nitakupa, ukianguka kunisuhudia.."

Shetani alikuwa na haki ya kumpa Yesu tawala hizi. Shetani, baada ya kudanganya na kuiba mamlaka ya Adamu, basi alikuwa mtawala wa dunia hii.

Lakini Yesu hakutaka kuirejesha dunia tena kutoka kwa Shetani katika hali yoyote yenye kumuasi Baba.

➢ *Yesu Alijibu*

Yesu hakuingia katika mjadala na Shetani. Yeye hakubishana naye kuhusu nani aliyetawala dunia hii. Yesu alimwambia aondoke. Alinena Neno la Mungu tena.

Mathayo 4:10 Ndipo Yesu alipomwambia, Nenda zako, Shetani; kwa maana imeandikwa, "Msujudie Bwana Mungu wako, umwabudu yeye peke yake."

Rudia

Kama Yesu angetenda kama Mwana wa Mungu jinsi alivyojaribiwa na Shetani, Yeye angepoteza haki zake kama Mwana wa Adamu. Yeye hangefanyika tena kuwa dhabihu kamili yenye kumkomboa mwanadamu.

Shetani akampa Yesu kile kitu Yesu alikuja kurejesha – haki ya kuitawala dunia hii. Ingekuwa "rahisi" kabisa sana kuifanya njia ya Shetani – bila kufa msalabani. Yesu alijua kuwa pasipo kumwagika damu Yake hapana msamaha wa dhambi.

Hata wakati Yesu alipokuwa akifa msalabani, Shetani, kupitia watu, walimdhihaki kwa maneno hayo hayo.

Mathayo 27:40 ...Ewe mwenye kulivunja hekalu na kulijenga kwa siku tatu, jiokoe nafsi yako; ukiwa ndiwe Mwana wa Mungu, shuka msalabani.

Mara nyingi, Shetani atatoa kwetu vitu ambavyo Mungu ametuahidi. Kile tunatakiwa kufanya ni kukubali tu kwa sehemu fulani. Mbinu ya kumshinda ni kujua na kunena Neno la Mungu.

YESU, MFANO WETU WA KUPINGA MAJARIBU

Yesu Anaelewa Majaribu

Kama vile hadithi ya kujaribiwa kwa Yesu inavyoelezwa katika Mathayo tunapewa fursa ya kujifunza jinsi Shetani anavyoweza kushindwa katika sehemu hii. Pia tunao uhuru wa kuamua. Pia tutajaribiwa, lakini Yesu alipoondoka katika ushindi – pia nasi tunaweza!

Paulo anataja kuwa; kwa kuwa Yesu ameteswa kwa kujaribiwa, anaweza kuwasaidia wale wanaojaribiwa.

Waebrania 2:18 Na kwa kuwa mwenyewe aliteswa alipojaribiwa, aweza kuwasaidia wao wanaojaribiwa.

Yesu Alijaribiwa Kama Sisi

Tunaweza kupata ujasiri katika kujua kuwa Yesu alijaribiwa katika kila hali kama vile sisi tunaweza kuwa. Kama vile hakushindwa katika majaribu, hata sisi tunaweza kuenda mbele za Mungu na kupata msaada Wake mkuu katika kuyashinda majaribu.

Waebrania 4:14-16 Basi, iwapo tunaye kuhani mkuu aliyeingia katika mbingu, Yesu, Mwana wa Mungu, na tuyashike sana maungamo yetu. Kwa kuwa hamna kuhani mkuu asiyeweza kuchukuana nasi katika mambo yetu ya udhaifu; bali yeye alijaribiwa sawasawa na sisi katika mambo yote, bila kufanya dhambi. Basi na tukikaribie kiti cha neema kwa ujasiri, ili

tupewe rehema, na kupata neema ya kutusaidia wakati wa mahitaji.

Majaribu Yote Ni Ya Kawaida

Mojawapo ya mbinu za Shetani ni kutufanya sisi tujihisi kuwa tu tofauti, kuwa majaribu yetu ni ya kipekee, au ngumu zaidi ya yale wengine wanapitia. Lakini majaribu yote ni ya kawaida na Mungu ametoa kwetu njia ya kuyaepuka ili tuweze kushinda.

1 Wakorintho 10:13 Jaribu halikuwapata ninyi, isipokuwa lililo kawaida ya mwanadamu, ila Mungu ni mwaminifu, ambaye hatawaacha mjaribiwe kupita mwezavyo; lakini pamoja na lile jaribu atafanya na mlango wa kutokea, ili mweze kustahimili.

Fuata Mfano wa Yesu

Yesu ni mfano wetu. Kama vile Yesu alipomjibu Shetani kwa kutumia Neno la Mungu, pia inatupasa kufanya hivyo.

Shetani alipomjia Yesu, Yesu haku

- ➢ bishana na Shetani
- ➢ waza na Shetani
- ➢ fikiri kutenda njia ya Shetani

Yesu alinukulu Neno la Mungu lililoandikwa.

Mathayo 4:4 Naye akajibu akasema, "Imeandikwa, Mtu hataishi kwa mkate tu, ila kwa kila neno litokalo katika kinywa cha Mungu."

Hivyo ndivyo Shetani hushindwa. Neno la Mungu ni sharti liwe kwenye vinywa vyetu.

Magonjwa yanapotujia miilini mwetu, tunaweza kusema, "imeandikwa, "kwa mapigo yake nimepona."

Umaskini unapokuja kinyume na fedha zetu, tunaweza kusema, "imeandikwa, 'Mungu wangu atakutana na mahitaji yangu yote ...'"

Shetani anapojaribu kuwapotosha watoto wetu, tunaweza kusema ""imeandikwa, 'Watoto wangu wote watafunzwa katika Bwana...'"

Nena suluhisho – wala si matatiza.
Nena majibu – wala si mahitaji,
Nena na kuamini Neno la Mungu,
naye Shetani atakuwa:
jumla,
kabisa,
kamwe,
ameshindwa!

Nawe utakuwa mshindi!

MASWALI YA KUJIFUNZA

1. Je, kwa nini ni muhimu kwako wewe kujua kuwa Yesu aliacha haki zake kama Mungu na akaishi na kutenda kama mwanadamu alipokuwa ulimwenguni?

2. Je, ni mfano gani unaweza kutoa kuhusu Yesu akitenda katika mamlaka ya mwanadamu akiwa ulimwenguni?

3. Kufuatia mfano wa Yesu, je, unaweza kumshinda vipi Shetani au pepo zake wanapokujaribu ili usimtii Mungu?

Somo La Tano

Yesu Alihudumu katika Mamlaka

MPANGO WA MUNGU KWA WAAMINI WOTE

Yesu, Kama Mwanadamu

Yesu alitenda hapa duniani kama mwanadamu. Alijitoa katika haki zote kama Mungu. Aliteswa katika majaribu kama mwanadamu na alimshinda Shetani.

Alikuwa Yesu wa kibinadamu aliyekuwa na mamlaka hapa duniani. Mamlaka Yake ni kwa sababu alikuwa Mwana wa Adamu, Adamu wa mwisho, wala si kwa sababu alikuwa Mwana wa Mungu.

Yesu alikuja kama Adamu wa Mwisho ili kutimiza yote ambayo Mungu alikusudia alipomuumba Adamu wa Kwanza awe. Kutimiza mpango wa Mungu kwa Adamu wa Kwanza, Yesu alitembea katika mamlaka kamili na utawala hapa duniani.

Ni vyema kuelewa mamlaka ambayo Yesu alitumia. Kama mamlaka haya ni mamlaka ambayo Mungu, katika kuumba, alimpa mwanadamu, basi tunaweza kutembea katika mamlaka hayo hayo leo kama waume kwa wake waliokombolewa.

Luka 10:19 Tazama, nimewapa amri ya kukanyaga nyoka na nge, na nguvu zote za yule adui, wala hakuna kitu kitakachowadhuru.

Ni kupitia tu, kuwa viumbe vipya katika Yesu tunaweza kufanyika waume kwa wake tulioumbwa kuwa katika mpango wa Mungu. Kama tunavyosoma katika Injili na kuona Yesu akitembea kama mwanadamu aliyekamilika ndipo tunaweza kuelewa mpango wa Mungu katika kuishi kwetu na kutembea katika mamlaka na uwezo kamili kila siku ya maisha yetu.

LUKA AELEZA KUHUSU MAMLAKA YA YESU

Ujumbe wa Kwanza

➢ ***"Katika Nguvu za Roho Mtakatifu"***

Yesu alipobatiswa katika mto Yordani, Roho Mtakatifu alikaa juu Yake na kumtia nguvu kwa huduma Yake duniani. Mara tu baada ya haya, Aliongozwa hadi jangwani, ambapo alimshinda Shetani na majaribu yake kwa kunena Neno la Mungu. Kwa kuonyesha mamlaka Yake hapa

duniani kama mwanadamu aliyejazwa Roho Mtakatifu, alikuwa tayari kuanza huduma Yake hapa duniani.

Alianza huduma hii Galilaya, akiwa na nguvu za Roho Mtakatifu na kunena katika mamlaka.

Luka 4:14,16,18-21 Yesu akarudi kwa nguvu za Roho, akenda Galilaya; habari zake zikaenea katika nchi zote za kandokando.

Akaenda Nazareti, hapo alipolelewa; na siku ya sabato akaingia katika sinagogi kama ilivyokuwa desturi yake, akasimama ili asome.

"Roho wa Bwana yu juu yangu, Kwa maana amenitia mafuta kuwahubiri maskini habari njema. Amenituma kuwatangazia wafungwa kufunguliwa kwao, Na vipofu kupata kuona tena, Kuwaacha nuru waliosetwa."

Na kutangaza mwaka wa Bwana uliokubaliwa. Akakifunga chuo, akarudishia mtumishi, akaketi; na watu wote waliokuwamo katika sinagogi wakamkazia macho. Akaanza kuwaambia, " Leo maandiko haya yametimia masikioni mwenu."

(Yesu alikuwa akisoma Isaya 61:1,2)

Ujumbe Wa Pili

Baada ya Yesu kunena Nazareti, alinena akiwa Kapernaumu. Hapo watu walishangaa na mamlaka Yake.

➢ ***Alikuwa na Mamlaka***

Luka 4:31, 32 Akashuka mpaka Kapernaumu, mji wa Galilaya, akawa akiwafundisha siku ya sabato; wakashangaa mno kwa mafundisho yake, kwa kuwa neno lake lilikuwa na uwezo.

➢ ***Mapepo Kutolewa***

ms. 33-35 Na ndani ya sinagogi mlikuwa na mtu mwenye roho ya pepo mchafu, akalia kwa sauti kuu, akisema, Acha! Tuna nini nawe, Yesu wa Nazareti? Umekuja kutuangamiza? Nakujua u nani Mtakatifu wa Mungu!"

Yesu akamkemea, akisema, Fumba kinywa, mtoke. Ndipo yule pepo akamwangusha katikati, akamtoka asimdhuru neno.

Yesu aliamuru pepo kutoka, na kwa sababu lilitambua mamlaka ya Yesu, lilitoka.

➢ ***"Mamlaka na Uwezo"***

ms. 36 Mshango ukawashika wote, wakasemezana wakisema, "Ni neno gani hili, maana awaamuru pepo wachafu kwa uwezo na nguvu, nao hutoka."

Mariko pia aliandika kuhusu huduma ya Yesu Kapernaumu na watu wakashangazwa juu ya mamlaka aliyoonyesha. Mariko aliendelea na kutaja juu ya wenye pepo na watu wagonjwa wakipona.

Mamlaka Juu Ya Mapepo

Yesu alikuwa na mamlaka juu ya mapepo.

ms. 40,41 Na jua lilipokuwa likichwa, wote waliokuwa na wagonjwa wenye maradhi mbali mbali waliwaleta kwake, akaweka mikono yake juu ya kila mmoja akawaponya. Pepo nao waliwatoka watu wengi, wakipiga kelele na kusema, Wewe u Mwana wa Mungu. Akawakemea, asiwaache kunena, kwa sababu walimjua kuwa ndiye Kristo..

Mamlaka Juu Ya Magonjwa Yote

Yesu alikuwa na mamlaka juu ya magonjwa yote.

Marko 1:40,41 Akaja kwake mtu mwenye ukoma, akamsihi na kumpigia magoti, na kumwambia, "Ukitaka, waweza kunitakasa."

Naye akamhurumia, akanyosha mkono wake, akamgusa, akamwambia, "Nataka, takasika."

Mamlaka Juu Ya Mwili wa Mwanadamu

Yesu alinena na mtu aliyekuwa na mkono uliopinda. "Nyosha mkono wako!"

Marko 3:1-3 Akaingia tena katika sinagogi, na palikuwako huko mtu mwenye mkono uliopooza; wakamvizia ili kuona kama atamponya siku ya sabato; wapate kumshitaki. Akamwambia yule mtu mwenye mkono uliopooza, "Simama katikati."

Yesu alijua mtu huyo atapona. Alisema, "Piga hatua mbele."

ms. 4,5 Akawauliza, Ni halali siku ya sabato kutenda mema au kuiua? Wakanyamaza. Akawakazia macho pande zote kwa hasira, akiona huzuni kwa ajili ya ugumu wa mioyo yao,

akamwambia yule mtu, "Nyosha mkono wako." Naye akaunyosha, mkono wake ukawa mzima tena.

Kwa mamlaka, Yesu alinena neno na mtu huyo akanyosha mkono wake na akapona.

Mamlaka Juu Ya Viumbe

➢ ***Kulaani Mti wa Mizabibu***

Yesu alikuwa na mamlaka juu ya mzabibu.

Mathayo 21:19 Akaona mtini mmoja kando ya njia, akauendea, asione kitu juu yake ila majani tu; akauambia, "Yasipatikane matunda kwako tangu leo hata milele," Mtini ukanyauka mara

Mamlaka Juu Ya Vitu

➢ ***Alituliza Dhoruba***

Yesu alinena kwa upepo na bahari katika mamlaka na vikamtii.

Marko 4:35-38 Siku ile kulipokuwa jioni, akawaambia, Na tuvuke mpaka ng'ambo.

Wakauacha mkutano, wakamchukua vile vile alivyo katika chombo. Na vyombo vingine vilikuwako pamoja naye. Ikatokea dhoruba kuu ya upepo, mawimbi yakakipiga chombo hata kikaanza kujaa maji. Naye mwenyewe alikuwapo katika shetri, amelala juu ya mto; wakamwamsha, wakamwambia, Mwalimu, si kitu kwako kuwa tunaangamia?"

Yesu alikemea upepo na akanena na bahari.

ms. 39,40 Akaamka, akaukemea upepo, ukakoma, kukawa shwari kuu.

Akawaambia, "Mbona mmekuwa waoga? Hamna imani bado?"

Yesu alimaanisha kuwa, "Kwa nini mliogopa? Mngetuliza dhoruba. I wapi imani yenu?"

ms. 41 Wakaingiwa na hofu kuu, wakaambiana, "Ni nani huyu, basi, hata upepo na bahari humtii!"

YESU, MFANO WETU

Yesu ni mfano wetu kuhusu jinsi tunavyotembea na kuhudumu katika mamlaka. Kazi Yake hapa duniani kama Adamu wa Mwisho ni mfano jinsi sisi, kama wanadamu waliokombolewa na kurejeshwa, tunaweza kufanya kazi ya Yesu leo. Tunatakiwa kuishi na kuhudumu katika mamlaka aliyokuwa nayo Yesu tunapotenda kazi Zake.

Yohana 14:12 Amin amin, nawaambieni, Yeye aniaminiye mimi, kazi nizifanyazo mimi, yeye naye atazifanya, naam, na kubwa kuliko hizo atafanya, kwa kuwa mimi naenda kwa Baba.

Yesu Alikemea Homa

Yesu alinena kwa ujasiri alipokemea homa kwa mamaye mkewe Petro.

Luka 4:38,39 Akatoka katika sinagogi, akaingia katika nyumba ya Simoni. Naye mkewe Simoni, mamaye mkewe, alikuwa ameshikwa na homa kali, wakamwomba kwa ajili yake. Akasimama karibu naye, akaikemea ile homa, ikamwacha; mara hiyo akaondoka, akawatumikia.

Kumfufua Lazaro

Yesu alinena kwa ujasiri na kwa nguvu kwa sauti kuu katika kaburi la Lazaro.

Yohana 11:43 Naye akiisha kusema hayo, akalia kwa sauti kuu, "Lazaro, njoo huku nje!"

Kufanya Kazi za Yesu

Kila alipoenda Yesu, alihudumu katika ujasiri uliotokana na kutambua mamlaka Yake kama Mwana wa Adamu. Alitoa mamlaka hayo katika nguvu za Roho Mtakatifu, aliponya wagonjwa, akatoa pepo na kufufua wafu. Alifanya hivyo kwa waamini wa nyakati zile na sasa.

Yesu aliwaambia wanafunzi wahudumu katika mamlaka hayo na kutenda kazi ile ile aliyokuwa akitenda.

Mathayo 10:8 Pozeni wagonjwa, fufueni pepo; mmepata bure, toeni bure.

Wanafunzi wangefanya kazi ya Yesu kwa sababu aliwapa mamlaka hayo hayo aliyoishi na kuhudumu.

Luka 10:19 Tazama, nimewapa amri ya kukanyaga nyoka na nge, na nguvu zote za yule adui, wala hakuna kitu kitakachowadhuru.

Mamlaka Yenye Ujasiri

Huduma ya Yesu ilitoa mfano wa ujasiri na nguvu, badala ya hofu na uoga.

2 Timotheo 1:7 Maana Mungu hakutupa roho ya woga, bali ya nguvu na ya upendo na ya moyo wa kiasi.

Yesu kwa ujasiri alihubiri Injili, akatoa pepo na kuwagusa wagonjwa na kuona wakipona alipohudumu katika mamlaka. Yesu, mfano wetu, alituacha na maneno haya ya mwisho.

Marko 16:15-18 Akawaambia, Enendeni ulimwenguni mwote, mkaibubiri Injili kwa kila kiumbe. Aaminiye na kubatizwa ataokoka; asiyeamini, atahukumiwa. Na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio; kwa jina langu watatoa pepo; watasema kwa lugha mpya; watashika nyoka; hata wakinywa kitu cha kufisha, hakitawadhuru kabisa; wataweka mikono yao juu ya wagonjwa, nao watapata afya."

Tunapofuata mfano wa Yesu, kama Adamu wa Mwisho, tutajikuta tukitii maneno ya Yesu, kama muumba, kwa Adamu wa kwanza. Tutajikuta tukitawala na kumiliki dunia hii na vyote vilivyomo pamoja na magonjwa, kufungwa, umaskini na kifo. Kwa mara nyingine tutakuwa tukitenda kile tuliumbwa kutenda.

Hofu Kuu Ya Shetani

Yesu alipohudumu hapa duniani, Shetani lazima alitazama akiwa na hofu kuu. Hapa, Yesu akihudumu kama mwanadamu, alichukua utawala, akinena na kuhudumu katika mamlaka na kwa hiyvo aliharibu kazi ya Shetani.

1 Yohana 3:8b Kwa kusudi hili Mwana wa Mungu alidhihirishwa, ili azivunje kazi za Ibilisi.

Tunapofuata mfano wa Yesu leo, sisi pia tutaweza kuishi na kuhudumu katika mamlaka ya kimungu. Nasi pia tutaiharibu kazi ya Shetani.

MASWALI YA KUJIFUNZA

1. Kulingana na Yohana 5:25-27, Je, Yesu alitenda katika mamlaka kama Mwana wa Mungu, au kama Mwana wa Adamu?

2. Toa mifano ya Yesu akitenda katika mamlaka juu ya vitu, juu ya magonjwa na mapepo.

3. Je, watu walimwitikia vipi Yesu akitenda katika mamlaka hapa duniani?

4. Je, watu wataitikia vipi sasa unapotembea katika mamlaka hapa duniani?

Somo La Sita

Kutoka Msalabani Hadi Enzini

KIFO CHA YESU

Ufalme wa Shetani ulikuwa unaharibiwa, naye Shetani alijua kuwa Yesu lazima auawe. Hila ilifanya kazi ndani ya malaika awali. Ilifanya kazi dhidi ya Adamu na Hawa. Lakini haikufanya kazi dhidi ya Yesu!

Lakini, kwa mara nyingine, Shetani alitumia hila. Aliwahadaa viongozi wa dini ya nyakati zile ili kutaka kifo cha Yesu. Aliutwaa mwili wa Yuda ili kutimiza kusulubiwa kama vile alipoingia mwili wa nyoka ili kuwahadaa Adamu na Hawa.

Shetani alimchukia Yesu sana hata hakutaka tu afe, bali na ateswe na kuangamia. Kila ngome, tawala, mamlaka ya giza na pepo chafu walikutana. Lazima walikuwa wakitayarisha wakati wao wa kushangilia ushindi na shangwe wakati maangamizi yao wenyewe yalifika.

Yesu alihainiwa, akapigwa, akasulubiwa

Mwongo wa Waongo Adanganywa

Shetani, mdanganyifu mkuu mwenyewe alidanganywa. Katika chuki yake, hakutambua kuwa alisababisha kifo cha Mtu ambaye, kwa kifo hicho na kufufuka, angemshinda kabisa na kumkomboa mwanadamu na dhambi zao.

Yesu alilipa deni la dhambi zetu kwa kufa msalabani.

Alituondolea dhambi zetu zote, magonjwa, maradhi na umasikini na kuwekwa mahali pa mateso. Wakati dhambi zote hapa duniani ziliondolewa kwa Yesu na nguvu za Mungu zikamjia. Dunia nzima ilitetemeka wakati huu wa vita vya kiroho. Yesu alimharibu Shetani na pepo zake. Shetani, tangu wakati wa Adamu, alikuwa ameshika watu chini ya mamlaka yake. Yesu alichukua funguo za mamlaka kutoka kwa ibilisi.

JE, NINI KILITENDEKA DUNIANI?

Palikuwa na siku tatu za kivita. Yesu alisema kuwa kama vile Yona alivyokuwa tumboni mwa nyangumi siku tatu, Yeye atakuwa siku tatu chini ya arthi.

Mathayo 12:40 Kwani kama vile Yona alivyokuwa siku tatu mchana na usiku katika tumbo la nyangumi, hivyo ndivyo

Mwana wa Adamu atakavyokuwa siku tatu mchana na usiku katika moyo wa nchi.

- ➢ ***Pasia Kupasuka mara Mbili***
- ➢ ***Tetemeko La Dunia***
- ➢ ***Mawe Kupasuka***
- ➢ ***Makaburi Kufunuliwa***

Wanadamu sasa hawatakiwi kutengana na Mungu. Pasia katika hekalu, iliyo mahali patakatifu pa patakatifu, ilipasuka mara mbili. Dunia ilitikisika sana wakati Yesu alipokata kamba za mauti chini ya arthi.

Mathayo 27:50-53 Naye Yesu akiisha kupaza sauti tena kwa nguvu, akaitoa roho yake. Na tazama, pazia la hekalu likapazuka vipande viwili toka juu hata chini; nchi ikatetemeka; miamba ikapasuka; makaburi yakafunuka; ikainuka miili mingi ya watakatifu waliolala; nao wakiisha kutoka makaburini mwao, baada ya kufufuka kwake, wakauingia mji mtakatifu, wakawatokea wengi.

JE, NINI KILITENDEKA KATIKA ULIMWENGU WA KIROHO?

Vita vilikuwa dhidi ya Yesu aliyetuwakilisha, na Shetani akiwa na mapepo zake.

Wakati Yesu alitundikwa msalabani, Shetani lazima aliwakusanya mapepo wote kushuhudia tukio hilo. Hii ilikuwa ya muhimu sana kwa yeyote kukosa! Yesu alipokufa msalabani, Shetani na mapepo zake lazima walijiandaa kwa vishindo kwa kile walidhani kuwa kikuu.

Haikutosha kwa Shetani kuuona mwili wa Yesu msalabani. Katika chuki, lazima alipaasa sauti, “lazima atupwe chini ya jehanamu. Shetani na pepo zake katika dharau zao na upumbavu lazima walianza kusherehekea, lakini kwa muda tu kwani milango ya Jehanamu ilifungwa nyuma ya Yesu.

Yesu, akiwa na dhambi za wanadamu wote, aliteswa Jehanamu alipoteremshwa chini ya shimo lisilo na mwisho. Hapo, alisimama na kutoa dhambi zote alizobeba na pia za baadaye. Alisizika dhambi zetu isikumbukwe tena kamwe.

Zaburi 103:12 Kama mashariki ilivyo mbali na magharibi, Ndivyo alivyoweka dhambi zetu mbali nasi.

Ilitabiriwa na Daudi

- ➢ ***Kubeba Adhabu ya Dhambi***
- ➢ ***Kubeba Hukumu ya Dhambi***

Daudi alieleza kile kilitendeka kwa Yesu baada ya kifo chake. Akibeba dhambi zetu, alionekana hajiwezi wakati

Shetani alipopanga kumwangamiza. Aliteremka china kabisa Jehanamu. Hapa, wote waliokufa katika kutotii waliwekwa katika mateso na hukumu.

Yesu alienda jehanamu, akibeba adhabu na hukumu ya dhambi zetu.

Zaburi 88:3-7 Maana nafsi yangu imeshiba taabu, Na uhai wangu umekaribia kuzimu. Nimehesabiwa pamoja nao washukao shimoni; Nimekuwa kama mtu asiye na msaada. Miongoni mwao waliokufa nimetupwa, kama waliouawa walalao makaburini. Hao ambao wewe huwakumbuki tena, wametengwa mbali na mkono wako. Mimi umeniliza katika shimo la chini, Katika mahali penye giza vilindini. Ghadhabu yako imenilemea.

Umenitesa kwa mawimbi yako yote.

Daudi pia alitoa unabii juu ya ufufuo wa Yesu.

Zaburi 16:10 Maana hutakuachia kuzimu nafsi yangu, Wala hutamtoa mtakatifu wako aone uharibifu.

Ilitabiriwa Na Isaya

Nabii Isaya alitabiri kifo na kufufuka kwa Yesu.

Isaya 53:8-12 Kwa kuonewa na kuhukumiwa aliondolewa; Na maisha yake ni nani atakayeisimulia? Maana amekatiliwa mbali na nchi ya walio hai, Alipigwa kwa sababu ya makosa ya watu wangu.

Wakamfanyia kaburi pamoja na wabaya; Na pamoja na matajiri katika kufa kwake; Ingawa hakutenda jeuri, Wala hapakuwa na hila kinywani mwake. Lakini BWANA aliridhika kumchubua; Amemhuzunisha:

Utakapofanya nafsi yake kuwa dhabihu kwa dhambi, Ataona uzao wake, ataishi siku nyingi, Na mapenzi ya BWANA yatafanikiwa mkononi mwake; Ataona mazao ya taabu ya nafsi yake, na kuridhika. Kwa maarifa yake mtumishi wangu mwenye haki;

Mwanakondoo wa Mungu

- ➢ ***Alibeba Dhambi za Wengi***
- ➢ ***Aliwaombea Wapotovu***

Naye atayachukua maovu yao, kwa hiyo nitamgawia sehemu pamoja na wakuu, naye atagawanya nyara pamoja nao walio hodari; Kwa sababu alimwaga nafsi yake hata kufa, Akahesabiwa pamoja na hao wakosao.

Walakini alichukua dhambi za watu wengi, Na kuwaombea wakosaji.

Msalabani, Yesu alitimiza kazi ya dhabihu ya mwanakondoo ya Agano la Kale.

Yohana 1:29 Siku ya pili yake amwona Yesu anakuja kwake, akasema, "Tazama, Mwana-kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu!"

Mbuzi wa Azazeli

Wakati Yesu alizibeba dhambi zetu hadi chini ya arthi, Alitimiza kazi inayoonyeshwa na mbuzi wa Azazeli ambaye alizibeba dhambi za watu.

Mambo Ya Walawi 16:10,21,22 Bali yule mbuzi aliyeangukiwa na kura kwa ajili ya Azazeli atawekwa hai mbele za BWANA ili kumfanyia upatanisho, ili kumpeleka jangwani kwa ajili ya Azazeli.

Na Haruni ataweka mikono yake miwili juu ya kichwa cha yule mbuzi aliye hai, na kuungama juu yake uovu wote wa wana wa Israeli, na makosa yao, naam, dhambi zao zote; naye ataziweka juu ya kichwa chake yule mbuzi, kasha atampeleka aende jangwani kwa mkono wa mtu aliye tayari. Na yule mbuzi atachukua juu yake uovu wao wote, mpaka nchi isiyo watu; naye atamwacha mbuzi jangwani.

YESU HANGEWEZA KUSHIKIKA!

Wakati Yesu alizibeba dhambi zetu hadi chini ya arthi, nguvu za Mungu zilikaa juu Yake.

Matendo Ya Mitume 2:27 ... Kwa maana hutaiacha roho yangu katika kuzimu; Wala hutamtoa Mtakatifu wako aone uharibifu.

Malango ya kuzimu haingeweza kushinda dhidi ya Yesu. Kwa kuyavunja malango ya kuzimu, Alinyakua funguo za mauti, kuzimu na kaburi kutoka kwa Shetani.

Ibilisi na Mapepo Washindwa

Historia ya vita vya kale na kushindwa kwa maadui hutoa mawazo maalumu kuhusu kiini cha msitari ufuatao.

Wakolosai 2:15 Akiisha kuzivua enzi na mamlaka, na kuzifanya kuwa mkogo kwa ujasiri, akizishangilia katika msalaba huo.

Nguvu na mamlaka kama tulivyojifunza awali, huonyesha mipango ya Shetani na mapepo zake.

Hapo kale, jeshi liliposhinda adui wao, waliwanyang'anya silaha, kuwavua nguo, kuwafunga kwa nyororo mmoja kwa mwingine, na bila heshima kuwaongoza kama watumwa, katika inchi iliyoshinda vita.

Yesu binafsi alimnyang'anya silaha Shetani na kila pepo. Alitwaa silaha zao kutoka kwao. Aliwatoa nguo. Aliwatia fedheha mbele ya watu.

Wale walioshangilia hapo awali Yesu alipotundikwa, uchi na aibu msalabani, sasa walitiwa aibu pia.

Shetani alishinda Adamu na Hawa

➢ Aliwaacha wakiwa uchi

➢ Aliwanyang'anya mamlaka yao.

Shetani alidhani amemshinda Yesu

➢ Na kumwacha akiwa uchi

➢ Akining'inia msalabani

Hata hivyo, Yesu alimshinda Shetani na Pepo zake

➢ aliwaacha wakiwa uchi

➢ alitwaa mamlaka yao hadi milele!

Ufufuo

Baada ya kulipia adhabu ya dhambi kwa kifo Chake msalabani na kuzitia dhambi zetu chini ya shimo, Yesu alizichukua funguo za mauti, kuzimu na kaburi kutoka kwa Shetani.

Baada ya kumshinda Shetani na kuzivunja nguvu zake juu ya kifo, kaburi halikuweza kuendelea kuweka mwili wa Yesu. Katika mlipuko mkuu, Yesu alifufuka kutoka kwa wafu. Shetani na kila pepo walishindwa!

Waefeso 1:19-21 ... na ubora wa ukuu wa uweza wake ndani yetu tuaminio jinsi ulivyo; kwa kadiri ya utendaji wa nguvu za uweza wake; aliotenda katika Kristo alipomfufua katika wafu, akamweka mkono wake wa kuumu katika ulimwengu wa roho; juu sana kuliko ufalme wote, na mamlaka, na nguvu, na usultani, na kila jina litajwalo, wala si ulimwenguni humu tu, bali katika ule ujao pia.

YESU ALIPAA

Katika Ushindi

Yesu kwa ushindi alipaa mbinguni tena na aliwaongoza wafungwa katika msafara Wake.

Waefeso 4:8-10 "Hivyo husema, Alipopaa juu aliteka mateka, Akawapa wanadamu vipawa."

(Basi neno hilo, Alipaa, maana yake nini kama siyo kusema kwamba yeye naye alishuka mpaka pande zilizo chini za nchi? Naye aliyeshuka ndiye yeye aliyepaa juu sana kupita mbingu zote, ili avijaze vitu vyote.)

Yesu alipowaongoza wafungwa kuwa huru, tunapata picha ya Yesu kama jenerali mshindi akimwongoza adui aliyeshindwa – wasiwe na silaha, wamevuliwa, kufungwa, na kutiwa fedheha mbele ya malaika

mbinguni. Shetani na kila pepo walishindwa kabisa na bila huruma walitiwa aibu wazi.

Yesu alipotwaa funguo za mamlaka kutoka kwa Shetani, alitwaa funguo ambazo Adamu katika kuasi kwake alimpa Shetani. Wakati Yesu alipozichukua funguo hizo za mamlaka kutoka mkononi mwa Shetani, alimnyang'anya Shetani mamlaka yake juu ya mwanadamu na dunia yake. Yesu binafsi alimshinda Shetani na kila pepo zake.

Alipokelewa kwa Furaha

Hakika hakuna maneno ya kueleza furaha ya viumbe wa mbinguni kwa Mwana wa Mungu kurejea pahali pake mbinguni.

Je, mwanadamu anawezaje kueleza ushindi huo wa kurudi?

Daudi alivuviwa kutoa kwetu maelezo kuhusu wakati huu.

Zaburi 24:7-10 Inueni vichwa vyenu, enyi malango, Inukeni, enyi malango ya milele, Mfalme wa utukufu apate kuingia.

Ni nani Mfalme wa utukufu? BWANA mwenye nguvu, hodari, BWANA hodari wa vita.

Inueni vichwa vyenu, enyi malango, Naam, viinueni, enyi malango ya milele, Mfalme wa utukufu apate kuingia.

Ni nani huyu Mfalme wa utukufu? BWANA wa majeshi, Yeye ndiye Mfalme wa utukufu.

Alitangaza Ushindi!

Mtume Yohana anatupatia maneno ya Yesu, alipotangaza ushindi Wake!

Ufunuo Wa Yohana 1:18 Na aliye hai; nami nalikuwa nimekufa, na tazama, ni hai hata milele na milele. Nami ninazo funguo za mauti, na za kuzimu.

YESU ALIKUWA NA FUNGUO!

Yesu alikuja mbinguni akipiga ukelele, "Baba, ninazo funguo! Shetani ameshindwa na ninazo funguo!"

Yesu alikuwa na funguo za mamlaka mkononi mwake alizochukua kutoka kwa Shetani aliyeziiba bustanini alipowahadaa Adamu na Hawa.

Umuhimu wa Funguo

Yesu alizichukua funguo kutoka kwa Shetani, lakini hakuziweka. Alizirejeshea mwanadamu.

Katika ufunuo wa kwanza wa kanisa, Yesu aliwaambia wanafunzi wake kuwa atawapa funguo za ufalme wa mbinguni.

Mathayo 16:19 Nami nitakupa wewe funguo za ufalme wa mbinguni; na lo lote utakalolifunga duniani,litakuwa limefungwa mbinguni, na lo lote utakalolifungua duniani, litakuwa limefunguliwa mbinguni.

Katika Isaya panatajwa tena funguo.

Isaya 22:22 Na ufunguo wa nyumba ya Daudi nitauweka begani mwake; yeye atafungua wala hapana atakayefunga; naye atafunga wala hapana atakayefungua.

Awali, funguo zilikuwa kubwa, nzito na rembo. Matajiri mara nyingi walizibeba begani kwa ajili ya uzito, lakini hasa kwa urembo wake. Mara nyingi watumwa wawili au watatu wangemfwata tajiri wakizibeba funguo begani mwao. Hii ilionyesha utajiri.

Wakati Isaya alipotoa unabii juu ya kuja kwa Masiya, alionyesha kiini cha funguo kubebwa begani.

Isaya 9:6a Maana kwa ajili yetu mototo amezaliwa, Tumepewa mototo mwanamume; Na uweza wa kifalme utakuwa begani mwake.

Funguo, serikali na mamlaka, vilikuwa katika mikono ya Yesu! Yesu alizichukua funguo hizo akazipa kanisa Lake.

Mamlaka hapa duniani
imerejeshewa
kwa mwanadamu

MASWALI YA KUJIFUNZA

1. Baada ya kifo chake msalabani, je, Yesu alizipeleka wapi dhambi zetu?

2. Je, Maandiko yana maana gani inaposema Yesu aliharibu ngome na nguvu na kuziweka aibu kwa wazi?

3. Je, nini maana ya funguo ambazo Yesu anataja katika Ufunuo 1:18?

Somo La Saba

Mamlaka Kurejeshewa kwa Mwanadamu

KAZI YA YESU IMEMALIZIKA!

Kazi ya Yesu ilikuwa, na bado ni, imekamilika!

Mungu alipowaumba Adamu na Hawa, aliwapa mamlaka ya kutawala dunia hii. Kupitia kwa dhambi, walipoteza mamlaka haya kwa Shetani. Kisha Yesu, mwanadamu kamili, Adamu wa Mwisho, alitembea hapa duniani katika kila hali ambayo Mungu alimuumba mwanadamu atende. Yesu alizichukua dhambi za wanadamu wote juu Yake na akafa msalabani akilipia adhabu ya dhambi hizo.

Alikufa kwa wanadamu wote. Alizitoa dhambi hizo chini ya shimo na nguvu za Mungu mwenyewe zikamjia Yesu. Alimshinda Shetani na pepo zote katika lango la kuzimu. Yesu alizichukua funguo za mamlaka.

Yesu alichukua kila kitu Shetani alikuwa ameiba kwa mwanadamu. Vyote Mungu alivyowaumba Adamu na Hawa wawe navyo ambapo Yesu aliwarejeshea wanadamu.

Yesu aliponena juu ya kanisa atakalojenga, Alisema,

Mathayo 16:18b,19 Na juu ya mwamba huu nitalijenga kanisa langu, wala milango ya kuzimu haitalishinda. Nami nitakupa wewe funguo za ufalme wa mbinguni; na lo lote utakalolifunga duniani, litakuwa limefungwa mbinguni; na lo lote utakalolifungua duniani, litakuwa limefunguliwa mbinguni..

Yesu Mbinguni

Mwandishi wa kitabu cha Waebrania anatuonyesha nafasi ya Yesu sasa.

Waebrania 10:12,13 Lakini huyu, alipokwisha kutoa kwa ajili ya dhambi dhabihu moja idumuyo hata milele, aliketi mkono wa kuume wa Mungu; tangu hapo akingojea hata adui zake wawekwe kuwa chini ya miguu yake.

Yesu ameketi katika mkono wa kuume wa Baba.

Daudi pia alitabiri nafasi ya Yesu ya sasa.

Zaburi 110:1 Neno la BWANA kwa Bwana wangu, "Uketi mkono wangu wa kuume, Hata niwafanyao adui zako kuwa chini ya miguu yako."

Daudi alitabiri Yesu ataketi mkono wa kuume wa Baba.

Yesu Anasubiri

Daudi na mwandishi wa kitabu cha Waebrania alitwambia kuwa Yesu anafanya zaidi ya kuketi katika mkono wa kuume wa Baba. Yesu anasubiri adui Zake wafanyike miguu ya kiti Chake.

Je, nani atafanya adui Zake wawe miguu ya kiti Chake?

Yesu anangoja waliokombolewa kutambua mamlaka yao na kuonyesha kuwa Shetani ni adui aliyeshindwa. Kazi ya Yesu imekamilika. Yeye anasubiri adui zake wafanyike miguu ya kiti Chake. Ni kazi ya waamini kumweka Shetani mahali pake. Waamini lazima wamweke Shetani na pepo zake chini ya miguu ya Yesu.

Yesu amefanya kila kitu alichotakiwa kufanya. Sasa jukumu ni letu. Sisi ni mwili Wake hapa duniani. Sisi ni mikono Yake, miguu Yake. Ni sisi ndio tunatakiwa kutawala dunia yetu leo.

OMBI LA PAULO

Mtume Paulo aliomba ombi la muhimu na lenye nguvu kwa wateule wote. Ombi lake lilichukua nafasi ya Yesu akiwa mkono wa kuume wa Baba, nafasi yetu, nguvu zetu na majukumu yetu.

Waefeso 1:18-23 ... macho ya mioyo yenu yatiwe nuru, mjue tumaini la mwito wake jinsi lilivyo; na utajiri wa utukufu wa urithi wake katika watakatifu jinsi ulivyo; na ubora wa ukuu wa uweza wake ndani yetu tuaminio jinsi ulivyo; kwa kadiri ya utendaji wa nguvu za uweza wake kadiri ya utendaji wa nguvu za uweza wake; aliotenda katika Kristo alipomfufua katika wafu, akamweka mkono wake wa kuume katika ulimwengu wa roho; juu sana kuliko ufalme wote, na mamlaka, na nguvu, na usultani, na kila jina litajwalo, wala si ulimwenguni humu tu, bali chini ya miguu yake, akamweka awe kichwa juu ya miguu yake, akamweka awe kichwa juu ya vitu vyote kwa ajili ya kanisa; ambalo ndilo mwili wake, ukamilifu wake anayekamilika kwa vyote katika vyote.

Nafasi Ya Yesu

Kulingana na mtume Paulo,

- ➢ Yesu amefufuka kutoka kwa wafu
- ➢ Ameketi mkono wa kuume mbinguni
- ➢ Yu juu ya tawala, nguvu, uwezo, na mamlaka
- ➢ Yu juu ya kila vyeo vinavyoweza kutolewa
- ➢ Vitu vyote viko chini ya miguu Yake
- ➢ Amechaguliwa awe kichwa/kiongozi

Yesu yuko juu ya nguvu za mapepo. Yesu yu juu ya vyeo vinavyotolewa, au kuwai kutolewa. Vitu vyote viko chini ya miguu Yake.

Kipimo Cha Nguvu

Kuna aina mbili ya nguvu: moja katika Agano la Kale na nyingine katika Agano Jipya.

Katika Agano la Kale kipimo cha nguvu kilikuwa kugawanyika kwa Bahari Nyekundu.

Katika Agano Jipya kipimo cha nguvu kilikuwa na bado ni, nguvu katika ufufuo wa Yesu Kristo.

Paulo aliandika,

Waefeso 1:19b,20a kwa kadiri ya utendaji wa nguvu za uweza wake kadiri ya utendaji wa nguvu za uweza wake; aliotenda katika Kristo alipomfufua katika wafu.

Nafasi Ya Waamini

Mtume Paulo alisema kuwa waamini watafunuliwa, na kuwa watafahamu:

- ➢ Matumaini ya mwito Wake
- ➢ Utajiri wa utukufu wa urithi Wake
- ➢ Ukuu na umahiri wa nguvu Zake
- ➢ Sisi tu mwili Wake
- ➢ Sisi tumejazwa na Yeye

Tunatakiwa kuwa na ufahamu wa utajiri katika utukufu wa urithi Wake na ukuu wa nguvu Zake kwetu tunaoamini. Tunatakiwa kutenda katika nguvu zile kuu zilizomfufua Yesu kutoka kwa wafu!

KUJAZWA NAYE

Paulo aliombea “kanisa, ambalo ni mwili wake, kujazwa kwake ajazaye wote katika yote.”

Ikiwa sisi, kanisa Lake, tunatimiza tupu au uwazi katika Mwana wa Mungu, je, ni lini utupu huu ulitokea? Labda utupu huu ulitokana na wakati Lusifa, makerubi afunikaye, alipotupwa toka mbinguni pamoja na malaika waliomfuata katika kuasi kwake.

Ezekieli 28:14 Wewe ulikuwa kerubi mwenye kutiwa mafuta afunikaye; nami nalikuweka hata ukawa juu ya mlima mtakatifu wa Mungu umetembea huko na huko kati ya mawe ya moto.

Uongozi wa Kimalaika

Kama vile pana utatu katika Mungu, hapo pia palionekana kuna utatu katika uongozi wa malaika. Palikuwa Mikaili, Lusifa na Gabrieli.

➢ ***Theluthu Moja***

Lusifa alipoasi, ilisemekana kuwa "malaika zake" walitupwa nje pamoja naye.

Ufunuo Wa Yohana 12:7-9 Kulikuwa na vita mbinguni; Mikaeli na malaika zake wakapigana na yule joka, yule joka naye akapigana nao pamoja na malaika zake; nao hawakushinda, wala mahali pao hapakuonekana tena mbinguni.

Yule joka akatupwa, yule mkubwa, nyoka wa zamani, aitwaye Ibilisi na Shetani, audanganyaye ulimwengu wote; akatupwa hata nchi, na malaika zake wakatupwa pamoja naye.

Malaika walioelezwa kuwa malaika wa Shetani na waliotupwa chini arithini wakiwa naye, walikuwa theluthu moja ya malaika wote mbinguni.

Ufunuo Wa Yohana 12:4a Na mkia wake wakokota theluthi ya nyota za mbinguni, na kuziangusha katika nchi.

➢ ***Mikaili***

Mikaili tu ndiye aliyeitwa malaika mkuu.

Waraka Wa Yuda 1:9a lakini Mikaeli, malaika mkuu...

Alikuwa Mikaili na "malaika wake" ambao walikuwa jeshi kupigana dhidi ya Shetani, "joka na malaika zake."

Ufunuo Wa Yohana 12:7 Kulikuwa na vita mbinguni; Mikaeli na malaika zake wakapigana...

Labda malaika mkuu, Mikaili na theluthu ya malaika chini ya amri yake, walimhudumia Baba.

➢ ***Gabrieli***

Labda Gabrieli, ambaye kila mara huonekana kama malaika wa ujumbe, na theluthu ya malaika chini ya amri yake; walihudumia Roho Mtakatifu.

Alimtokea Zekaria, ili ampe ujumbe kuwa mkewe Elizabeti atamzaa mwana "atakayejazwa na Roho Mtakatifu hata tangu kuzaliwa."

Luka 1:19 Malaika akamjibu akamwambia, "Mimi ni Gabrieli, nimetumwa niseme nawe, na kukupasha habari hizi njema."

Gabrieli pia alimtokea bikira aitwaye Mariamu.

Luka 1:30,31,35 Malaika akamwambia, Usiogope, Mariamu, kwa maana umepata neema kwa Mungu. "Tazama, utachukua

mamba na kuzaa mototo mwanamume, na jina lake utamwita Yesu."

Mariamu aliuliza, "Je, itawezekanaje ... maana simjui mwanamume?"

Malaika akajibu akamwambia, "Roho Mtakatifu atakujilia juu yako, na nguvu zake Aliye juu zitakufunika kama kivuli; kwa sababu hiyo hicho kitakachozaliwa kitaitwa kitakatifu, Mwana wa Mungu."

Gabrieli alionyesha kazi ya Roho Mtakatifu.

➢ ***Lusifa***

Je, inawezekana kuwa, Lusifa na malaika zake walimutumikia Mwana wa Mungu?

Lusifa alihudumu kama makerubi wa kufunika, na alijulikana kwa kufunika kila upande wa Kiti cha Neema. Alikuwa kando ya kiti cha enzi cha Mungu. Kama tulivyoona, kufunika kulikuwa ni huduma ya sifa na kuabudu.

Kisha, ghafla katika kuasi, Lusifa na malaika wake wote walitupwa toka mbinguni. Je, pengo hili lingejazwa vipi?

Je, Baba alimwuliza Mikaili na Gabrieli kuwapa malaika wengine kuchukua nyadhifa hizo na kumhudumia Mwana? Hatuna habari iliyochapishwa kuonyesha hayo.

Je, pana uwezekano kuwa, Mungu alikuwa na mpango bora alipomwumba mwanadamu katika mfano Wake, wawe wakimuabudu, kukaa naye kule mbinguni, kuwa upande wake na kutawala na kuongoza Naye milele?

Uwazi Ukajazwa

Waume kwa Wake, wameumbwa katika mfano wa Mungu, na wanaweza tu kukamilika na kutimiza ikiwa Muumba tena atawavuvia pumzi Mwenyewe ndani yao wakati wa wokovu. Anajaza uwazi katika maisha Yeye mwenyewe. Sasa mwili Wake ni sharti utimize uwazi ndani yao ili wajitolee Kwake katika huduma ya sifa na kuabudu.

Hapo mwanzo, palikuwa na huduma moja tu, huduma ya sifa na kuabudu. Wakati hiyo ilisimama, huduma zingine nyingi ziliitajika – huduma za uponyaji, kukombolewa, kurejeshwa, na nyingine.

Je, panawezekana kuwa wakati huduma ya sifa na kuabudu ikirejeshwa kanisani, huduma hizi zingine zisiwe na umuhimu katika mwili wa Kristo kama vile zilivyo sasa?

Tunapotumia muda zaidi katika huduma ya sifa na kumwabudu Mungu, tutagundua kuwa kuna upungufu

katika uponyaji au ukombozi au huduma nyingine katika maisha yetu.

Sisi tu wa muhimu kwa Mungu! Inatupasa tuwe tunatimiza Kwake. Inatupasa kumuhudumia katika sifa na kuabudu. Tunapofanya hivyo, sisi kama mwili Wake tunakuwa "tumejazwa Naye ajazaye wote ndani ya yote."

Waefeso 1:22,23 Akavitia vitu vyote chini ya miguu yake, akamweka awe kichwa juu ya vitu vyote kwa ajili ya kanisa; ambalo ndilo mwili wake, ukamilifu wake anayekamilika kwa vyote katika vyote.

Tunaposifu na kumwabudu Mungu, hatutimizi tu kazi ya awali ya Lusifa na malaika zake, tunaonyesha kweli kuwa wameshinda na hawana tena nafasi mbinguni. Tunawatia aibu na kuwaweka chini ya miguu yetu. Tunapocheza mbele za Bwana, tunamponda Shetani na kumushinda kwa tendo la miguu yetu.

Kumbukumbu: Kwa kujifunza kwa undani juu ya sifa na kuabudu, soma the *Praise And Worship Manual* na A.L. na Joyce Gill.

NAMAANA YA HII KWETU

Kwa kazi ya Yesu msalabani na kwa matukio yaliyofuata, Shetani ameshindwa! Kila pepo limeshindwa! Yesu aliwashinda na kuwaweka patupu! Aliweka "sufuri" ndani yao.

- Kwa nini tunamuruhusu Shetani kutushinda sasa?
- Kwa nini tunamruhusu kunyakua nyumba zetu, miji yetu, mataifa zetu?
- Kwa nini tunamruhusu aweke magonjwa juu yetu?
- Kwa nini tunakubali umasikini?

Jibu ni kuwa ni lazima tujifunze na kufahamu kile tumepewa katika Yesu Kristo. Lazima tutambue mamlaka yetu iliyorejeshwa.

Tumekombolewa!

Wakati mtume Paulo aliandika kwa Wakolosai, alisema tume:

- Okolewa
- Badilishwa
- Kombolewa
- Samehewa

Wakolosai 1:13,14 Naye alituokoa katika nguvu za giza, akatuhamisha na kutuingiza katika ufalme wa Mwana wa

pendo lake, ambaye katika yeye tuna ukombozi, yaani, msamaha wa dhambi.

Ufalme Uko Hapa

Je, ufalme wa Mwana ni upi?

Jesu alipowafunza wanafunzi wake kuomba, aliomba maneno haya

Mathayo 6:10 Mapenzi yako yatimizwe, hapa duniani kama huko mbinguni.

Ufalme wa Mungu si kitu katika siku za usoni. Bali uko hapa sasa. Tumeokolewa na utawala wa giza na kuletwa katika ufalme wa Mwana katika kukombolewa na msamaha wa dhambi zetu.

Tukiwa na ufahamu wa mamlaka yetu iliyorejeshwa, tunaweza kuwa waume kwa wake watakaokuwa na uwezo mkuu kuendeleza ufalme wa mbinguni hapa duniani.

Mathayo 11:12 Tangu siku za Yohana Mbatizaji hata sasa ufalme wa mbinguni hupatikana kwa nguvu, nao wenye nguvu wauteka.

Paulo aliendelea na maelezo mazuri kuhusu Yesu.

Wakolosai 1:15-18 Naye ni mfano wa Mungu asiyeonekana, mzaliwa wa kwanza wa viumbe vyote. Kwa kuwa katika yeye vitu vyote viliumbwa, vilivyo mbinguni na vilivyo juu ya nchi, vinavyoonekana na visivyoonekana; ikiwa ni vitu vya enzi, au usultani, au enzi, au mamlaka; vitu vyote viliumbwa kwa njia yake, na kwa ajili yake. Naye amekuwako kabla ya vitu vyote, na vitu vyote hushikana katika yeye. Naye ndiye kichwa cha mwili, yaani, cha kanisa; naye ni mwanzo, ni mzaliwa wa kwanza katika wafu, ili kwamba awe mtangulizi katika yote.

Yesu Ambaye ni Kichwa

Yesu:

- **Ni mfano wa Mungu**
- **Muumba wa vyote**
- **Alikuwa kabla ya vitu vyote**
- **Anashikilia vitu vyote pamoja**
- **Ni kichwa cha mwili, kanisa**
- **Ni mwanzo, kifungua mimba kutoka kwa wafu.**

Yesu ni kichwa chetu. Sisi ni mwili Wake. Mwili Wake umetengenezwa na waamini wote. Kama mwili Wake, tunaelezwa kuwa tayari tumenyakuliwa kutoka kwa tawala za Shetani na kubadilishwa kwa ufalme mpya ambapo tutatawala na Yesu, Mwana wa Mungu.

Tunaelezwa kama waliokombolewa kabisa tumesamehewa dhambi zote.

Kichwa cha mwili, Yesu, yu mbinguni. Sehemu nyingine ya mwili Wake na, pia miguu, iko duniani. Ni hapa duniani ambapo mwanadamu lazima atimize kazi yake ya mamlaka tele. Ni hapa ndipo tunatakiwa kuendeleza ufalme wa Mungu katika vita kamili vya kiroho.

NAFASI YA SHETANI

Chini ya Miguu ya Yesu

Mungu alimweka Shetani chini ya miguu ya Yesu na kumchagua Yesu awe kichwa juu ya kila kitu kuhusu kanisa.

Waefeso 1:22 Akavitia vitu vyote chini ya miguu yake, akamweka awe kichwa juu ya vitu vyote kwa ajili ya kanisa..

Chini ya Miguu Yetu

Warumi 16:20a Naye Mungu wa amani atamseta Shetani chini ya miguu yenu upesi.

Kuwa chini ya miguu ya mtu ni mfano wa kushindwa kabisa na kutawaliwa. Ni picha ya mamlaka kamili na utawala.

Mwanzo 3:15 Nami nitaweka uadui kati yako na huyo mwanamke, na kati ya uzao wako na uzao wake; huo utakuponda kichwa, na wewe utamponda kisigino.

Chini ya Mamlaka Yetu

Shetani yu chini ya miguu ya Yesu kwa sababu Yesu alimshinda kabisa na kupaa juu yake na pepo zake zote. Shetani na pepo zake sasa watawekwa chini ya miguu yetu tunapogundua mamlaka yetu na kuyatumia duniani.

Kukanyagwa

Luka anatuonyesha mfano wa nafasi au msimamo wa Shetani. Ni sharti akanyagwe chini ya miguu yetu. Pia tumeahidiwa kuwa hakuna kitakachotudhuru katika hali yoyote.

Luka 10:19 Tazama, nimewapa amri ya kukanyaga nyoka na nge, na nguvu zote za yule adui, wala hakuna kitu kitakachowadhuru.

Mwanadamu baada ya kuokolewa, kuletwa, kukombolewa, kusamehewa kabisa na kurejeshwa katika mfano wa Mungu duniani, sasa atamkanyaga Shetani chini ya miguu na kuonyesha kuwa yeye ni adui aliyeshindwa.

Isaya alipoeleza mwisho wa Shetani, alimtaja kama mmoja anayekanyagwa chini ya miguu.

Isaya 14:18-20 Wafalme wote wa mataifa wamezik wa wote kwa heshima, kila mmoja ndani ya nyumba yake mwenyewe; Bali wewe umetupwa mbali na kaburi lako, Kama chipkizi lililochukiza kabisa; kama vasi la wale waliouawa, Wale aliochomwa kwa upanga, Wale ashukao mpaka misingi ya shimo; kama mzoga uliokanyagwa chini ya miguu. Hutaungamanishwa pamoja nao katika mazishi, Kwa maana umeiharibu nchi yako, umewaua watu wako kizazi chao watendao uovu hakitatajwa milele..

MFULULIZO WA AMRI

Yesu aliporudi kwa Baba Yake, aliweka kando haki zake kama Mwana wa Adamu na kutwaa tena juu Yake haki Zake zote kama Mwana wa Mungu.

Haki ya Mwanadamu Duniani

Kama Mungu, Yeye sasa hatawali hapa duniani kwa sababu, alitoa utawala wote kwa mwanadamu.

Ni mwanadamu ndiye anatakiwa kumweka Shetani chini ya miguu yake kama alivyoumbwa kufanya.

Nabii Isaya alitueleza unabii mzuri na wa kutia moyo.

- ➢ Katika haki utaimarishwa
- ➢ Mateso yatakuwa mbali nawe.
- ➢ Wewe huogopi kitu
- ➢ Hofu kuu haitakuja karibu nawe
- ➢ Yeyote anayeinuka dhidi yako atasalimu amri
- ➢ Hakuna silaha iliyoundwa dhidi yako itafaulu
- ➢ Utakana kila ulimi utakaokuja kinyume chako

Isaya14-17 "Aliyeufanya ulimwengu ukiwa, akaipindua miji yake; Asiyewafungua wafungwa wake waende wao?"

Kwa kweli watakusanyika,, lakini si kwa sababu Yangu. Yeyote atakayekusanyika dhidi yako ataanguka kwa ajili yako.

Tazama, nimeumba mhunzi anayepuliza makaa katika moto, anayeleta chombo kwa kazi yake, na nimemwumba mwaribifu aiharibu. Hakuna silaha iliyoundwa kinyume chako itafaulu, na kila ulimi unaoinuka dhidi yako katika hukumu utahukumu. Huu ni urithi wa watumwa wa Bwana, na haki yao inatoka kwangu," asema Bwana..

Urithi wetu ni kitu ambacho ni chetu katika haki ya kuzaliwa.

Isaya alitabiri,

Huu ni urithi wa watumishi wa Bwana!

MASWALI YA KUJIFUNZA

1. Ikiwa vitu vyote viko chini ya miguu ya Yesu, kwa nini ibilisi na nguvu za mapepo bado zinaendelea na kazi ya uovu wao hapa duniani?

2. Kwa nini Mungu anamruhusu Shetani kuendelea na uovu duniani baada ya Yesu kumshinda yeye kwa kifo Chake msalabani na ufufuo Wake?

3. Je, ni mabadiliko gani maishani mwako ambayo yatafaa ikiwa utatembea katika mamlaka – kuonyesha kuwa Shetani ni adui aliyeshindwa?

NINI KILITENDEKA

MIAKA 2,000 BAADAYE – SHETANI AMEYATWAA TENA MAMLAKA HAYO

Miaka 2,000 baadaye tunaona:
Watu kuishi bila
jina la Yesu.
Watu kuishi katika umaskini
Watu kuishi katika dhambi
watu kuishi katika kushindwa
Watu kupewa talaka
watu na wana wao wakitumia madawa ya kulevya
watu kuabudu dini za uwongo.

Kwa nini Shetani anafanya hivi kama
mungu wa dunia hii?

Ameshindwa na Yesu
na kuwekwa mahali pasipo na uwezo.
Yesu amefanya kazi yake kutukomboa sisi!

Je, tumefanya nafasi yetu
kwa nguvu zetu – utawala – mamlaka?

Kuiba, Kuua na Kuharibu

Katika nyakati zote, kusudi la Shetani halijabadilika.

Yohana 10:10a Mwivi haji ila aibe na kuchinja na kuharibu; mimi nalikuja ili wawe na uzima, kasha wawe nao tele.

Ibilisi anatuchukia sana hata ametoa amri kwa jeshi lake la mapepo ili kuiba, kuua na kuaharibu! Jukumu limetolewa ili tuibiwe yaliyo muhimu katika maisha na huduma zetu. Amri zimetolewa ili tuuliwe katika roho za udhaifu, kuua na kujitia kitanzi. Ajali mbaya hujaribiwa maishani mwetu. Ibilisi ametoa amri yake, “chochote itagharimu lazima wauawe!”

Ikiwa mapepo hayawezi kutuua, labda, wanaweza kutoa habari kuwa wametuzuia au kutukomesha katika kutimiza huduma zetu tulizopewa na Mungu.

Kutumia Pepo Za Udhaifu

Shetani hujaribu kuiba afya yetu kwa kutumia pepo za udhaifu.

Luka 13:11-13 Na tazama, palikuwa na mwanamke aliyekuwa na pepo wa udhaifu muda wa miaka kumi na minane, naye amepindana, hawezi kujinyosha kabisa. Yesu alipomwona alimwita, akamwambia, Mama, umefunguliwa katika udhaifu wako. Akaweka mikono yake juu yake, naye akanyoka mara hiyo, akamtukuza Mungu.

Yohana 5:5 Na hapa palikuwa na mtu, ambaye amekuwa hawezi muda wa miaka thelathini na minane.

Kufinya, Kufadhaisha na Kusaliti

Mtume Paulo anaeleza mapigo ya Shetani maishani mwake na huduma. Inatia moyo kuona kuwa mipango yote ya Shetani ilishindwa kuzuia huduma ya Paulo kwa Bwana.

2 Wakorintho 4:8,9 Pande zote twadhikika, bali hatusongwi; twaona shaka, bali hatukati tama; twaudhiwa, bali hatuangamizwi; twatupwa chini, bali hatuangamizwi.

Shetani hupiga vyote vyenye ubora na manufaa maishani mwetu.

- ➢ Ndoa
- ➢ Watoto
- ➢ Jamii
- ➢ Marafiki
- ➢ Huduma

➢ Afya

➢ Furaha

➢ Amani

KINGA YETU

Tambua Mbinu ya Adui Wako

Waume kwa wake huangamia kwa kukosa hekima. Ikiwa wanaenda kumkomesha Shetani asifikie lengo lake la kuiba, kuua na kuharibu, ni lazima wamtambue adui na mbinu zake.

➢ Shetani huleta mauti – Mungu huleta uzima.

➢ Shetani huleta chuki – Mungu huleta upendo.

Yesu

➢ ***Aliharibu Mauti***

Yesu ameharibu mauti na kuleta uzima na kuishi milele.

2 Timotheo 1:10...na sasa inadhihirishwa kwa kufununuliwa kwake mwokozi wetu Kristo Yesu; aliyebatili mauti, na kuufunua uzima na kutokuharibika, kwa ile Injili.

➢ ***Aliharibu Nguvu za Shetani***

Yesu ameharibu ibilisi na kutuweka huru kutokana na hofu ya kifo na mapepo.

Waebrania 2:14,15 Basi, kwa kuwa watoto wameshiriki damu na mwili, yeye naye vivyo hivyo alishiriki yayo hayo, ili kwa njia ya mauti amhasibu yeye aliyekuwa na nguvu za mauti, yaani, Ibilisi, awaache huru wale ambao kwamba maisha yao yote kwa hofu ya mauti walikuwa katika hali ya utumwa

➢ ***Alitukomboa Kutoka kwa Utumwa***

Shetani hana haki ya kutuweka katika utumwa. Sisi, katika imani ndani ya Yesu Kristo, tumekombolewa kutoka kwa kufungwa na utumwa wa Shetani na ufalme Wake.

Wakati Shetani au pepo zake huja kuiba, kuua na kuharibu, ni sharti wasitukute tukiwa wanyonge na bila kinga. Badala yake kupitia ufahamu wa Neno la Mungu, lazima tuwe tumefunikwa na damu ya Yesu. Lazima tusimame imara na chepeo yetu ya imani. Lazima kwa ujasiri na bila uoga tunene Neno la Mungu kama nabii Isaya.

Isaya 54:17a Kila silaha itakayofanyika juu yako haitafanikiwa

Noa Upanga Wako

Ikiwa tutakosa Neno akilini mwetu na rohoni, hatutaweza kumshinda Shetani na wafwasi wake kwa Neno. Yesu anataka tuwe na vingi kila sehemu maishani mwetu. Ikiwa hatuna hivi, basi tumeibiwa na Shetani.

Lazima tutambue sisi tuko ndani ya Kristo ili kutambua kuwa tayari tumeshinda vita!

Mfano wa Mpanzi – Ufunuo wa Ushindi

Mfano wa Mpanzi

Marko 4:3-8

"Sikilizeni! Tazama, mpanzi alitoka kwenda kupanda.

Ikawa alipokuwa akipanda, mbegu nyingine ilianguka kando ya njia wakaja ndege wakaila.

Nyingine ikaanguka penye mwamba, pasipokuwa na udongo mwingi, mara ikaota kwa kuwa na udongo haba, hata jua lilipozuka iliungua, na kwa kuwa haina mizizi, ikanyauka.

Nyingine ikaanguka penye miiba, ile miiba ikamea ikaisonga, isizae matunda.

Nyingine zikaanguka penye udongo ulio mzuri, zikazaa, moja thelathini, moja sitini, na moja mia."

Yesu Akaelezea Mfano

Marko 4:14-20

"Mpanzi huyo hulipanda Neno.

Hawa ndio walio kando ya njia lipandwapo Neno, nao wakiisha kusikia, mara huja Shetani, akaliondoa lile neno lililopandwa mioyoni mwao.

Kadhalika na hawa ndio wapandwao penye miamba, ambao kwamba wakiisha kulisikia lile neno, mara hulipokea kwa furaha, ila hawana mizizi ndani yao, bali hudumu muda mchache, kasha ikitokea dhiki au udhia kwa ajili ya lile neno, mara hujikwaa.

Na hawa ndio wale wapandwao penye miiba, ni watu walisikiao lile neno, na shuguli za dunia, na udanganyifu wa mali, na tama za mambo mengine halizai.

Na hawa ndio waliopandwa penye udongo ulio mzuri, ni watu walisikiao lile Neno na kulipokea, na kuzaa matunda, mmoja thelathini, mmoja sitini, na mmoja mia."

Wengi wameelewa mfano huu kuwa mbegu ya wokovu ikipandwa na matokeo tofauti ya uinjilisti na hivyo ni kweli.

Lakini, Yesu alisema kuwa alimaanisha Neno la Mungu. Yesu alifundisha kuwa tunapopokea ufahamu mpya juu ya Neno la Mungu, Shetani atafika mara moja kuliiba kutoka kwetu. Hii inaweza kuwa Neno la Mungu kama katika kila sehemu ya maisha yetu.

Je, ni mara ngapi umesikia watu wakisema kuwa baada ya wakati mzuri na Bwana majaribu mara nyingi yatakuja? Baada ya semina nzuri, kila kitu huonekana "kikienda kombo". Yesu alisema kuwa huyu ni Shetani akija kuiba Neno.

Moja Kati ya Vitu Vitatu

Neno linapopandwa vitu vitatu hufanyika:

- ➢ Shetani anaweza kuiba Neno mara moja ikiwa tutahuzunika Shetani anapoleta mateso na kusaliti.
- ➢ Neno linaweza kupotezwa na mahangaiko ya maisha haya, hila za mali au tamaa ya dhambi.
- ➢ Neno liruhusiwe kupata mizizi na kuchipuka.

Mateso /Kusaliti

Yesu aliwaonya kuwa mateso na majaribu yatatokea kwa ajili ya ulimwengu.

Marko 4:17 ... ila hawana mizizi ndani yao, bali hudumu muda mchache; kasha ikitokea dhiki au udhia kwa ajili ya lile neno, mara hujikwaa.

Shetani Huja Ghafula

Shetani anajua kuwa ufunuo wa Neno la Mungu ukibaki ndani ya mioyo yetu, kwa Neno hilo hilo, anaweza kushindwa. Ingawa anazo mbinu nyingi ili kuleta kushindwa katika maisha yetu, kipa umbele chake kila mara ni kuiba ufunuo wa Neno la Mungu. Yesu alisema Shetani huja wanaposikia.

Marko 4:15 hawa ndio walio kando ya njia lipandwapo neno; nao wakiisha kusikia, mara huja Shetani, akaliondoa lile neno lililopandwa mioyoni mwao.

YESU ALITULIZA BAHARI

Yesu alipomaliza kufundisha, Yeye pamoja na wanafunzi Wake waliingia mashuani. Baadaye Yesu akasinzia pale nyuma. Kisha Shetani akaja na mahangaiko ya dunia hii.

Marko 4:35-41 Siku ile kulipokuwa jioni, akawaambia, Na tuvuke mpaka ng'ambo. Wakauacha mkutano, wakamchukua vilevile alivyo katika chombo.

Na vyombo vingine vilikuwako pamoja naye.

katokea dhoruba kuu ya upepo, mawimbi yakakipiga chombo hata kikaanza kujaa maji. Naye mwenyewe alikuwapo katika shetri, amelala juu yam to; wakamwamsha, wakamwambia, Mwalimu, si kitu kwako kuwa tunaangamia? Akaamka, akaukemea upepo, akaiambia bahari, Nyamaza, utulie, Upepo ukakoma, kukawa shwari kuu. Akawaambia, Mbona mmekuwa waoga? Hamna imani bado? Wakaingiwa na hofu kuu, wakaambiana, Ni nani huyu, basi hata upepo na bahari humtii!"

Dhoruba iliyokuja ilikuwa mojawapo wa mateso na masaliti amabyo Yesu alisema yataletwa na Shetani punde tu Neno linapopandwa.

Angalia mtazamo wa wanafunzi. Walisumbuka. "Mwalimu, je, haukujali kuwa twaangamia?" Walisumbuka kwa sababu Yesu alikuwa amelala na wala hakuonyesha wasiwasi kama wao, na walimshitaki Yeye kwa kutojali.

Tunao Uhuru wa Kuamua

Shetani anapoleta mateso dhidi yetu katika kutuibia Neno la Mungu, tunao uhuru. Tunaweza kumshukuru Bwana kwa kutuonya ili tusipuuze mbinu za Shetani na tumukemee. Tunaweza kuwa na usumbuvu, kupoteza furaha yetu na hapo kumruhusu Shetani kutuibia ufunuo wa Neno la Mungu ambalo limepandwa mioyoni mwetu.

Je, ni mara ngapi mateso na masaliti yanapokuja, sisi huanza kulia na kumlaumu Mungu?

- "Mwalimu, je, hujali kuwa tunangamia?"
- "Mungu, je, hujali kuwa watoto wangu wanapotea?"
- "Mungu, je, hujali kuwa magonjwa yamenijia maishani?"
- "Mungu, je, hujali kuwa siwezi kulipa mahitaji yangu?"

Tunapokuwa na huzuni na kumlaumu Mungu kwa dhoruba maishani mwetu, tunamruhusu Shetani kutuibia mbegu yenye dhamana ya Neno la Mungu.

Kunena Katika Imani

Imani yenye matunda inahitajika iwapo tutaweka mbegu ya Neno ndani ya mioyo yetu na kutazamia mazao makuu ya thelathini, sitini au hata mia ya kile kimepandwa.

Marko 4:40 Akawaambia, Mbona mmekuwa waoga? Hamna imani bado? Wakaingiwa na hofu kuu, wakaambiana, Ni nani huyu, basi hata upepo na bahari humtii!"

Kunena Katika Mamlaka

Badala ya kuhuzunika dhoruba inapokuja maishani dhidi ya mashua yetu, lazima tusimame kinyume cha Shetani na kwa nunena kwa ujasiri Neno la Mungu kwa imani.

Marko 4:39 Akaamka, akaukemea upepo, akaiambia bahari, Nyamaza, utulie, Upepo ukakoma, kukawa shwari kuu.

Uwe Macho

Hata kama Shetani ni adui aliyeshindwa, atafanya kila kitu kutuzuia kutembea katika mamlaka ya Mungu. Lazima tuwe macho, imara na tayari kushinda kila pigo maishani mwetu.

1 Petro 5:8 Mwe na kiasi na kukesha; kwa kuwa mshitaki wenu Ibilisi, kama samba angurumaye, huzunguka-zunguka, akitafuta mtu ammeze.

Silaha ya Mungu

Kwa imani, tuvae silaha ya Mungu ili tushinde mbinu za Shetani.

Waefeso 6:10,11 Hatimaye, mzidi kuwa hodari katika Bwana na katika uweza wa nguvu zake. Vaeni silaha zote za Mungu, mpate kuweza kuzipinga hila za Shetani.

Tunapofanya hivyo, tutajikuta tumesimama kumpinga Shetani wakati wa dhoruba.

Waefeso 6:13 Kwa sababu hiyo twaeni silaha zote za Mungu, mpate kuweza kushindana siku ya uovu, na mkiisha kuyatimiza yote, kusimama..

Mamlaka Yetu

Kazi ya Yesu imekamilika! Tayari amemshinda Shetani na pepo zake.

Duniani, amewaumba waume kwa wake kuenda katika mamlaka. Amerejesha mamlaka yetu, na sasa, ni lazima tuinuke na kuonyesha kuwa Shetani ni adui aliyeshindwa. Ni lazima kwa bidii tuendeleze ufalme wa Mungu hapa duniani.

MASWALI YA KUJIFUNZA

1. Kulingana na Yohana 10:10, Shetani huja kuyapiga maisha yetu akitumia malengo matatu ya msingi. Yataje malengo haya.
2. Kulingana na mfano wa mpanzi je, kipa umbele kwa Shetani kama mwizi ni kipi?
3. Kwa nini ni muhimu kutenda katika mamlaka na wala sio kukasirika tunapokutana na mateso?

Somo La Tisa

Kanisa na Mamlaka

JE, KANISA NI NINI?

Kutajwa Mara ya Kwanza

Katika agano la Kale, ibada iliwekwa karibu na hekalu au sinagogi. Hapakuwa kanisa kama vile tunaelewa sasa.

Yesu alipotaja kanisa mara ya kwanza, alidhihirisha pia vitu vitatu ambavyo vilionyesha kazi Yake juu ya majukumu mengine yote. Litajengwa na Yesu. Litakuwa jeshi lenye ushindi ambalo litashinda malango ya kuzimu. Litakuwa na nguvu za kufunga na kufungua.

Mathayo 16:13-18 Basi Yesu akaenda pande za Kaisaria-Filipi, akawauliza wanafunzi wake akasema, "Watu hunena Mwana wa Adamu kuwa ni nani?"

Wakasema, "Wengine husema u Yohana Mbatizaji, wengine Eliya, wengine Yeremia au mmojawapo wa manabii."

Akawambia, "Nanyi mwaninena mimi kuwa ni nani?"

Simoni Petro akajibu, wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai.

Yesu akajibu, akamwambia, "heri wewe Simoni Bar-yona; kwa kuwa mwili na damu havikukufunulia hili, bali Baba yangu aliye mbinguni."

Nami nakuambia, wewe ndiwe Petro, na juu ya mwamba huu nitalijenga kanisa langu; wala milango ya kuzimu haitalishinda."

Kweli za Kimsingi

Petro alijua kupitia ufunuo wa Mungu kuwa Yesu alikuwa Kristo, Mwana wa Mungu. Hii ilikuwa ukweli ambako kanisa lingejengwa.

Lilijengwa na Yesu

Sifa ya kwanza ya kanisa ni kuwa Yesu atalijenga. Halitajengwa na wanadamu, na mipango au tamaduni zao.

Linashinda Malango ya Jehanamu

Sifa ya pili ni kuwa malango ya kuzimu haitalishinda.

Katika Biblia yenye ufafanuzi tunasoma,

Nitajenga kanisa langu, na malango ya kuzimu (nguvu za sehemu ya moto) hayatalishinda – au iwe na nguvu kulivunja, au kulipita.

Funguo za Kufunga na Kufungua

Kanisa lina nguvu ya kufunga na kufungua.

Mathayo 16:19 Nami nitakupa wewe funguo za ufalme wa mbinguni, na lo lote utakalolifunga duniani, litakuwa limefungwa mbinguni; na lo lote utakalolifungua duniani, litakuwa limefunguliwa mbinguni.

Kuna vitu vitatu ambavyo tunahitaji kujifunza kuhusu kanisa kwa mara hii ya kwanza Yesu alipolitaja.

- ➢ Kanisa litajengwa na Yesu katika ufunuo kutoka kwa Baba kuwa Yesu ni Kristo, Mwana wa Mungu aishiye.
- ➢ Malango ya kuzimu hayatalishinda kanisa.
- ➢ Kanisa litapewa funguo za ufalme wa mbinguni na kuwa na nguvu ya kufunga na kufungua.

FUNGUO KUREJESHWA

Tumegundua kuwa funguo ni mfano wa mamlaka hapa duniani. Funguo zinaweza kufunga au kufungua milango ambayo tumeona kama mtu, jamii, shirika, mji, taifa na nchi.

Funguo za Kutawala

Hizi zilikuwa funguo za mamlaka ambazo Mungu alimpa mwandamu alipowaumba mume na mke kwa mfano wake.

Mwanzo 1:26 Mungu akasema, Na tumfanye mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu; wakatawale samaki wa baharini, na ndege wa angani, na wanyama, na nchi yote pia, na kila chenye kutambaa kitambaacho juu ya nchi."

Kuibwa na Shetani

Funguo hizi zilikusudiwa na Mungu kutumika kwa mema hapa duniani. Lakini, Adamu na Hawa walipotenda dhambi, walimpa Shetani funguo ambaye alikuja kuiba, kuua na kuharibu.

Funguo za mamlaka, chini ya usimamizi wa Shetani zilifanyika funguo za mauti na jehanamu.

Ufunuo Wa Yohana 1:18 Na aliye hai, nami nalikuwa nimekufa, na tazama, ni hai hata milele na milele. Nami ninazo funguo za mauti, na za kuzimu.

Kutwaliwa na Yesu Tena

Hizi zilikuwa funguo za mamlaka ambazo Yesu alinyakua kutoka kwa Shetani baada ya kuzichukua dhambi zetu chini ya kuzimu. Yesu alikuja kwa vishindo malangoni jehanamu, alizitwaa funguo hizi za mamlaka kutoka kwa

Shetani. Shetani hana tena mamlaka kisheria hapa duniani.

Kurejeshwa kwa Mwanadamu

Funguo hizi zilikuwa mamlaka ambayo Yesu alimurejeshea mwanadamu kama kiumbe kipya baada ya ufufuo na kupaa Kwake kwa Baba. Kwa maana funguo hizi zilirejeshwa kwa wenyewe hapa duniani, hazikuwa tena zitumiwe kama funguo za mauti na kuzimu. Badala yake zikajulikana kama funguo za ufalme wa mbinguni.

Funguo za Ufalme

Mathayo 16:19 Nami nitakupa wewe funguo za ufalme wa mbinguni, na lo lote utakalolifunga duniani, litakuwa limefungwa mbinguni; na lo lote utakalolifungua duniani, litakuwa limefunguliwa mbinguni.

Kwa funguo hizi tunaweza kujenga mapenzi ya Mungu na ufalme wake hapa duniani.

Huu ni ushindi ambao Yesu aliwafunza wanafunzi Wake kuomba.

Mathayo 6:9,10 Basi ninyi salini hivi; Baba yetu uliye mbinguni, Jina lako litukuzwe, Ufalme wako uje, Mapenzi yako yatimizwe, hapa duniani kama huko mbinguni.

Tunapotumia, sisi mwili wa Kristo, funguo tulizopewa na Mungu za mamlaka katika mapenzi Yake, tunaimarisha ufalme wa Mungu duniani.

MALANGO YA KUZIMU

Kanisa la Kushambulia

Yesu alipotaja neno, kanisa mara ya kwanza, alitaja mara tu kuwa malango ya kuzimu haitalishinda.

Mathayo 16:18b ... Kanisa langu; wala milango ya kuzimu haitalishinda.

Ni muhimu kuelewa kuwa Yesu alimaanisha malango ya kuzimu hayatalipinga kanisa.

Katika nyakati zetu, tunaona malango kama mwanya kwenye ua. Kwa picha hiyo, ni vigumu kupata ufahamu wa kweli katika msitari huu. Wengi wetu hatujawai pingwa na lango

.Je, Malango ni Nini?

Katika nyakati za kibiblia, serikali na biashara ya mji ilifanyika mbele ya malango. Kwa hivyo malango mbali na kuweka usalama kwa mji uliozungukwa na ukuta, pia iliashiria mji na serikali ya nchi hiyo. Mfalme Suleimani alitaja juu ya hii katika mojawapo ya mithali yake.

Mithali 31:23 Mme wake hujulikana malangoni; Aketipo pamoja na wazee wa nchi.

Kunyakua Malango

Mungu alipombariki Ibrahimu, alitaja kupokea malango ya adui zake. Hiyo ilikuwa baraka.

Mwanzo 22:17 katika kubariki nitakubariki, na katika kuzidisha nitauzidisha uzao wako kama nyota za mbinguni, na kama mchanga ulioko pwani; na uzao wako utamiliki mlango wa adui zao.

Baraka zilizowekwa juu ya Rebeka pia zilitaja juu ya kupokea malango ya maadui.

Mwanzo 24:60 Wakambaraikia Rebeka, wakamwambia, "Ndugu yetu, uwe wewe mama wa kumi elfu, mara elfu nyingi, na wazao wako waurithi mlango wa hao wawachukiao."

Ili kurithi malango ya adui ina maana kuchukua usukani na kuongoza serikali yake. Sasa tunatakiwa kunyakua malango ya adui zetu katika roho. Kwa mamlaka, utawala na shambulio na vita vikali vya kiroho malango hunyakuliwa.

Mfalme Suleimani alinena juu ya haya.

Mithali 14:19 Wabaya huinama mbele ya wema, Na wasio haki malangoni mwao wenye haki.

Wengi wamejiona wakipigwa na ibilisi wanapojificha ndani ya malango kwa uoga. Lakini, ni kanisa wala si Shetani lenye kusimama na kushambulia.

Sisi, kanisa, inatupasa kuingia malango ya kuzimu na kwa fujo kuendeleza ufalme wa Mungu duniani kote.

FUNGUO ZA UFALME

Yesu alipotaja kanisa mara ya kwanza, alisema, "nitawapa ninyi funguo." Hiyo ingetendeka siku za usoni. Baadaye, baadaya kifo Chake na ufufuo, alimwambia Baba, "ninazo funguo!"

Funguo huwakilisha mamlaka yaliyorejeshwa. Ni funguo ndizo Yesu alinyakua kutoka kwa Shetani alipomnyang'anya utawala na mamlaka.

Je, ufalme wa mbinguni ni gani, ambao tunazo funguo zake?

Yesu, mfalme wa wafalme, anatawala na Baba juu ya dunia nzima. Ni hapa duniani ndipo ufalme Wake unatakiwa kujengwa.

Ufalme wa Mungu ni lazima uenezwe kote duniani wakati waume kwa wake wanatumia funguo zao walizorejeshewa za mamlaka ya kiroho.

Hizi ndizo funguo Yesu alisema tutatumia kufunga na kufungua. Tunayo mamlaka ya kumfunga Shetani na pepo zake na tunazo funguo za mamlaka ya kuwafungulia wafungwa! Tunaposhinda vita katika roho itaonekana wazi, au katika mwili.

KANUNI YA KUFUNGA NA KUFUNGUA

Yesu alisema atatupatia funguo za ufalme wa mbinguni na chochote tunafunga duniani hufungwa mbinguni na chochote tunafungulia hapa duniani kinafunguliwa mbinguni.

Je, maana yake ni nini?

Yesu Amfunga Mtu Mwenye Nguvu

Yesu alinena juu ya kumfunga mtu mwenye nguvu.

Mathayo 12:28, 29 Lakini mimi nikitoa pepo kwa Roho wa Mungu, basi ufalme wa Mungu umekwisha kuwajilia. Ama awezaje mtu kuingia ndani ya nyumba ya mtu mwenye nguvu? Ndipo atakapoiteka nyumba yake.

Mtu Mwenye Nguvu ni Nani?

Mtu mwenye nguvu ni Shetani au kiongozi wa mapepo ambayo ametenga kwa serikali, shirika, au maisha ya mtu.

Yesu aliingia nyumbani mwa mwenye nguvu na kumufunga yeye Shetani na mapepo zake zitawalazo.

Tunamfunga Shetani na mapepo yake yote yanayotawala kwa kusema kwa mamlaka,

➢ "Shetani, nakufunga wewe katika jina la Yesu!"

Kisha tunatakiwa kumfunga mtu mwenye nguvu, kwa kusema kwa ujasiri kwa yule mtawala wa pepo,

➢ "Wewe pepo mbaya, nakufunga katika jina la Yesu!"

Je, Kufunga ni Nini?

Kufunga maana yake ni kumzusha Shetani au mtawala wa pepo juu ya hali fulani ambapo Mungu ametuongoza katika vita vya kiroho.

Kwa mfano, tunapomfunga mbwa kwa nyororo iliyofungwa kwa kikingi, basi mbwa ataenda tu hadi mahali fulani. Amezuiliwa kuenda zaidi ya nyororo na sehemu aliyofungiwa. Tumemzuia katika sehemu yake ya kufika. Basi hii ndiyo maana ya neno funga.

Kuiharibu Nyumba Yake

Kisha, tunatakiwa kuharibu nyumba yake. Tunafanya hivyo kwa kuwaamuru mapepo chini ya mtu mwenye mamlaka ku,

➢ "Ondoka katika jina la Yesu!"

Tunaweza kuwatambua mapepo haya kwa kuenda katika karama ya roho na kipawa cha roho na neno la ufahamu. Pia tunaweza kuwatambua kwa kazi zao za wazi. Kama vile:

➢ Roho za kidini,

➢ Roho za vizuizi,

➢ Roho chafu – za tamaa na potovu

➢ Roho za udhaifu,

➢ Roho za kutesa,

➢ Roho za kujitia kitanzi

Kemea Roho Hizo!

Kwa kukemea roho hizi tunaiharibu nyumba ya mwenye nguvu. Nyumba yake inapoharibiwa, hana tena msaada na tunaweza kumuamuru kuondoka katika jina la Yesu.

Luka 11:21, 22 Mtu mwenye nguvu aliyejifunga silaha zake, alindapo nyumba yake, vitu vyake vi salama; lakini mtu mwenye nguvu kuliko yeye atakapomwendea na kumshinda, amnyang'anya silaha zake zote alozokuwa akizitegemea na kuyagawanya mateka yake.

Yesu tayari amenyang'anya nguvu na mamlaka na kuwatia aibu. Amepaa juuyao wote na kuketi mkono wa kuume wa Mungu Baba. Huu ni ukweli uliotimika mbinguni.

Mamlaka ya Mwamini

Kama waamini, ni lazima tuonyeshe mamlaka yetu na utawala duniani. Ni lazima sasa tutimize hapa duniani kile ambacho tayari kimetimizwa ulimwenguni kote – ambacho kimetimizwa kweli mbinguni. Duniani, ni lazima tumfunge Shetani pamoja na pepo zake na kuwaweka wafungwa huru. Lazima tukomeshe ushawizi wake.

Mathayo 16:19b Na lo lote utakalilolifungua duniani, litakuwa limefunguliwa mbinguni

Tunapofanya hivyo, sisi pia, tunaziharibu nguvu na mamlaka na kumtia aibu, kuzikanyaga kwa msalaba.

MSIMAMO WA SHETANI

Ameumbwa Bila Ushawishi

Yesu kwa kifo Chake na ufufuo, viliharibu ushawishi wa Shetani.

Waebrania 2:14 Basi kwa kuwa watoto wameshiriki damu na mwili, yeye naye vivyo hivyo alishiriki yayo hayo, ili kwa njia ya mauti amharibu yeye aliyekuwa na nguvu za mauti, yaani, Ibilisi

Yeye Hatufanyi Watumwa Tena

Tumewekwa huru na hofu ya kifo na kufungwa.

Waebrania 2:15 ... awaache huru wale ambao kwamba maisha yao yote kwa hofu ya mauti walikuwa katika hali ya utumwa.

Kupitia kazi iliyokamilika ya Yesu katika kifo chake na ufufuo, waume na wake kamwe wasiwe watumwa katika hofu ya kifo. Tunapogundua ukweli huu, tunawekwa huru kabisa kutokana na kufungwa na pia hofu ya ibilisi.

Kazi Zinaharibiwa

Kwa nini Mwana wa Mungu alikuja?

- ➢ Kuziharibu kazi za Shetani!
- ➢ Kuwatia aibu hadharani!

1 Yohana 3:8 Atendaye dhambi ni wa Ibilisi; kwa kuwa Ibilisi hutenda dhambi tangu mwanzo. Kwa kusudi hili Mwana wa Mungu alidhihirishwa, ili azivunje kazi za Ibilisi.

Wakolosai 2:15 Akiisha kuzivua enzi na mamlaka, na kuzifanya kuwa mkogo kwa ujasiri, akizishangilia katika msalaba huo.

MAKANISA YANAYOLALA YANAAMUKA!

Yesu alipokuja hapa duniani kuharibu kazi za ibilisi, aliweka kando mamlaka Yake kama Mungu. Duniani kama Adamu wa Mwisho, alitembea na kuhudumu katika mamlaka na utawala.

Yesu alimshinda Shetani kabisa. Aliwekwa patupu na kuachwa bila ushawishi. Yesu aliweka “sufuri” kubwa kwa ibilisi.

Sasa mamlaka haya na utawala ni funguo ambazo zimerejeshwa kwa mwanadamu aliyekombolewa ambaye, kwa imani, sasa ni kanisa Lake na mwili Wake duniani.

Kama adui aliyeshindwa, kitu cha pekee anachoweza kufanya hapa duniani ni kile sisi katika upuzi tumemruhusu afanye. Kwa ufunuo huu kutoka kwa Neno la Mungu, tunaweza kuinuka na kumfunga Shetani na mapepo yake yanayotawala. Tunaweza kuzizusha ngome

za Shetani tunapomfunga mtu wa nguvu na kuiharibu nyumba yake, huku tukiamuru pepo kuondoka katika jina la Yesu.

2 Wakorintho 10:4 Maana silaha za vita vyetu si za mwili, bali zina uwezo katika Mungu hata kuangusha ngome.

Kanisa ambalo Yesu alisema Atajenga limekuwa jitu linalolala. Sasa, linaamuka ili kutenda katika mamlaka ya Mungu na litaharibu ngome za Shetani!

MASWALI YA KUJIFUNZA

1. Je, Yesu alimaanisha nini aliposema kuwa “malango ya kuzimu haitalishinda” kanisa?

2. Yesu alisema kuwa tunatakiwa kufunga na kufungua. Eleza jinsi umepanga kutekeleza maagizo haya muhimu kutoka kwa Yesu.

3. Kwa kuwa alimfunga mtu mwenye nguvu juu ya mojawapo ya ngome za Shetani, Yesu alisema kuwa lazima mtu aharibu vitu vyake. Je, nani anatajwa kuwa ndiye mtu wa nguvu? Je, mbinu ya kuharibu vitu vyake ni ipi?

Somo La Kumi

Funguo za Ufalme

YESU ANAZO FUNGUO

Je, unayakumbuka maneno ya ushindi aliyotamka Yesu aliporejea tena mbinguni?

Ufunuo Wa Yohana 1:18 Na aliye hai hata milele na milele. Nami ninazo funguo za mauti, na za kuzimu.

Yesu alizichukua funguo za kuzimu na mauti kutoka kwa Shetani. Yesu alipozichukua dhambi zetu kuzimuni, haikuwezekana tena Yeye kuwekwa mtumwa.

Matendo Ya Mitume 2:24 ... ambaye Mungu alimfufua, akiufungua uchungu wa mauti, kwa sababu haikuwezekana ashikwe nao.

Yesu alishinda kifo!

Yesu alirejesha mamlaka, utawala na ufalme kwa mwanadamu. Alirejesha kwetu vyote alivyoiba Shetani.

Tunajua kuwa Mungu anataka sisi tuishi katika mamlaka kamili na tawala juu ya Shetani kwa sababu Yeye alimsulubisha Mwana Wake ili kurejesha vyote alivyoumba kwetu tuwe na kutenda hapa duniani.

Kile Yesu alifanya hapa duniani, uhai Wake, maisha Yake, kifo Chake, na kufufuka kwake ilikuwa ili turejeshwe tena. Alifanya hivyo ili tuende katika mamlaka na ushindi juu ya Shetani, pepo zake, na vyote hapa duniani.

DAMU YA YESU – UFUNGUO WA USHINDI

Mungu aliumba Adamu, alimvuvia uhai Wake Mwenyewe. Uhai huu haukuwekwa tu kwa sehemu moja mwilini mwa Adamu. Mungu aliweka uhai ndani ya damu ya Adamu. Ulipitishwa kila sehemu ya mwili wa Adamu wakati wote.

Musa aliandika kuwa uhai wa kiumbe uko ndani ya damu.

Mambo Ya Walawi 17:11a Kwa kuwa uhai wa mwili u katika damu...

Dhambi ya Adamu - Mauti

Katika dhambi, Adamu alipoteza uhai wa Mungu uliokuwa ndani ya damu yake. Uhai huu unaweza tu kurejeshwa kwa mwanadamu kupitia mpango wa Mungu

wa ukombozi. Ili mwanadamu arejeshwe tena kwa mfano wa Mungu, lazima awe na uhai wa Mungu ndani ya damu yake.

Katika mpango wa Mungu wa ukombozi, Mwana Wake Yesu ataimwaga damu Yake.

Waebrania 9:22 Na katika Torati karibu vitu vyote husafisha kwa damu, na pasipo kumwaga damu hakuna ondoleo.

Adhabu ya dhambi, ambayo ilikuwa kifo, ililipwa kwa niaba na yule aliyekuwa hajapoteza uhai wa Mungu ndani ya damu yake kupitia dhambi.

Kwa kupajikwa na Roho Mtakatifu na kuzaliwa na bikira, Yesu alirithi damu ya Adamu. Alifanyika dhabihu iliyokamilika aliyejitolea kwa dhati na kutoa maisha Yake kwa kumwaga damu Yake mwenyewe.

Kupitia Damu ya Yesu Tunapata

➢ ***Msamaha wa Dhambi***

Kukombolewa kwetu ku ndani ya damu ya Yesu.

Waefeso 1:7 katika yeye huyo, kwa damu yake, tunao ukombozi wetu, masamaha ya dhambi, sawasawa na wingi wa neema yake...

1 Petro 1:18,19 ... nanyi mfahamu kwamba mlikombolew si kwa vitu viharibivyo, kwa fesha au dhahabu; mpate kutoka katika mwenendo wenu usiofaa mlioupokea kwa baba zenu; bali kwa damu ya thamani, kama ya mwana kondoo asiye na ila, asiye na waa, yaani, ya Kristo.

➢ ***Haki***

➢ ***Wokovu***

Tumedhibitishwa na kupata haki ya Mungu juu ya maisha yetu iliyorejeshwa kwa damu ya Yesu.

Warumi 5:8,9 Bali Mungu aonyesha pendo lake yeye mwenyewe kwetu sis, kwa kuwa Kristo alikufa kwa ajili yetu, tulipokuwa tungali wenye dhambi. Basi zaidi sana tukiisha kuhesabiwa haki katika damu yake, tutaokolewa na ghadhabu kwa yeye.

Hukumu ya Mungu iliyokamilika ilitoshelezwa na tuliokolewa kutokana na ghadhabu ya Mungu wakati Yesu kwa niaba yetu aliibeba adhabu ya kifo kwa kumwaga damu Yake msalabani.

Ni kwa kuhusika katika damu ya Yesu iliyomwagika iliyo na uhai wa Mungu, ndipo tunaweza kupata uhai Wake ndani yetu.

Yohana 6:53 Basi Yesu akawaambia, "Amin, amin, nawaambieni, Msipoula mwili wake mwana wa Adamu na kuinywa damu yake, hamna uzima ndani yenu."

➢ ***Ushirika***

Damu ya Yesu itaondoa hali zote za dhambi juu ya maisha yetu ili kwa mara nyingine uhai wa Mungu urejeshwe.

1 Yohana 1:7 Bali tukienenda nuruni, kama yeye alivyo katika nuru, twashirikiana sisi kwa sisi, na damu yake Yesu, Mwana wake, yatusafisha dhambi yote.

➢ ***Kukombolewa***

Kukombolewa kwetu na msamaha kamili ni kwa damu Yake.

Wakolosai 1:13,14 Naye alituokoa katika nguvu za giza, akatuhamisha na kutuingiza katika ufalme wa Mwana wa pendo lake; ambaye katika yeye tuna ukombozi, yaani msamaha wa dhambi

Pasipo kupokea dhabihu ya ukombozi na zawadi ya Mungu ya wokovu katika damu ya Yesu iliyomwagika, hakuna vile mwanadamu atasamehewa na kurejeshwa.

Waebrania 9:22 Na katika Torati karibu vitu vyote husafishwa kwa damu, na pasipo kumwaga damu hakuna ondoleo.

Waebrania 9:12 Wala si kwa damu ya mbuzi na ndama, bali kwa damu yake mwenyewe aliingia mara moja tu katika patakatifu, akiisha kupata ukombozi wa milele.

➢ ***Hawana Dosari***

➢ ***Tunaweza Kutumika***

Kwa damu ya Yesu tumeoshwa ili tumtumikie Mungu.

Waebrania 9:14 Basi si zaidi damu yake Kristo, ambaye kwamba kwa Roho wa milele alijitoa nafsi yake kwa Mungu kuwa sadaka isiyo na mawaa, itawasafisha dhamiri zenu na matendo mafu, mpate kumwabudu Mungu aliye hai?

➢ ***Tuwe na Ujasiri***

Adamu alipotembea katika ushirika kila siku katika uwepo wa Mungu kabla hajatenda dhambi, hata kwa damu ya Yesu, sasa mwanadamu, yu huru kutokana na lawama na hukumu, na anaweza tena kutembea katika uwepo wa Mungu.

Waebrania 10:19 basi, ndugu, kwa kuwa tuna ujasisi wa kupaingia patakatifu kwa damu ya Yesu...

➢ ***Kuwa na Amani***

Amani na marudiano vinawezekana kwa damu Yake.

Wakolosai 1:19,20 Kwa kuwa katika yeye ilipendeza utimilifu wote ukae, na kwa yeye kuvipatanisha vitu vyote na nafsi yake akiisha kufanya amani kwa damu ya msalaba wake, kwa yeye ikiwa ni vitu vilivyo juu ya nchi, au vilivyo mbinguni.

➢ ***Kurejeshwa katika Hali ya Awali***

Ilikuwa damu ya Yesu iliyomshinda Shetani ilivyokomboa na kumrejesha mwanadamu katika uhai wa Mungu kupitia kuzaliwa upya.

Shetani alikuja kuiba, kuua na kuharibu mwanadamu ambaye Mungu aliumba kwa mfano na sura ya kweli hapa duniani. Kupitia dhambi, mwanadamu alipoteza uhai wa Mungu. Mwanadamu alikuwa hajiwezi katika mapigo ya Shetani maishani mwake. Kwa mpango wa Mungu wa ukombozi katika kumwagika kwa damu ya Mwana Wake, mwanadamu angerejeshwa kamili kwa hali yake ya awali na uhusiano na Mungu. Kwa damu ya Yesu, mwanadamu, aliyekuwa kashindwa, sasa angefanyika mshindi tena.

➢ ***Kufunikwa Katika Ulinzi***

Kama vile kuhani katika Agano la Kale alipochukua damu ya mwanakondoo wa dhabihu na kuimwaga kwenye kiti cha rehema cha Mungu ili kufunika au kuosha dhambi za watu, vile vile leo, kwa imani, damu ya Mwanakondoo huwafunika na kuwazingira wanadamu waliokombolewa.

➢ ***Ushindi***

Katika damu ya Yesu, tunapata ushindi!

Tunapotembea katika msamaha, katika kumtii Mungu na kwa imani, tunaweza kusema kwa ujasiri:

- ➢ "Shetani, mimi nimefunikwa na damu ya Yesu!"
- ➢ "Jamii yangu na mali yangu imefunikwa na damu ya Yesu!"
- ➢ "Shetani, umeshindwa na damu ya Yesu!"
- ➢ "Kwa sababu ya damu ya Yesu, hutanigusa!"

Hata Yesu alipomshinda Shetani kwa damu Yake, nasi pia tunaweza kuwa washindi kwa damu ya Yesu! Kwa kinga ya damu Yake, hakuna silaha dhidi yetu itafaulu.

Ufunuo Wa Yohana 12:11a Nao wakamshinda kwa damu ya Mwana-kondoo, na kwa neno la ushuhuda wao; ambao hawakupenda maisha yao hata kufa.

Shetani alishindwa na damu ya Yesu.

Ufunguo wa mamlaka ya damu ya Yesu umepewa kila mmoja wetu ambao kwa damu hiyo wamekombolewa. Kwa nguvu ipatikanayo katika ufunguo wa damu Yake sisi tu washindi na Shetani ataendelea kushindwa maishani mwetu.

NENO LA MUNGU – UFUNGUO WENYE USHINDI

Upanga wa Roho

Katika Waefeso, silaha yetu ya ushindi katika vita imeelezwa kama "upanga wa Roho, ambayo ni Neno la Mungu" (6:17). Neno la Mungu linapotoka vinywani mwetu huwa silaha kuu dhidi ya Shetani na ambapo hana kinga. Tunaponena Neno la Mungu kwa mamlaka, tutamshinda Shetani maishani mwetu.

Ufunuo Wa Yohana 12:11a Nao wakamshinda kwa damu ya Mwana-kondoo, na kwa neno la ushuhuda wao.

Neno Katika Ushuhuda

"Neno la ushuhuda wao" inaweza kutafsiri kwa makini kama "Neno katika ushuhuda wao." Ushuhuda wetu ni kile tunanena. Tunapoacha kunena shida, mawazo yetu, hofu yetu, na kuanza kunena kwa ujasiri kile Neno la Mungu linasema kuhusu hali yetu kisha nasi pia tutakuwa washindi.

Neno Huleta Ushindi

Ili kuwa na Neno la Mungu likitoka vinywani mwetu kila wakati, inatupasa kusoma, kujifunza na kulitafakari Neno. Kisha litakuwa mizizi iliyokomaa katika imani maishani mwetu.

1 Yohana 2:13,14 Nawaandikia ninyi, akina baba, kwa sababu mmemjua yeye aliye tangu mwanzo. Nawaandikia ninyi, vijana, kwa sababu mmemshinda yule mwovu. Nimewaandikia ninyi, watoto, kwa sababu mmemjua Baba.

Nimewaandikia ninyi, akina baba, kwa sababu mmemjua yeye aliye tangu mwanzo. Nimewaandikia ninyi, vijana, kwa sababu mna nguvu, na neno la Mungu linakaa ndani yenu, nanyi mmemshinda yule mwovu

Vijana hawa walijulikana kuwa wenye nguvu katika kushinda kwa sababu walikuwa na Neno la Mungu ndani yao. Waliponena kwa ujasiri Neno hilo vinywani mwao kwa mamlaka na utawala wa Mungu waliwashinda waovu.

Waefeso 6:17 Tena ipokeeni chapeo ya wokovu, na upanga wa Roho ambao ni neno la Mungu.

Upanga wa Roho ni Neno la Mungu.

Ufunuo Wa Yohana 19:13-16 Naye amefvikwa vasi lililochovywa katika dame, na jina lake aitwa, Neno la Mungu. Na majeshi yaliyo mbinguni watkamfuata, wamepanda farasi weupe na kuvikwa kitani nzuri, nyeupe, safi. Na upanga mkali hutoka kinywani mwake ili awapige mataifa kwa huo. Naye atawachunga kwa fimbo ya chuma, naye anakanyaga shinikizo la mvinyo ya ghadhabu ya hasira ya Mungu Mwenyezi. Naye ana jina limeandikwa katika vasi lake na paja lake;

WAFALME, NA BWANA WA MABWANA

Nena Neno

Yesu alisema mfano bora wa imani ni mtu aliyeelewa mamlaka na kufahamu jinsi ya kulinena Neno.

Mathayo 8:8-10 Yule akida akamjibu, akasema, "Bwana, mimi sistahili wewe uingie chini ya dari yangu, lakini sema neno tu, na mtumishi wangu atapona. Kwa maana mimi nami ni mtu niliyewekwa chini ya mamlaka, mwenye askari chini yangu; nikimwambia huyu, nenda, huenda; na huyu, njoo, huja; na mtumwa wangu, Fanya hivi, hufanya"

Yesu aliposikia hayo, alistaajabu, akawaambia wale waliomfuata, "Amin, nawaambieni, Sijaona imani kubwa namna hii, kwa ye yote katika Israeli!"

Kulithibitisha Neno

Neno la Mungu litathibitishwa kwa ishara na maajabu.

Marko 16:19-20 Basi Bwana Yesu, baada ya kusema nao, akachukuliwa juu mbinguni, akaketi mkono wa kuume wa Mungu.

Nao wale wakatoka, wakahubiri kotekote, Bwana akitenda kazi pamoja nao, na kulithibitisha lile neno kwa ishara zilizofuatana nalo. Amina.

Yesu Ni Neno

Jina la Yesu hasa ni Neno la Mungu.

Ufunuo Wa Yohana 19:13 Naye amevikwa vasi lililochovywa katika damu, na majeshi yaliyo mbinguni wakamfuata, wamepanda farasi weupe na kuvikwa kitani nzuri, nyeupe, safi.

Yohana 1:1 hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu.

Neno Halitarejea Tupu

Mungu alinena kwa nguvu Neno Lake katika Isaya.

Isaya 55:11 Ndivyo litakavyokuwa neno langu, litokalo katika kinywa changu; halitanirudia bure, bali litatimiza mapenzi yangu, nalo litafanikiwa katika mambo yale niliyolituma.

Mungu alinena juu ya nguvu iponyayo katika Neno kupitia Daudi.

Zaburi 107:20 Hulituma neno lake, huwaponya, Huwatoa katika maangamizo yao.

Neno tunalonena katika mamlaka linatimiza mambo yampendezayo Mungu. Neno la Mungu linatuahidi kuwa litastawi!

Maneno Hujenga

Maneno yana nguvu ya kujenga.

Waebrania 11:3 Kwa imani twafahamu ya kuwa ulimwengu uliumbwa kwa neno la Mungu, hata vitu vinavyoonekana havikufanywa kwa vitu vinavyo dhahiri.

Maneno yana Mamlaka

Yesu alinena Neno kwa mamlaka.

Luka 4:36 Mshangao ukawashika wote, wakasemezana wakisema, "Ni Neno gain hili, maana awaamuru pepo wachafu kwa uwezo na nguvu, nao hutoka."

Neno Ndani – Neno Nje

Ni vyema kulijua Neno, lakini tusipokutana na hali zetu tukinena Neno la Mungu vinywani mwetu, hatutakuwa na ushindi!

Yesu alinena Neno kwa mamlaka na nguvu.

Imani ya Mungu:

- **Inaamini Neno,**
- **Inanena Neno,**
- **Huona Neno likitimiza miujiza.**

Ufunguo wa Neno la Mungu hautashindwa tunapoendelea kunena katika mamlaka na utawala.

Ili tutende katika utawala hapa duniani ambapo ndivyo tuliumbwa duniani kufanya, Yesu ametupa, kanisa Lake, funguo za mamlaka ya ushindi wa vita za kiroho. Tunapogundua funguo hizi na njia bora ya kuzitumia, tutajikuta tunaishi katika ushindi juu ya vita maishani. Tutajikuta tumekuwa wale Yesu amesema tutakuwa.

Sisi ni zaidi ya washindi,
Sisi ni washindi katika jina Lake

MASWALI YA KUJIFUNZA

1. Eleza kwa nini damu ya Yesu inatimiza katika kushinda mapigo ya ibilisi au mapepo.

2. Toa mfano wa jinsi kunena Neno la Mungu limekupa ushindi katika maisha yako.

3. Je, ni maandiko gani utakayokariri na utakayotumia kama silaha katika vita vya kiroho?

Somo La Kumi na Moja

Jina La Yesu

JINA LA YESU – UFUNGUO WA USHINDI

Tunapotumia jina la Yesu, tunanena katika mamlaka ya Yesu. Tunaponena katika hilo jina, kuna matokeo kama vile Yesu mwenyewe amesimama pale akinena katika hali hiyo. Ametupa haki ya kutumia jina Lake.

Ishara Kufuata Kuamini Katika Jina

Ishara zitafuata wale wanaoamini katika jina la Yesu.

Marko 16:15-18 Akawaambia, Endeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe. Aaminiye na kubatizwa ataokoka, asiyeamini, atahukumiwa.

"Na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio, kwa jina langu watatoa pepo, watasema kwa lugha mpya; watashika nyoka, hata wakinywa kitu cha kufisha, hakitawadhuru kabisa, wataweka mikono yao juu ya wagonjwa, nao watapata afya."

Hapakuwa na mpangilio katika Kigiriki, lugha ambayo Agano Jipya liliandikwa hapo awali. Vituo na mpangilio uliopo katika Biblia zetu iliongezwa na watafsiri kutokana na maoni yao.

Mariko 16:17 inasoma,
Na ishara hizi zitafuatana nao waamini ...

Kifungu hiki kinaweza kutafsiriwa kwa makini kama,
Na ishara hizi zitawafuata wale wanaoamini katika jina langu ...

Yesu alisema, ni muhimu tuamini katika jina Lake. Ni lazima tuelewe mamlaka yetu katika jina la Yesu. Ni lazima kwa ujasiri tuachilie mamlaka hayo kwa imani tunapotumia jina la Yesu.

Tunaponena na kutenda imani yetu katika jina la Yesu, tutakemea mapepo. Tutaweka mikono yetu kwa wagonjwa, na watapata nafuu.

Haki ya Kustaajabisha

Kabla ya kumalizika kwa kazi ya Yesu msalabani, hakuna yeyote angetaja majina ya Mungu. Yalidhaniwa kuwa takatifu kutajwa kwa sauti. Yaliandikwa ndani Mahali Patakatifu Sana, na yalijulikana tu kwa Kuhani Mkuu.

Yesu alipowapa waamini haki ya kulitumia jina Lake, ilikuwa fursa mwafaka, na isije ikapuuzwa.

Kufungua Mamlaka ya Yesu

Kwa sababu Yesu alikuwa Mwana wa Mungu,

➢ Alikuwa na mamlaka yote mbinguni.

Kwa sababu Yesu alikuwa Mwana wa Adamu,

➢ Alikuwa na mamlaka duniani.

Mathayo 28:18 Yesu akaja kwao, akasema nao, akawaambia, "Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani."

Tunapolitumia jina Lake, mamlaka na nguvu yenye kusisimua huachiliwa. Ni kama tumesimama pahali Pake na kutumia mamlaka Yake.

Nguvu Za Kisheria

Yesu alipotupatia haki kisheria kutumia jina Lake, aliweka matumaini Yake yote kwetu. Kisheria, alitupa Uwezo wa Kisheria kulitumia jina Lake.

Katika mahakama Uwezo wa Kisheria ni stakabadhi ya sheria inayompa mtu haki ya kutumia jina la mtu mwingine. Mtu aliyetengwa kwa hilo, anapotia sahihi mapatano kwa niaba ya mtu na kuweka pia nakala ya Uwezo wa Kisheria kwa patano hilo. Inakubalika kisheria kama vile mtu huyo ametia sahihi patano hilo mwenyewe.

Kusikia Kutoka Kwa Mungu

Yesu alipohudumu hapa duniani, alifanya hivyo kwa niaba ya Baba Yake.

Yohana 5:19 "Mwana hawezi kutenda neno mwenyewe ila lile ambalo amwona Baba analitenda, kwa maana yote ayatendayo yeye, ndiyo ayatendayo Mwana vile vile."

Sasa tunapohudumu hapa duniani, inatupasa tutende kwa niaba ya Mwana. Tusilitumie jina la Yesu kujitosheleza wenyewe bila kwanza kuchukua muda kusikia kutoka kwa Mungu.

Kulitumia Jina Kwa Msaha

Kujaribu kulitumia jina la Yesu ili kujitosheleza bila kwanza kutambua mapenzi ya Mungu, itakuwa kutumia jina Lake kwa mzaha.

Kumbukumbu La Torati 5:11 Usilitaje bure Jina la BWANA, Mungu wako, maana BWANA hatamhesabia kuwa hana hatia, mtu alitajaye Jina lake bure.

Jina Juu ya Majina Yote

Jina la Yesu li juu ya majina mengine

Wafilipi 2:5-11 Iweni na nia iyo hiyo ndani yenu ambayo ilikuwamo pia ndani ya Kristo Yesu, ambaye yeye mwanzo alikuwa yuna namna ya Mungu, naye hakuona kule kuwa sawa na Mungu kuwa ni kitu cha kushikamana nacho, bali alilifanya

kuwa hana utukufu, akatwaa namna ya mtumwa, akawa ana mfanowa wanadamu.

Tena alipoonekana ana umbo kama mtii hata mauti, naam, mauti ya msalaba.

Kwa hiyo tena Mungu alimwadhimisha mno, akamkirimia Jina lile lipitalo kila jina, ili kwa jina la Yesu kila goti lipigwe, la vitu vya mbinguni, na vya duniani, na vya chini ya nchi, na kila ulimi ukiri ya kuwa YESU KRISTO NI BWANA kwa utukufu wa Mungu Baba.

- ➢ Kila pepo ana jina.
- ➢ Kila mtu ana jina.
- ➢ Kila ugonjwa na maradhi yana jina.
- ➢ Kila mbinu ya Shetani ina jina.
- ➢ Jina la Yesu linapotajwa nguvu za mapepo hutoroka.
- ➢ Jina la Yesu linapotajwa, saratani na magonjwa mengine yote huinama.
- ➢ Jina la Yesu linapotajwa, mbinu za Shetani hushindwa.

Jina la Yesu li juu ya majina mengine. Kila goti litapigwa kwa unyenyekevu wa Bwana Yesu jina Lake linapotajwa katika imani.

Mapepo Yanatii Jina

Mapepo yanajua jina la Yesu, na watalitii jina hilo.

Luka 10:17, 19 Ndipo wale sabini waliporudi kwa furaha, wakisema, "Bwana, hata pepo watutii kwa jina lako."

"Akawaambia, Nilimwona Shetani, akianguka kutoka mbinguni kama umeme. Tazama, nimewapa amri ya kukanyaga nyoka na nge, na nguvu zote za yule adui, wala hakuna kitu kitakachowadhuru."

Mathayo 28:18 Yesu akaja kwao, akasema nao, akawaambia, "Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani."

Mamlaka yote amepewa Yesu. Kwa jina la Yesu tunayo mamlaka hayo hayo hapa duniani.

Amini Katika Jina Lake

Tunaamuriwa kuamini katika jina la Yesu.

1 Yohana 3:23 Na hii ndiyo amri yake, kwamba tuliamini jina la Mwana wake Yesu Kristo, na kupendana sisi kwa sisi, kama alivyotupa amri.

Tunatakiwa kuamini katika jina la Yesu ili kupata uzima wa milele.

Yohana 3:18 Amwaminiye yeye hahukumiwi; asiyeamini amekwisha kuhukumiwa, kwa sababu hakuliamini jina la Mwana pekee wa Mungu.

Yohana 20:31 Lakini hizi zimeandikwa ili mpate kuamini ya kwamba Yesu ndiye Kristo, Mwana wa Mungu; na kwa kuamini mwe na uzima kwa jina lake.

Tunaweza kuwa na hakikisho kamili la wokovu wetu kwa sababu tunaamini katika jina Lake.

1 Yohana 5:13 Nimewaandika ninyi mabo hayo, ili mjue ya kuwa mna uzima wa milele, ninyi mnaoliamini Jina la Mwana wa Mungu.

Uliza Katika Jina Lake

Tumeagizwa kuuliza katika jina la Yesu.

Yohana 14:12-14 Amin, amin nawaambieni, Yeye aniaminiye mimi, kazi nizifanyazo mimi, yeye naye atafanya, naam, na kubwa kuliko hizo atafanya, kwa kuwa mimi, naenda kwa Baba. Nanyi mkiomba lo lote kwa jina langu, hilo nitalifanya, ili Baba atukuzwe ndani ya Mwana. Mkiniomba neno lo lote kwa jina langu, nitalifanya.

Yesu alipoondoka kwenda kwa Baba, aliwaagiza wafuasi Wake walitumie jina Lake. Aliwaambia kuwa kile wangeuliza, Angefanya, ili Baba atukuzwe katika Mwana.

Yohana 15:16 Si ninyi mlionichagua mimi, bali ni mimi niliyewachagua ninyi, nami nikawaweka mwende mkazae matunda, na matunda yenu yapate kukaa, ili kwamba lo lote mmwombalo Baba kwa jina langu awapeni.

Yohana 16:23,24 Tena siku ile hamtaniuliza neno lo lote, Amin, amin, nawaambia, mkimwomba Baba neno lo lote atawapa kwa jina langu. Hata sasa hamkuomba neno kwa jina langu; ombeni, nanyi mtapata, furaha yenu iwe timilifu

Tumeagizwa kuuliza katika jina la Yesu.

Kutenda Yote Katika Jina Lake

Tunatakiwa kufanya kila kitu katika jina la Yesu. Je, hii ni fursa iliyoje!

Wakolosai 3:17 Na kila mfanyalo, kwa neno au kwa tendo, fanyeni yote katika jina la Bwana Yesu, mkimshukuru Mungu Baba kwa yeye.

Ni lazima pia tutambue kuwa yote tunayofanya ni lazima tufanye katika jina la Yesu. Tukifanya hivyo tunapata msisimko katika maisha yetu.

Mitume na waamini wa awali katika kitabu cha Matendo kwa ujasiri walilitumia jina la Yesu na matokeo yalikuwa miujiza.

Nguvu Katika Jina Lake

Matendo Ya Mitume 3:1-10 Basi Petro na Yohana walikuwa wakikwea pamoja kwenda hekaluni, saa ya kusali, saa tisa.

Na mtu mmoja aliyekuwa kiwete toka tumboni mwa mamaye alichukuliwa na watu, ambaye walimweka kila siku katika mlango wa hekalu uitwao Mzuri, ili aombe sadaka kwa watu waingiao ndani ya hekalu. Mtu huyu akiwaona Petro na Yohaya wakiingia hekaluni aliomba apewe sadaka.

Na Petro, akimkazia macho, pamoja na Yohana, akasema, "Tutazame sisi. Akawaangalia, akitaraji kupata kitu kwao. Lakini Petro akasema, Mimi sina fedha, wala dhahabu, lakini nilicho nacho ndicho nikupacho. Kwa jina la Yesu Kristo wa Nazareti, simama uende."

Akamshika mkono wa kuume, akamwinua, mara nyayo zake na vifundo vya miguu yake vikatiwa nguvu.

Akaondoka upesi akasimama, akaanza kwenda, akaingia ndani ya hekalu pamoja nao, akienda, akiruka-ruka, na kumsifu Mungu. Wakamtambua, ya kuwa yeye ndiye aliyekuwa akiketi na kuomba sadaka penye mlango Mzuri wa hekalu, wakajaa ushangao wakastaajabia mambo yale yaliyompata.

Imani Katika Jina Lake

Petro alieleza kuwa kibali cha kulitumia jina la Yesu, ilikuwa ni kuachilia mamlaka katika jina la Yesu.

Matendo Ya Mitume 3:12 Hata Petro alipoyaona haya akawajibu wale watu, "Enyi Waisraeli, mbona mnatukazia macho sisi, kana kwamba tumemfanya huyu aende kwa nguvu zetu sisi, au kwa utauwa wetu sisi?"

Matendo Ya Mitume 3:16 "Na kwa imani katika jina lake, jina lake limemtia nguvu mtu huyu mnayemwona na kumjua, na imani ile iliyo kwake yeye imempatia huyu uzima huu mkamilifu mbele yenu ninyi nyote."

Uponyaji Katika Jina Lake

Baada ya uponyaji huu, Petro na Yohana walishikwa, wakawekwa jela siku kutwa na kutishwa na viongozi wa kidini wasinene tena katika jina la Yesu. Petro alijibu kwa ujasiri swali lao kuhusu uponyaji huu akisema:

Matendo Ya Mitume 4:10 ... "Jueni ninyi nyote na watu wote wa Israeli ya kuwa kwa jina la Yesu Kristo wa Nazareti, ambaye ninyi mlimsulibisha, na Mungu akamfufua katika

wafu, kwa jina hilo mtu huyu anasimama ali mzima mbele yenu."

Wokovu Katika Jina Lake

Baadaye Petro na Yohana walipolitumia jina la Yesu wakihudumu uponyaji kwa mtu kiwete, idadi ya walioamini iliongezeka na kuwa kama elfu tano.

Matendo Ya Mitume 4:4 Lakini wengi katika hao waliosikia lile neno waliamini, na hesabu ya watu waume ikawa kama elfu tano.

Wokovu wetu upo katika jina nzuri la Yesu.

Matendo Ya Mitume 4:12 Wala hakuna wokovu katika mwingine awaye yote, kwa maana hapana jina jingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo.

Hofu ya Mwanadamu kwa Jina Lake

Petro na Yohana walitishwa na viongozi wa kidini wasinene tena katika jina hilo.

Matendo Ya Mitume 4:17,18 "Lakini neno hili lisije likaenea katika watu, na tuwatishe wasiseme tena na mtu awaye yote kwa jins hili. Wakawaita, wakawaamuru wasiseme kabisa wala kufundisha kwa jina la Yesu.

Ujasiri Katika Jina Lake

Wakati huo roho wa ujasiri alikaa juu ya Petro na Yohana.

Matendo Ya Mitume 4:29,30 Basi sasa, Bwana, yaangalie matisho yao, ukawajalie watumwa wako kunena neno lako kwa ujasiri wote, ukinyosha mkono wako kuponya, ishara na majaabu vifanyike kwa jina la Mtumishi wako mtakatifu Yesu.

Philipo Alihubiri Jina Lake

Matendo Ya Mitume 8:12 Lakini walipomwamini Filipo, akizihubiri habari njema za ufalme wa Mungu, na jina lake Yesu Kristo, wakabatizwa, wanaume na wanawake.

Alishikwa Kwa Ajili ya Jina la Yesu

Paulo alitumwa kuwashika wale walioliita jina la Yesu.

Matendo Ya Mitume 9:14 hata hapa ana amri itokayo kwa wakuu wa makuhani awafunge wote wakuitiao Jina lako.

Kuchaguliwa Kulibeba Jina Lake

Paulo alichaguliwa na Mungu ili kueneza jina la Yesu duniani.

Matendo Ya Mitume 9:15 Lakini Bwana akamwambia, "Nenda tu, kwa maana huyu ni chombo kiteule kwangu, alichukue Jina langu mbele ya Mataifa, na wafalme, na wana wa Israeli."

Kuhubiri Katika Neno Bila Hofu

Matendo Ya Mitume 9:27 lakini Barnaba akamtwaa, akampeleka kwa mitume, akamtwaa, akampeleka kwa mitume, akawaeleza jinsi alivyomwona Bwana njiani, nay a kwamba alisema naye, na jinsi alivyohubiri kwa ushujaa katika Dameski kwa jina la Yesu.

Ukombozi Katika Jina

Matendo Ya Mitume 16:18 Akafanya haya siku nyingi. Lakini Paulo akasikitika, akageuka akamwambia yulepepo, "Nakuamuru kwa jina la Yesu Kristo, mtoke huyu." Akamtoka saa ile ile.".

Heshima Kuu ya Jina Lake

Matendo Ya Mitume 19:17,18 habari hii ikajulikana na Wayahudi wote na Wayunani waliokaa Efeso, hofu ikawaingia wote, na jina la Bwana Yesu likatukuzwa. Na wengi wa wale walioamini wakaja wakaungama, wakidhihirisha matendo yao.

ISHARA NA MAAJABU KATIKA JINA LA YESU

Tunapomsikiliza Mungu na kutii sauti Yake, lazima tutoke kwa ujasiri na kwa imani na kutumia mamlaka ya jina la Yesu. Tunapofanya hivyo, tutaona ishara na maajabu maishani na katika huduma zetu kila siku.

Matendo Ya Mitume 4:29-31 Basi sasa, Bwana, yaangalie matisho yao, ukawajalie watumwa wako kunena neno lako kwa ujasiri wote, ukinyosha mkono wako kuponya, ishara na majaabu vifanyike kwa jina la Mtumishi wako mtakatifu Yesu.

Hata walipokwisha kumwomba Mungu, mahali pale walipokusanyika pakatikiswa, wote wakajaa Roho Mtakatifu, wakanena neno la Mungu kwa ujasiri.

Tunapoendelea kutumia mamlaka na uwezo wa jina la Yesu, nasi pia tutatikisa ulimwengu kwa uwepo na uwezo wa Mungu wa ajabu.

Funguo katika maisha ya Mkristo aliye mshindi inapatikana katika jina kuu la Yesu.

Tunaweza kuenda katika nguvu zile kama zilivyoelezwa katika kitabu cha Matendo, tunapojiunga na kanisa la awali katika kutumia mamlaka katika jina la Yesu.

MASWALI YA KUJIFUNZA

1. Toa mifano miwili kutoka kwa kitabu cha Matendo ambapo mitume walitumia jina la Yesu.

2. Je, nini maana yake tunaposema jina la Yesu ni kama kuwa na Uwezo wa Kisheria?

3. Katika changamoto ambazo unapitia kwa sasa, je, umepanga kupata ushindi kwa kulitumia jina la Yesu?

Somo La Kumi na Mbili

Ushindi wa Vita vya Kiroho

KUTAYARISHWA KWA AJILI YA VITA

Nguvu Za Kimungu

Sasa kwa kuwa tunaelewa utengano wa milele na kutambua mamlaka yetu na silaha zetu zenye nguvu, tunatayarishwa katika nguvu na ushindi wa kivita.

Paulo aliandika,

2 Wakorintho 10:4 Maana silaha za vita vyetu si za mwili, bali zina uwezo katika Mungu hata kuangusha ngome...

Wengi wamejaribu kuingia vitani bila ya ufunuo. Hawakuelewa mamlaka waliyo nayo na kuwa wao ni nani katika Yesu.

Kwao, vita vya kiroho vimekuwa vikali vinavyoendelea dhidi ya adui mwenye nguvu. Wamezungukwa na Shetani na pepo zake. Kadri wanapomtazama Shetani na pepo, kadri anavyoonekana mkubwa, mchoyo, na mwenye nguvu sana.

Adui Aliyeshindwa

Nabii Isaya aliandika kuhusu siku za usoni za Shetani. Alitueleza picha ya mwisho wake.

Isaya 14:15-17 Lakini utashushwa mpaka kuzimu, Mpaka pande za mwisho za shimo. Wao wakuonao watakukazia macho, watakuangalia sana, wakisema, Je! Huyu ndiye aliyeitetemesha dunia, Huyu ndiye aliyetikisha falme, aliyewafungua wafungwa wake waende kwao?'

Watu watamkazia macho huyu aitwaye Shetani ambaye ameshindwa na kuaibishwa. Watamtazama kwa mshangao yule waliyemdhania kuwa alikuwa mkubwa na mwenye nguvu. Watamwona amejaa hofu na aibu. Watauliza, “je, huyu siye mtu …?” Je, huyu siye mtu ambaye kila mtu anamfahamu sana?”

Watamkazia macho yule aliyeambulia patupu. Watamtazama kwa dhihaki. Watamwona ameshindwa kabisa.

Tukiwa na ufunuo juu yetu ndani ya Yesu, basi kamwe Shetani hatatutawala. Kila mara tumezungukwa na Yesu!

Shetani ni adui aliyeshindwa. Nguvu zake zimeshindwa. Yesu alifanya “sufuri” ndani yake. Amevuliwa silaha, akalemaa na kutiwa fedheha hadharani.

Aliwekwa Patupu

Waebrania 2:14b Ili kwa njia ya maui amharibu yeye aliyekuwa na nguvu za mauti, yaani, Ibilisi.

Hatutashindwa kamwe tunapopigana na Shetani na pepo zake. Tumepewa uwezo juu ya nguvu zote za adui.

Tunapoingia katika vita, lazima tuanzie mahali pa ujasiri katika hakikisho na imani kuwa tutashinda. Ni sharti tuingie vitani tukisimama kwenye ufahamu sisi ni nani ndani ya Yesu. Tusije tukapanga kumenyana na adui mwenye nguvu sana. Bali sisi, badala yake, tutazamie mbele kwa furaha ushindi tunapoonyesha kuwa Shetani tayari ameshindwa.

➢ Shetani si "hoja sana"

➢ Yesu ni "**Hoja Sana"!**

➢ Tunaweza kufanya mambo yote katika yeye.

Wafilipi 4:13 Nayaweza mambo yote katika yeye anitiaye nguvu.

HATUA YA USHINDI

Nguvu na mamlaka ya mwamini si kitu cha kuchezea katika kutimiza matakwa yetu binafsi. Lazima tuwe katika makubaliano na mapenzi ya Mungu.

Kukiri Dhambi

Ili tuwe washindi katika vita vyetu vya kiroho, lazima kwanza tutupu na kukiri dhambi zetu kwa Mungu na kupokea msamaha. Mtume Yohana alituambia jinsi ya kufanya hivyo.

1 Yohana 1:9 Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote.

Kukata Kauli

Lazima tuyatoe maisha yetu asili mia moja, kwa Yesu kama Bwana maishani mwetu.

Warumi 12:1,2 Basi, ndugu zangu, nawasihi, kwa huruma zake Mungu, itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai, takatifu, ya kumpendeza Mungu, ndiyo ibada yenu yenye maana. Wala msiifuatishe namna ya dunia hii, bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza, na ukamilifu

Kutengwa na Ulimwengu

Lazima tujitenge na kuhusika na anasa za dunia hii.

2 Timotheo 2:4 Hakuna apigaye vita ajitiaye katika shughuli za dunia, ili ampendeze yeye aliyemwandika awe askari.

Kuweka Kando Tamaa Zetu

Lazima tuweke kando tamaa zetu na kuongozwa na Roho wa Mungu. Sisi, kama Yesu, lazima tuseme, "Mimi ninatenda kile naona Baba yangu akitenda."

Yohana 5:19 Basi Yesu akajibu, akawaambia, Amin, amin, nawaambia, "Mwana awezi kutenda neno mwenyewe ila lile ambalo amwona Baba analitenda, kwa maana yote ayatendayo yeye, ndiyo ayatendayo Mwana vile vile."

Mungu amempa kila mwamini sehemu fulani ya mamlaka juu ya:

- ➢ Ndoa zao, watoto na jamii
- ➢ Mahali wanaishi – ujirani, miji, mataifa
- ➢ Mahali wametumwa na Mungu kuhudumu

Mara nyingi hatutaachiliwa katika roho zetu kuenda vitani dhidi ya ngome za Shetani nje ya sehemu tuliyotengewa na Mungu katika mamlaka. Mungu anataka waamini katika sehemu hiyo wajifunze mamlaka yao na kuzizusha ngome.

Kuwa na Mtazamo wa Upendo

Kama askari, waume kwa wake wenye imani katika jeshi la Mungu, tusiwe na kiburi na tusiowajali wengine.

Filemoni 1:4,5 Namshukuru Mungu wangu sikuzote, nikikukumbuka katika maombi yangu, nikisikia habari za upendo wako na imani uliyo nayo kwa Bwana Yesu na kwa watakatifu wote.

Lazima tumkazie Shetani na mapepo, lakini lazima tutembee katika upendo kwa watu wengine. Tunamchukia Shetani, lakini tunawapenda watu.

Lazima kila mara tukumbuke kuwa mamlaka yetu kama waamini si kuwatawala watu, bali ni kuchukua utawala juu ya Shetani na mapepo zake.

Tunapotembea katika upendo kwa Mungu na watu wengine, tusiwe kila mara tunafikiria juu ya vita dhidi ya Shetani.

Tusiwe na Maridhiano

Tunapotembea katika uhusiano wa karibu na Mungu – bila mchanganyiko wa dhambi, au mambo ya kidunia maishani mwetu – Mungu atatuonya juu ya mipango ya Shetani ili kutushinda kwa kutembea katika vipawa vya kiroho na ujuzu wa kuona mapepo. Kadri tunavyokuwa

karibu na Mungu, ndivyo tunapotambua uwepo wa uovu, hila na mchanganyiko yanapotokea.

Tuyaweke macho yetu kwa Yesu. Ikiwa Shetani na mapepo zake zitasimama mbele yetu – zishughulikie, zipinge, zikemee – kemea mawazo yasiyo ya Mungu. Kisha tuyaweke macho yetu kwa Yesu tukimsifu kwa ushindi.

2 Wakorintho 2:14 Ila Mungu ashukriwe, anayetushangiliza daima katika Kristo, na kuidhihirisha harufu ya kumjua yeye kila mahali kwa kazi yetu.

Hakuna Mtu Spesieli wa Kiroho

Katika ufalme wa Mungu, si mpango Wake kuwa vita vya kiroho na ukombozi vitimizwe kwa kuita, au kuenda kwa, mwenye ujuzi au "mwenye nguvu afukuzaye mapepo". Badala yake, kama mtume Yakobo alivyoandika, kila mwamini sharti ampinge Shetani.

Yakobo 4:7 basi mtiini Mungu. Mpingeni Shetani, naye atawakimbia.

SILAHA YA MUNGU

Mungu ametoa kwetu silaha kwa ajili ya vita tunavyopigana. Mtume Paulo hakuandika kuwa tuvae silaha yetu; aliandika kuwa tuvae silaha ya Mungu.

Wakati jeshi la zamani walivaa silaha zao, na chapeo na kufunika nyuso zao, wote walionekana kama jeshi lenye nguvu, misuli, na hatari kwa adui. Bila kujali upungufu wa mwili ulio ndani ya silaha, walionekana kama jeshi kuu.

Tunapovaa silaha ya Mungu, tunaonekana tu kama Mungu mbele ya Shetani. Kisha yote tunayoweza kufanya ili kushinda vita ni kuongea kama Mungu, kutembea kama Mungu, na kutenda kama Mungu!

Nguvu Zetu

Ni lazima tuende katika nguvu za Mungu. Tusije tukaingia vitani kwa nguvu zetu.

Waefeso 6:10,11 Hatimaye, mzidi kuwa hodari katika Bwana na katika uweza wa nguvu zake. Vaeni silaha zote za Mungu, mpate kuweza kuzipinga hila za Shetani

Vita Vyetu

ms. 12 Kwa maana kushindana kwetu sisi si juu ya damu na nyama, bali ni juu ya falme na mamlaka, juu ya wakuu wa giza hili, juu ya majeshi ya pepo wabaya katika ulimwengu wa roho

Paulo anatukumbusha kuwa vita vyetu si dhidi ya mwili na damu, bali ni watawala, mamlaka, na uovu wa jeshi la

mapepo. Vita vyetu si katika dunia hii ya kawaida, bali katika ulimwengu wa kiroho.

Silaha Zetu

- ➢ ***Ukanda wa Ukweli***
- ➢ ***Dirii ya Haki***
- ➢ ***Miguu ya Injili***

ms. 13-15 Kwa sababu hiyo twaeni silaha zote za Mungu, mpate kuweza kushindana siku ya uovu, na mkiisha kuyatimiza yote, kusimama. Basi simameni, hali mmejifunga kweli viunoni, na kuvaa dirii ya haki kifuani, na kufungiwa miguu utayari tupatao kwa Injili ya amani.

Paulo alirudia neno "simama" mara tatu. Kwanza alisema kuwa siku ya uovu ikija, tutaweza kusimama. Kisha akasema kuwa baada ya kufanya yote, lazima tusimame. Mwishowe, akasema, simama imara basi na dirii ya haki mahali pake, na miguu yetu iwe na utayari wa njili ya amani.

Ukweli ni Neno la Mungu. Ili liwe ulinzi kwetu, ni lazima tufahamu kile linasema.

Dirii yetu ya haki ni haki ya Mungu. Hatuitajiki kuwa kamili, lakini tunaitajika tusiwe na dhambi-ijulikanayo maishani mwetu ili dirii hii iwe kwenye nafasi yake.

Miguu yetu iwekwe na utayari wa injili ya amani. Utayari ni kazi yetu na hufanyika kwa kujifunza Neno la Mungu.

Paulo aliandika kwa Timotheo:

2 Timotheo 2:15 Jitahidi kujionyesha kuwa umekubaliwa na Mungu, mtenda kazi asiye na sababu ya kutahayari, ukitumia kwa halali neno la kweli.

- ➢ ***Ngao ya Imani***
- ➢ ***Chepeo Cha Wokovu***
- ➢ ***Upanga wa Roho***

Waefeso 6:16,17 ... zaidi ya yote mkiitwa ngao ya imani, ambayo kwa hiyo mtaweza kuizima mishale yote yenye moto ya yule mwovu. Tena ipokeeni chapeo ya wokovu, na upanga wa Roho, ambao ni neno la Mungu.

Inatupasa kutumia ngao ya imani ili kuizima mishale ya Shetani. Mishale ni mawazo, majaribu, magonjwa na mbinu zingine Shetani anarusha kwetu. Lazima tuzisime kwa imani katika Mungu na imani katika Neno Lake.

Chapeo ya wokovu huvaliwa tunapopata wokovu. Huu ni wokovu ambao kando na kutuhakikishia uzima wa milele, pia huturejesha kwa vyote tulivyoumbwa tuwe tulipoumbwa kwa mfano Wake. Chapeo ya wokovu

hutuhusu kuyafanya mawazo yetu upya katika ufunuo wa wokovu wetu kamili.

Warumi 12:2a Wala msiifuatishe namna ya dunia hii, bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu.

Kufanya upya mawazo huja kwa kuyaosha mawazo yetu kwa "maji" yaishiyo ya Neno la Mungu tunapolisoma, kujifunza na kulitafakari.

Waefeso 5:26 ... Ili makusudi alitakase na kulisafisha kwa maji katika neno...

Tumepewa silaha moja ya kinga na mbayo ni upanga wa Roho ambalo ni Neno la Mungu. Paulo anatueleza zaidi juu ya upanga wa Roho katika kitabu cha Waebrania.

Waebrania 4:12 Maana Neno la Mungu li hai, tena lina nguvu, tena lina ukali kuliko upanga uwao wote, ukatao kuwili, tena lachoma hata kuzigawanya nafsi na roho, na viungo na mafuta yaliyomo ndani yake, tena li jepesi kuyatambua mawazo na makusudi ya moyo.

Neno la Mungu ni ukanda wa kweli, mavazi ya miguu yetu na upanga wetu! Je, pana tashwishi yoyote juu ya umuhimu wa kulisoma Neno?

Maombi ya Ushindi

Mara kwa imani, tunapovaa silaha kamili ya Mungu, inatupasa kuomba katika Roho nyakati zote.

Waefeso 6:18 ... kwa sala zote na maombi mkisali kila wakati katika kuwaombea watakatifu wote.

Tunapoendelea kuomba kwa imani kwa wateule wote, tukitumia mamlaka yetu, tutaona ngome za Shetani zikianguka. Tutakuwa washindi katika vita na kupinga nguvu za Shetani.

Waebrania 11:33,34 ... ambao kwa imani walishinda milki za wafalme, walitenda haki, walipata ahadi, walifunga vinywa vya samba, walizima nguvu za moto, waliokoka na makali ya upanga, walitiwa nguvu baada ya kuwa dhaifu, walikuwa hodari katika vita, walikimbiza majeshi ya wageni.

KUTAYARISHWA KWA KAZI YA HUDUMA

Yesu alisema tuenende ulimwenguni kote na kuhubiri habari njema.

Marko 16:15 Akawaambia, "Endeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe."

Isaya alinena juu ya wale walioleta habari njema.

Isaya 52:7 Jinsi ilivyo mizuri juu ya milima Miguu yake aletaye habari njema, Yeye aitangazaye amani, aletaye habari njema

ya mambo mema, Yeye autangazaye wokovu, Alumbiaye Sayuni, Mungu wako anamiliki!"

Paulo anatueleza kuwa sisi ni zaidi ya washindi na kuwa hakuna kitakachotutenga na upendo wa Mungu.

Warumi 8:37-39 Lakini katika mambo hayo yote tunashinda, na zaidi ya kushinda, kwa yeye aliyetupenda. Kwa maana nimekwisha kujua hakika ya kwamba, wala mauti, wala uzima, wala malaika, wala wenye mamlaka, wala yaliyopo, wala yatakayokuwapo, wala wenye uwezo, wala yaliyo juu, wala yaliyo chini, wala kiumbe kinginecho chote hakitaweza kututenga na upendo wa Mungu ulio katika Kristo Yesu Bwana wetu.

Yesu anatwambia kuwa tokea nyakati za Yohana Mbatizaji hadi sasa, ufalme wa Mungu unaendelea kwa nguvu.

Mathayo 11:12 Tangu siku za Yohana Mbatizaji hata sasa ufalme wa mbinguni hupatikaka kwa nguvu, nao wenye nguvu wauteka.

Paulo anatwambia kuwa nguvu hizo ni imani!

Waebrania 11:33 ...ambao kwa imani walishinda milki za ufalme, walitenda haki, walipata ahadi, walifunga vinywa via samba.

Kwa Kumalizia

Kazi ya Yesu imekamilika!
Amemshinda Shetani
na kurejesha vyote
Shetani alivyonyakua kwa Adamu na Hawa

Amerejesha mamlaka hapa duniani
na kumkomboa mwanadamu
kwa wale ambao ni
kanisa Lake – Jeshi Lake kuu!

Sasa ni juu yetu!
sisi ndio tunapeleka ujumbe
wa wokovu huu mkuu kwa dunia nzima.

Tunatakiwa kuendeleza kwa bidii
ufalme wa Mungu..

Tunatakiwa kuwafanya maadui
wa Yesu miguu ya kiti Chake.

Tunatakiwa kuenda katika mamlaka
hapa duniani,
leo!

Mistari ya Kukariri

Waefeso 6:12	**Kwa maana kushindana kwetu sisi si juu ya damu na nyama, bali ni juu ya ufalme na mamlaka, juu ya wakuu wa giza hili, juu ya majeshi ya pepo wabaya katika ulimwengu wa roho.**
1 Petro 5:8,9	**Mwe na kiasi na kukesha, kwa kuwa mshitaki wenu Ibilisi, kama samba angurumaye, huzunguka-zunguka, akitafuta mtu ammeze. Nanyi mpingeni huyo, mkiwa thabiti katika imani, mkijua ya kuwa mateso yale yale yanatimizwa kwa ndugu zenu walioko duniani.**
Yohana 10:10	**Mwivi haji ila aibe na kuchinja na kuharibu, mimi nalikuja ile wawe na uzima, kasha wawe nao tele.**
Mwanzo 1:26	**Mungu akasema "Na tumfanye mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu, wakatawale samaki wa baharini, na ndege wa angani, na wanyama, na nchini yote pia, kila chenye kutambaa kitambaacho juu ya nchi."**
Mwanzo 3:15	**Nami nitaweka uadui kati yako na huyo mwanamke, na kati ya uzao wako na uzao wake, huo utakuponda kichwa, na wewe utamponda kisigino.**
Waebrania 2:14	**Basi, kwa kuwa watoto wameshiriki damu na mwili, yeye naye vivyo hivyo alishiriki yayo hayo, ili kwa njia ya mauti amharibu yeye aliyekuwa na nguvu za mauti, yaani Ibilisi.**
1 Yohana 3:8	**Atendaye dhambi ni wa Ibilisi, kwa kuwa ibilisi hutenda dhambi tangu mwanzo. Kwa kusudi hili Mwana wa Mungu azivunje kazi za Ibilisi.**
Wakolosai 2:15	**Akiisha kuzivua enzi na mamlaka, na kuzifanya kuwa mkogo kwa ujasiri, akizishangilia katika msalaba huo.**
Ufunuo Wa Yohana 1:18	**Na aliye hai, nami nalikuwa nimekufa, na tazama, ni hai hata milele na milele. Nami ninazo funguo za mauti na za kuzimu.**
Waefeso 1:22,23	**Akavitia vitu vyote chini ya chini ya miguu yake, akamweka awe kichwa juu ya vitu vyote kwa ajili ya kanisa, ambalo ndilo mwili wake, ukamilifu wake anayekamilika kwa vyote katika vyote.**
Wakolosai 1:13	**Naye alituokoa katika nguvu za giza, akatuhamisha na kutuingiza katika ufalme wa Mwana wa pendo lake.**
Warumi 16:20	**Naye Mungu wa amani atamseta Shetani chini ya miguu yenu upesi.. Neema ya Bwana Yesu Kristo na iwe pamoja nanyi. Amina.**

Luka 10:19	**Tazama, nimewapa amri ya kukanyaga nyoka na nge, na nguvu zote za yule adui, wala hakuna kitu kitakachowadhuru..**
Mathayo 16:18,19	**Nami nakuambia, Wewe ndiwe Petro, na juu ya mwamba huu nitalijenga kanisa langu, wala milango ya ya kuzimu haitalishinda. Nami nitakupa Wewe funguo za ufalme wa mbinguni; na lo lote utakaliolifunga duniani, litakuwa limefungwa mbinguni; na lo lote utakalolifungwa duniani, litakuwa limefunguliwa mbinguni.**
Ufunuo Wa Yohana 12:11	**Nao wakamshinda kwa damu ya Mwana-kondoo, na kwa neno la ushuhuda wao, ambao hawakupenda maisha yao hata kufa.**
1 Yohana 2:13,14	**Nawaandikia ninyi, akina baba, kwa sababu mmemshinda yule mwovu. Nimewaandikia ninyi, watoto, kwa sababu mmemjua Baba. Nimewaandikia ninyi, akina baba, kwa sababu mmejua yeye aliye tangu mwanzo. Nimewaandikia ninyi, vijana, kwa sababu mna nguvu, na neno la Mungu linakaa ndani yenu, nanyi mmemshinda yule mwovu.**
Wafilipi 2:9,10	**Kwa hiyo tena Mungu alimwadhimisha mno, akamkirisha mno, akamkirimia jina lile lipitalo kila jina, ili kwa jina la Yesu kila goti lipigwe, la vitu vya mbinguni, na vya duniani, na vya chini ya nchi.**